

Yaliyomo ni kazi za Jim Harries alizoandikwa tangu mwaka wa 2006 mpaka 2019. Maandishi yake yanaangalia sana utumizi wa lugha kwa huduma ya Ukristo kwa bara la Afrika. Anataja mada mengine pia; utume, mafunzo ya Biblia, utamaduni wa Kiafrika, maendeleo, uchawi, nk. Alipendelea ayaweke maandishi yake pamoja ndani ya kitabu kimoja. Jim anatumaini maandishi yake yatakuwa himizo kwa wenyeji wa Afrika ya Mashariki kuandika maono ambayo wamepewa na Bwana, na yale waliojifunza kulingana na huduma yao.



Jim Harries anajulikana pia, akiwa Kenya, kwa jina la Jacob Otieno. Alikuwa kuishi Afrika (Zambia, halafu Kenya) 1988 kutoka Uingereza. Jim anafunza Neno la Mungu kupitia Kiswahili na Dholuo, akitembelea makanisa mbali mbali, hasa eneo la Siaya, Kenya. Amefunza pia kwa shule ya Biblia za Kanisa la Mungu, Kima, Kenya, na Babati, Tanzania. Jim hajaoa, lakini watoto yatima wanaishi pamoja naye kwa nyumba anayokodesha kijijini. Jim alipata shahada ya PhD Uingereza mwaka wa 2007. Hiki ni kitabu chake cha kumi kuchapishwa. Maandishi yake mengi yanahusika na jinsi inafaa

kufanya kazi ya Bwana kwa bara la Afrika. Jim anafanya huduma yake akiwa chini ya Kanisa Orthodox la Koptiki. Kutoka Uingereza anatumwa na Kanisa la Baptisti.

ISBN 978-3-86269-176-0

ISSN 1436-0292 (World of Theology Series)



sponsored by:




Verlag für Kultur und Wissenschaft
(Culture and Science Publ.)
Dr. Thomas Schirmacher

Jim Harries
Jarida juu ya Maisha ya MwAfrika katika huduma ya Ukristo

World of Theology Series 14
VKW

Jim Harries

Jarida juu ya Maisha ya MwAfrika katika huduma ya Ukristo



World of Theology Series 14

Jim Harries

Jarida juu ya Maisha ya MwAfrika katika huduma ya Ukristo

World of Theology Series

**Published by the Theological Commission
of the World Evangelical Alliance**

Volume 14

- Vol 1 Thomas K. Johnson: The First Step in Missions Training: How our Neighbors are Wrestling with God's General Revelation
- Vol 2 Thomas K. Johnson: Christian Ethics in Secular Cultures
- Vol 3 David Parker: Discerning the Obedience of Faith: A Short History of the World Evangelical Alliance Theological Commission
- Vol 4 Thomas Schirrmacher (Ed.): William Carey: Theologian – Linguist – Social Reformer
- Vol 5 Thomas Schirrmacher: Advocate of Love – Martin Bucer as Theologian and Pastor
- Vol 6 Thomas Schirrmacher: Culture of Shame / Culture of Guilt
- Vol 7 Thomas Schirrmacher: The Koran and the Bible
- Vol 8 Thomas Schirrmacher (Ed.): The Humanisation of Slavery in the Old Testament
- Vol 9 Jim Harries: New Foundations for Appreciating Africa: Beyond Religious and Secular Deceptions
- Vol 10 Thomas Schirrmacher: Missio Dei – God's Missional Nature
- Vol 11 Thomas Schirrmacher: Biblical Foundations for 21st Century World Mission
- Vol 12 William Wagner, Mark Wagner: Can Evangelicals Truly Change the World? How Seven Philosophical and Religious Movements Are Growing
- Vol 13 Thomas Schirrmacher: Modern Fathers
- Vol 14 Jarida juu ya Maisha ya MwAfrika katika huduma ya Ukristo

Jim Harries

**Jarida juu ya Maisha ya MwAfrika
katika huduma ya Ukristo**

Verlag für Kultur und Wissenschaft
Culture and Science Publ.
Dr. Thomas Schirmmacher
Bonn 2019

Bibliographic information published by the Deutsche Nationalbibliothek

The Deutsche Nationalbibliothek lists this publication in the Deutsche Nationalbibliografie; detailed bibliographic data are available in the Internet at <http://dnb.d-nb.de>

© Copyright 2019 by
Verlag für Kultur und Wissenschaft
(Culture and Science Publ.)
Prof. Dr. Thomas Schirmacher
Friedrichstraße 38, D-53111 Bonn
Fax +49 / 228 / 9650389
www.vkwonline.com / info@vkwonline.com

ISSN 1436-0292
ISBN 978-3-86269-176-0

Printed in Germany

Cover design:
HCB Verlagsservice Beese, Friedensallee 44, 22765 Hamburg, Germany

Production:
CPI Books / Buch Bücher.de GmbH, 96158 Birkach
www.cpi-print.de / info.birkach@cpi-print.de

Publishing Distribution Center:
SCM-Verlagsgruppe
D-71087 Holzgerlingen, Tel. 07031/7414-177 Fax -119
<https://haendler.scm-verlagsgruppe.de>
catalog for book stores:
www.vkwonline.com

Private costumers: in any book store or at www.vkwonline.com

Iliyomo

Iliyomo	5
Utangulizi	9
1. Kumbe, Maneno yanayo Umbol!	11
Hitimisho	14
2. Uvumbuzi wa Isimu Amali – kwa Wajaluo, Kenya uhusiano wa lughu na utamaduni wake	15
Hitimisho	24
Bibliografia	24
3. Mzungu alisema, Mwafrika alisema: sera za lugha zinazotakikana kanisani kwa Bara ya Afrika	27
Hitimisho	32
Bibliography	33
4. Pasipo Kujua Mila yake Huwezi Kujadiliana na Mtu Barabara	35
Utangulizi	35
Lugha iwe sawa/moja	36
Wadukizi na Wasikilizaji Wasioonekana	36
Kujitakia Hali, au Siasa	38
Hali ya Mawazo	39
Hitimisho	39
5. Jiwe lililochongwa bila kazi ya mikono: injili ilivyo leta mapinduzi kwa waganga	41
Mathayo 2	41
Kutoka 22:18	42
1 Samueli 28	42
2 Wafalme 25	43
Yeremia 29	43
Danieli 2	44
Hitimisho	46
6. Mitume wa KiAfrika wawe wasikivu – majibu kwa upinzani wa utume wenye usikivu	47
Mafupisho	47
Maelezo juu ya Maneno	48
Utangulizi	48

1. Kumtaka mtume awa masikivu, je, ni kupita kiasi?.....	49
2. Mitume ni watumishi wa waliowatuma, au ni watumishi wa Mungu?.....	51
3. Jinsi watu watakaomfahamu mtume.....	52
4. Uhusiano kati ya mali na watu: urafiki au uadui.....	53
5. Mtume kuwa na usawa na wenyeji.....	55
6. Mitego iloyopo, na jinsi kuihepa.....	56
7. Uajibikaji uzidi kukaswa.....	57
8. Kufanya huduma na mitume na wamisionari wengine.....	58
Kwa Ufupi na Hitimisho.....	60
7. Kiingereza ni lugha itakayotuokoa? Kiingereza siyo lugha ya Mungu.....	63
Mafupisho.....	63
Utangulizi.....	63
Wanaojua Kiingereza ya Asili wako mbele.....	64
Biblia.....	66
Wanao haribu umoja wa Watu.....	68
Kiingereza ya asili kipambau mbele.....	70
Mizizi ya Lugha imo penye jamii, na siyo kwa mashirika.....	71
Lugha zote siyo Sawa.....	71
Wenyeji waliohusika na usambaji wa Kiingereza.....	73
Wanafunzi pia wana uchungu juu ya kutawaliwa kwa lugha geni?.....	73
Kiingereza kama lugha ya Mungu.....	74
Hitimisho.....	76
Bibliography.....	77
8. Maendeleo ya Kiroho: kulisaidia kanisa kujitegemea na kujiepuka na utegemeo wa nje usiofaa.....	81
Somo la kwanza – Umuhimu wa uaminifu.....	81
Mwalimu kujieleza Maneno ya utangulizi.....	81
Mafunzo juu ya Uaminifu.....	81
Somo la Pili – Wafu hulala.....	83
Somo la Tatu – Bidii isitokee penye Ushirikina.....	83
Somo la Nne – Sherehe.....	84
Somo la Tano – Mijadala: juu ya sherehe.....	86
Somo la Sita – Debate: asili ya hela inayofaa.....	86
Somo la Saba – Mijadala.....	86
9. Masuhulisho ya hali za kulaumiana na kushitakiwa wachawi bara la Afrika.....	87
1. Utangulizi.....	87
2. Kifo na Maafa, lazima isababishwe na mtu fulani.....	88

3. Mpaka Utubu	92
4. Upekee wa Injili	93
5. Kazi ya Dini	95
6. Tamaa	96
7. Uoga wa nchi za Magharibi wa ukweli wa Mungu	99
8. Hitimisho.....	100
Bibliography	101
Sources:.....	105
Chapter 1	105
Chapter 2	105
Chapter 3	105
Chapter 4	106
Chapter 5	106
Chapter 6	106
Chapter 7	106
Chapter 8	107
Chapter 9	107

Utangulizi

Yaliyomo ni kazi za Jim Harries (ambaye pale Kenya anapoishi na Wajaluo pia anajulikana kwa jina la Jacob Otieno). Ni kazi alizoandika tangu zamani (miaka 2006) mpaka mwaka huu. Alipendelea ayaweke maandishi yake pamoja ndani ya kitabu kimoja. Jim anaishi Siaya, Kenya. Huduma wake ni kufunza Neno la Mungu kwa makanisa mbali mbali.

Lengo linakuwa kuwapa motisha wasomi wenzake pia waangalie mada muhimu inaohusika na maisha ya Ukristo bara la Afrika wakati huu. Ukiwa na maandishi kama hayo, au ukiwa na mpango kuyaandika, muelezee Jim Harries (jim@vulnerablemission.org) ili tusaيدiane kazi zetu zichapishwe, ndivyo tupate kutangaza kile Mungu anachotufunulie kwa wengine pia. Maandishi yawe kwa lugha ya Swahili, au lugha zingine za KiAfrika.


Iliomo, maandishi moja mpaka nne, ni mijadala juu ya utumizi wa lugha kati ya nchi za Magharibi na Afrika. Maandishi hayo yanaeleza ugumu uliopo ambao wengi, wanaodhania wanaweza ,kutafisir tu' hawafikirie. Sura ya 5 inafafanua Biblia ili kutufahamisha hali inayohitajika kufahamu uchawi. Sura ya 6 inaeleza umuhimu wa *vulnerable mission*, na jinsi kuitekeleza. Kiswahili inayotumika kutafsiri *vulnerable mission* ni utume masikivu. Sura ya 7 inaeleza tena jinsi ni kosa kutegemea lugha ya Kiingereza kwa wasio Waingereza, au watotowao. Sura ya 8 ni tofauti kidogi; ni kosi ya kuwafunza wachungaji. Sura ya 9 inafafanua aina ya theologia inayowezakusaidia kupunguza hali ya uchawi bara la Afrika.

I. Kumbe, Maneno yanayo Umbo!

Tutajifunza jinsi kulifahamu neno kuwa na umbo kitatusaidia kutafakari juu ya maneno juu ya Mungu na ya theologia.


Nitaanza kusema, maneno kazi yao ni kuyagusa masikio, na kupitia masikio ubwongo mwa mtu. Pasipo kutambuliwa ubwongoni, tunaweza sema neno halitakuwa na mstuko, kama Elezo 1.

Elezo 1. Eneo la kustushwa na watu wote wakati wote wa dunia mzima




Halafu kati ya hayo uwezekano wa mstuko wote, neno fulani litalistua sehemu ndogo ya eneo kwa jumla.

Elezo 2. Eneo linaloweza kustushwa na neno fulani (nyekundu)



Angalia jinsi neno moja linaweza kustua maeneo mbali mbali – neno moja linaweza kuwa na maana zaidi ya moja. Tunaweza kuyaunganisha maeneo ya kustuka ya neno, ili neno liwe na umbo lake binafsi:


Elezo 3. Mstuko wa neno fulani ukionganishwa



Eneo linalo stushwa na hilo neno ni ndogo sana likilinganishwa na eneo kwa jumla.


Hata ikiwa eneo linaloweza kustushwa kwa watu wote duniani ni kubwa sana, eneo la kila mtu ni sehemu tu la lile eneo kwa ujumla.

Elezo 4. Eneo la kustushwa la mtu moja (rangi ya majani mabichi) kama sehemu la eneo la kustushwa na watu wote



Neno linalo gusa nje ya eneo la kustushwa la mtu (kwa mfano A) halitakuwa na maana (mstuko) kwake.¹ Neno likiwa ndani kabisa la eneo litakuwa na mstuko sawa (B). Neno likiwa nusu ndani na nusu nje, litakuwa na mstuko nusu (C).

Elezo 5. Matokeo ya eneo la kustushwa kwa maneno hayo A, B na C.




A		→	<input type="text"/>
B		→	<input type="text"/>
C		→	<input type="text"/>

Neno A linaonekana limepotea kabisa, sababu huyu mtu hakuwa na ufahamu wo wote juu lake. Neno la B limepokewa sawa na vile lilivyo tajwa. Neno la C limepokewa tofauti kabisa na vile lilivyo tajwa.

Kwa mfano, tunaweza kulinganisha eneo la kustushwa la Mmasai na Mkisii (kulingana na utamaduni wao) na mstuko wa neno moja, *mahindi*, kwao.

¹ Ukweli ni, itakuwa na mstuko fulani, lakini sitaongea juu yake hapa leo.

Elezo 6. Mstuko kwa Mmasai (kushoto) na Mkisii (kulia) la Neno la 'Mahindi'



Kufuatana na hiyo hali (inayosababishwa na Mmasai kuwa mfugaji lakini Mkisii kuwa mkulima) neno mahindi linalo umbo tofauti kwa Mmasai na Mkisii hivyo:

Elezo 7. Neno 'Mahindi' linalopokewa na Mmasai (A) na Mkisii (B)

A 


B 

Tunaweza kujiuliza je, mahindi ni neno moja kwa Mmasai na Mkisii? Kwa kiasi ndiyo. Lakini kwa sehemu kubwa, kulingana na mstuko wa hilo neno, la!

Sasa tufikirie pande wa theologia na kazi za kanisa. Nataka kulichunguza neno moja, *Takatifu*, kulinganisha lugha tatu *Kimombo*, *Kiswahili* na *Kiluo*.

Holy kwa Waingereza halimaanishi kitu kilicho takaswa, au mwanga, lakini linaonekana kumaanisha kitu chenye mashimo! *Ler* linamaanisha safi na mwanga pamoja na *utakatifu*. *Takatifu* linamaanisha utakatifu, na pia kitu kilichotakaswa. Kwa hivyo haya maneno yanaweza chorwa hivyo:

Elezo 8. *Takatifu* kwa *Kiswahili*, *Kimombo* na *Kiluo*



Itafahamika kwamba eneo la 4 peke yake inakuwa sawa kwa hayo maneno yote.² Tukitafsiri *holy* na *ler* yanaongezeka mambo mengi ambayo mnenaji anawezakuwa hayajui. Na kadhalika. Utofauti wa aina hio wa maneno ukiongezwa na utofauti utakaokuwa kati ya eneo la kustushwa la watu mbali mbali, na kutafsiri neno linalopoteza maana zaidi ya maana yanayosafarishwa, hali ambayo inafanya ukalimani ufanane na uharibifu, au ujangaji upya!

Biblia inatuhimiza ili tuwe na upendo sana (1 Yohana 4:21). Hasa kwa ndoa. Lakini ndoa ya Kiafrika imekuwa na uwezekano wa kuoza Mke wa pili au zaidi kuongezeka – hali inayofanya heshima na hata uoga uwepo badala ya upendo. Kujaribu kuurekebisha upendo uliopo kwa ndoa ya Afrika ili ufanane na upendo wa ndoa za Wazungu mara nyingi inafanya iwe rahisi kwa nyumba kufunjika. Tufanyeje?

Wazungu wanao shida tofauti. Biblia inatuhimiza ili tuombe Mungu mtu akiugua (Yakobo 5:14), lakini Wazungu wanakimbia haraka kwa madawa na matibabu ya hospitali. ‘Maombi’ kwao ni neno linalokuwa na umbo tofauti na hili neno kwa Waafrika, na kibiblia. Tufanyeje?

Hitimisho

Matatizo haya yanarifanye nifikie kauli kwa kusema – theologia na mipango ya maisha ya Wakristo lazima ifanywe kutumia lugha ya watu wanaotumia maishani mwao, sababu kuchanganya kutachanganyika kweli!

² 1 inakuwa kwa Takatifu peke yake. 2 inakuwa kwa Ler peke yake. 3 inakuwa kwa Holy peke. 4 kwa wote tatu. 5 kwa Takatifu na Holy. 6 kwa Ler na Takatifu. 7 kwa Holy na Ler.

2. **Uvumbuzi wa Isimu Amali – kwa Wajaluo, Kenya uhusiano wa lugha na utamaduni wake**

Nilipoishi Zambia miaka 1988 mpaka 1991, nilishangazwa kwa matumizi ya Wazambia ya lugha ya Kiingereza. Mara nyingi maneno walioyatumia hayakutosha kunifahamisha maana ambayo walilenga. Nilijiuliza, hilo ni jambo gani? Je, Wazambia ni wabaya ambao hawapendi kuongea ili waweze kueleweka au ni mimi ambaye sijafahamu mambo yao? Niligundua kwamba lazima kosa lilikuwa langu. Lazima nijitolee ili niwaelewe.

Baada ya kuondoka nchini Zambia, kuanzia 1993 mpaka sasa nimekuwa nikiishi Yala, Gem, kwa Wajaluo wa Kenya. Ninaishi kijijini nikifanya kazi ya kanisa. Tunao mpango wa mafunzo ya Biblia hapo Yala. Pia ninafundisha katika chuo cha Kima International School of Theology, Bungere, chini ya *Church of God*.

Pamoja na kufundisha Biblia nimejitolea ili nijifunze Kiswahili na *Dholuo*. Mambo mengi ambayo ninayataja kuwahusu Wajaluo na lugha yao haimaanishi kwamba yanahusika na *Dholuo* peke yake, ila *Dholuo* ni lugha ambayo nimeweza kujifunza kwa undani kiasi fulani. Hapo nimepata changamoto kubwa sana. Ninawashukuru watu ambao wamenisaidia kujifunza lugha zao, na pia kwa kiasi fulani mila na desturi zao. Kwa makosa yeyote yanoyojitokeza sasa, simlaumu ye yote ila ni yangu tu.

Mnamo mwaka wa karibuni utafiti wangu ulinifanya nichunguze semantiksi, ili nijisaidie kufahamu juu ya lugha na maana yake. Nilistaajabu nilivyo soma maandishi ya Kempson juu ya nadharia ya semantiksi (1977): “... *there is almost no aspect of semantics with which there is any degree of certainty*” (p184) anaandika Kempson. (Hatuwezi kuwa na uhakika na karibu mambo yoyote kwa somo la semantiksi.) Njia ya kugundua maana ya sentensi ni kusema “*S is true only if P*” (23), S ikiwa sentensi, na P ikiwa sharti linalouhakikisha ukweli wa sentensi. Kwa hivyo tunaweza kusema “majani ni mabichi (S) ikiwa majani ni mabichi (P).” Niligundua kumbe kuchunguza semantiksi haitakuwa na msaada sana kuniwezesha kukamilisha lengo langu la kuwafahamu Waafrika ili kazi yangu ya kufundisha Biblia iwe ya maana. Lakini, Kempson anatuelekeza kwa isimu amali (*pragmatic linguistics*) au ‘matumizi ya lugha’ (Kempson 1977:47).

Nilianza kugundua kwamba maana ya lugha inatokea kufuatana na utumiaji wake! Jinsi lugha inavyotumiwa, na mahali au muktadha wake

unachukua sehemu kubwa kuhusu uvumbuzi wa maana. Nilijichorea ifuatavyo:

Fonetika → syntaksi → semantiksi → amali
(phonetics) → (syntax) → (semantics) → (pragmatics)

Uvumbuzi wa maana ya utamshi fulani unategemea kwa kiasi kubwa sana eneo na muktadha wake. Sasa, muktadha unapobadilisha, je maana yanakosakufahamika? Hapo ndipo panaweza kuwa mwanzo wa jibu la swali kubwa langu!

Ni Grice ambaye anakubaliwa kuwa moja wa waanzilishi wa mijadala juu ya amali ya lugha (Levinson 1983:16). Grice aliunda nadharia ya *cooperative principle* – sheria ya msingi inayofuatwa ili watu wawasiliane barabara. Aliunda sheria yake kwa sehemu nne:

- 1) (*Quantity*) – mtu ataeleza mambo ya kutosha na sio zaidi.
- 2) (*Quality*) – mtu ataongea kitu cha kweli.
- 3) (*Relation*) – anachoongea mtu kitahusisha wasikilizaji.
- 4) (*Manner*) – jambo litajadiliwe kwa uwasi.

Leech (1983) alianza kupinga msingi uliowekwa na Grice. Sisi leo tutamfuata sana Leech, sababu anaeleweka wasi kwa jinsi anagawa mambo ya Grice kwa masehemu.

Lengo langu ni kuonyesha jinsi matumizi ya Wajaluo kwa lugha yao (*Dholuo*) haufuatani na sheria za Grice, na vile hali hio inafanya kusikilizana kati ya Wajaluo na wenye asili cha Kiingereza lazima kuwe ngumu.

Mjaluo anaishi kwa dunia pamoja na wafu (*juogi / jochiende*). Kwa ufahamu wake, hawa wafu (mizimu) wanaweza kuwa wana sikiliza mijadala yo yote inayoendelea. Kwa hivyo mjadala unaonekana kuwa kati ya watu wawili (yaani *dialogue*) unasikilizwa na watu wengi (yaani *polylogue*; Kerbrat 2004). Swali ambalo wengine wanaweza kuuliza “*are the spirits real*” ni duni. Mjaluo anajua wapo. Pia, wengi wao hupenda kuleta uovu. (Shuguli ya mjaluo pande ya *juogi* na *jochiende*, zaidi siku hizi, ni kujikinga nao. Maana yake, wanaonekana kuwa waovu.) Uzuri sasa unafahamika unatoka kwa Nyasaye (Mungu) na maisha ya kisasa.

Egner alishangaa kwa matumizi ya lugha ya watu wa Ivory Coast (Egner 2002). Anaeleza jinsi mtu mmoja alimwahidi atakuwa naye kwa sherehe fulani, lakini pia siku ile alikuwa amepanga kuwa kwa mji mwingine mbali na hapo. Ni kama ahadi yake ilikuwa bure kabisa. Egner anajaribu kueleza jinsi kufanya ahadi kwa Waafrika maneno lazima yarudiwa maradufu (Egner 2002). Lakini Mhogolo anatumia “kwa ... mtu mgeni, mtu

(Mwafrika) akaweza akamwambia vingine ambavyo si kweli ama uongo” (1985:64). Kwa hivyo, matumizi ya lugha kwa Mwafrika sio lazima utaje ukweli kwa mgeni. Mwafrika pia hapendi kumwambia mtu ‘la’ uso kwa uso. Afadhali aseme ‘ndio’, hata ikiwa anajua atashindwa kutekeleza jambo hilo. Kukataa katakata maneno yanayo ongolewa kwa lengo nzuri ni kukosa heshima. Kwa njia ingine tena tunaweza sema *abiro biro* (‘nita kuja’) kwa *Dholuo* inafaa itafsiriwe kwa Kiingereza kuwa ‘*I would like to come*’ na sio ‘*I will come*’.

Wengine wanaweza kusema, Wajaluo siku hizi wameshawachana na imani yao ya awali ya *jochiende* na *juogi*. Hata ikiwa hivyo, lazima tuendeleo kujjuliza ikiwa njia ya matumizi wa lugha unaweza kubadilisha mara moja watu wakisema wamewachana na ushirikina? (Mara nyingi ninasikia Mwafrika mweusi hawezi kuwachana na imani yake kwa nguvu ya mizimu, lakini sasa tuseme hata ikiwezekana.) Je, mazoezi ya matumizi ya lugha haitaendelea? Ni rahisi mtu kusema ‘simwogopi simba’, lakini akijikuta anavamiwa na simba, je hatakimbia? Hivyo ndivyo wale wanaokataa imani kwa Mungu wakiwa mahututini. Hivyo ndivyo wanaokataa hawaamini kwa uwezo wa Wafu.

Mtu moja akibadilisha hali yake kuongea, mara moja hatafahamikwa na wenzake. Kwa hivyo uzozi wake utaendelea kumwongoza. Kwa hivyo, kubadilisha kwa hali ya eneo na imani (dini) ya Mjaluo haitaleti mabadiliko kwa matumizi wa lugha yake mara moja.

Nilipokuwa ninatembea kwa barabara ya Maseno-Kisumu kabla haijatangenezwa juzi, niliweza kushangaa gari inapokuja kutoka mbele vile mara moja inageuka na kutuelekea kamili kwa kufuata pande yetu ya barabara. Tulipofika hapo mahali pa kisa hiki, shimo kubwa barabarani ilionekana wazi. Hivyo ndivyo mtu anaweza kuitumia lugha kwa njia ya kutofahamika kwa mtu ambaye hajaona shimo, yaani mzimu.

Mbali na CP (*co-operative principle*), ni rahisi kwa Mjaluo kusema kitu ambacho sio ‘kweli’. Hivyo atakuwa anatumia lugha ili ajihepe na uovu fulani unao mwelekea. Mifano, ipo kueleza hali hiyo kwa kitamaduni ya Wajaluo. Inasemekana Mzee Mjaluo anajaribu kutumia njia tofauti kila siku kutoka na kurudi nyumbani (Mboya 1978:np). Anafanya hivyo ili mtu asimwekee dawa njiani mwake ambayo itamuumiza. Tena mwanamke mwenye *kisoni* (watoto wake wana kufa wakiwa bado wadogo) anaponywa kwa kumdanganya pepo wenye kifo ili atambue mtoto ameshaaga – halafu amwache bila kumsumbua. Pepo anadanganywa kwa kumpelekea mtoto msituni na kumwacha hapo kwa muda kidogo, mtu akipiga sauti ya fisi. Hivyo pepo wa kifo anaenda kwake na anamwacha mtoto aishi. Kwa hivyo Mjaluo anatumia lugha kumdanganya pepo (km *jachien*), maneno yakiwa kweli au la. Tena hivyo mazingira ya mtu yanatengenezwa kupitia kwa

matumizi ya lugha! (Ifahamikwe hapa lugha ni chombo cha uundaji na sio uelezo peke – Steiner 1998:275).

Kwa hivyo Mjaluo anafahamu amepewa lugha yake ili aitumie kujikinga na uovu – bila kujali ikiwa anachosema ni kweli au la.

Austin alikiita kitabu chake *Doing Things with Words* (1962). Anaeleza humo jinsi maneno mengi yanatumiwa sio kueleza kitu bali *kufanya* kitu, Mambo ambayo Wajaluo wamekuwa wameyafahamu tayari kwa miaka mingi. Maneno yanaweza kutumiwa kuwadanganya au kuwafurahisha mizimu kwa faida ya mtu mwenyewe.

Leech anatuambia kufuatana na CP watu huongea na *informativeness required* (kuyaeleza mambo kwa kiasi yanavyohitajikwa). Hapa tunaweza kujjuliza, yanayohitajika ni yapi? Leech anafahamu ‘yanayohitajikwa’ ni kulingana na ufahamu wa dunia ambayo yanakuwa haina watawala wengine kama miungu au mizimu, ila watu tu. Tena watu ambao wanalenga kusaidiana. Mambo ambayo yapo tofauti kwetu hapo Luoni.

Nikiwa Luoni, ninavyo mwambia mtu niliona ng’ombe wake sio mzima, atajiuliza kwa nini nimekuwa nimewaangalia ng’ombe wake? Pengine kumbe ni mimi ndiye nimewaroga ng’ombe wake, na sasa ninafurahia kwa balaa yake. Nikiuliza tena ikiwa amefaulu kuwalipia watoto wake karo ya shule, nisipokuwa na pesa kumpa atafikiria ninauliza kwa lengo mbaya. Kwa ujumla tunaweza sema mambo mengi ya maisha ya mtu hayapo wazi kujadiliwa na mtu mwingine asipokuwa mhusika mwenyewe. Hatua moja tu baada ya kuyaficha mambo tuna kuja kwa kutaja uongo juu ya mambo. Kila mtu hana pesa au mali, sababu anaogopa akikubali kuwa nayo yakutosha atarogwa na mwenye wivu.

Watu wengi hawaoni kama ni kosa kuyatumia maneno kuunda hali ambayo ni sawa, na sio kuelezea hali vile ilivyo. Mvulana ambaye anataka kuo kusema ‘hawa ng’ombe ni wangu’, na hata kumwambia mchumba wake anavyo viti, vitanda, pasia na makabati kwa nyumba yake, hahesabiwi mwenye makosa sababu kumbe kitu anachotaka ni kitu kizuri – kumposa msichana. Ni kawaida kwa mtu kujifanya aonekane mtu mzuri na sio mbaya mbele ya watu. Hivyo ndivyo kwa shule yetu ya kitheologia hapo Yala karibu kila mara tukimwongelesha mtu anasema atakuja kuhudhuria mafunzo yetu, halafu haonekani. Kwa kuongea kwake amejifanya aonekane mtu sawa. Amejiokoa kwa hali duni ambayo inataka kumshinda na hajali sana kuwa amevunja CP (*cooperative principle*)!

Tuko mbali na Leech, anayetuambia mtu hatasema kitu bila uthibitisho au uhakika fulani juu ya ukweli wa neno lake. Mara nyingi nimejikuta ninasubiri kitu, kwa mfano basi kufika au stima ambayo imepotea kurudi. Mtu akiniona ninayo wasiwasi, au nikimuuliza mwenzangu atasema ‘basi inakuja saa hii’ au ‘stima iko karibu kurudi’. Kwa ukweli hajui, lakini

anapenda kunihimiza kuliko kukubali ujinga wake na kuniwacha kwa wasiwasi.

Uponyaji tena ni hivyo. Baada ya kumwomba mtu, haifai kusema hali yake bado haijabadilika. Hapana. Unahitajika kusema ‘sasa amepona’, ili maneno yetu yamsaidie huyu mtu ili kweli apona.

Omari (1993) anakubali katakata na hali ya ushirikina wa Watanzania. Iteyo anagundua jamaa ya waafrika wanakubalia kuwepo kwa mapepo (“*incorporeal things*” 2002:150). Ni matokeo ya imani aina hiyo panda ya matumizi ya lugha ambayo ni ngumu kwa mtu kutoka nchi za Ulaya kutambua au kufahamu. Makosa yake mara nyingi ni kutotambua uhusiano wa imani ya ushirikina na jinsi mtu anavyotumia lugha yake.

CP pia inatuambia mtu ata *avoid obscurity of expression*. Je, hii ni sawa kwa bara la Afrika? Amuka (1978) hangeweza kukubali, kwa vile anafafanua njia ya Wajaluo kuongea kupitia kwa *ngeche* (mithali, fumbo au kitendawili). Inaonekana matumizi ya *ngero* unamfurahisha mtu. Hivyo kitu au hali ambayo ilikuwa ya kawaida inachochewa kuwa ya ajabu, ya fumbo, ya kuchekelewa. Maneno yanatumiwa hivyo kuunda hali ingine juu ya hiyo ambayo inaonekana na macho. Kumwambia mtu *mi mana piri* (kaza matako yako) ili umhimize afanye bidii ni kumwongeza hali ya uchanga moto pamoja na furaha moyoni, kupitia kwa *obscurity* (fumbo) mwenyewe!

Kupinga maneno ya Grice na Leech, Sperber na Wilson (nd) wameunda nadharia nyingine ya *relevance*, yaani uhusiko. Wanasema mtu atayafahamu maneno au utamshi kwa kutumia *maximum cognitive effect and minimum processing effort*, yaani wingi wa uhusiano na mawazo ya mtu kupitia kwa ukazo ya ubongo kidogo. Tuseme, maana ya utamshi unaosikika utatambuliwa kwa njia hizo, zinazohusiana na hali ya mtu. Nikiambiwa ‘ameenda’ nikijua daktari wa ng’ombe yuko nitajua huyu ng’ombe aliyekuwa mgonjwa ameaga dunia. Nikiambiwa hivyo baada ya kumsubiri mtu kumsindikiza mtoto wangu shuleni nitajua ni mtoto wangu ambaye ameenda (shuleni).

Sperber na Wilson wanawaandikia watu Waulaya, ambao wanaonekana hawana uhusiano na mizimu / mapepo maishani mwao. Wakielezwa juu ya mambo fulani hali ya uhusiano mawazoni mwao itawaelekeza kisiensi. Kwa mfano, wakiambiwa ‘kiti kimevunjika’ wanaweza kufikiri ‘kumbe chuma kilichotumiwa hakikukuwa kimetengenezwa na nguvu ya kutosha’. Lakini mtu wa bara la Afrika kuambiwa hivyo atajiuliza ni nani aliy sababisha kitendo hicho? Tukiendelea kutafakari juu ya hayo tutagundua kwa kutafuta hali ya uhusiano wenye maana mahali Mgaribi atakapoona siensi, Mwafrika hataiona! Inapotea kwa maandiko!

Hio inatuonyesha vile maandiko ya kisiensi yataweza kufahamikwa kwa Mwaafrika kama yawe ya ushirikina, na hali kadhalika maneno yaliyoandikwa juu ya ushirikina na Mwaafrika yatafahamikwa kwa mtu wa Ulaya kama maneno ya siensi! Amali ya maneno yanayageuza maana yao kabisa! Kiini cha maandiko kinaweza kupotea chupu chupu.

Nadharia inachosema maneno yanatumiwa kukifanya kitu na sio kueleza juu ya kitu, kinahitajika kuchunguzwa zaidi. Austin (Kempson 1977:51) anatuambia kila tamshi la mtu linalo mambo ya *locutionary*, *illocutionary* na *perlocutory*. Kitendo cha *locutionary*, kina kuwa maneno yenyewe. Kitendo cha *illocutionary* kwa hilo tamko kinakuwa nguvu fulani, ikiwa kusifu, kulaani, kupinga nk. Kitendo cha *perlocutionary* ni matokeo yanayotakikana kwa msikilizaji, ikiwa kutahadhari, kutengeneza chai, kucheka nk. Itafahamika kwamba *locution* fulani inaweza kuwa na *illocution* na *perlocution* mbali mbali, kulingana na mazingira. ‘Nimekuona’ linaweza kuwa ya maana ‘asante kwa kujifichua’, linaweza kuwa onyo ili usiibe, au furaha sababu nimekuwa kipofu kwa muda mrefu! Kulitaja hilo neno linaweza kukufanya ujitokeze zaidi, uregea mikono yako mfukoni mwako, au uanze kushangilia nami pamoja.

Uchunguzi bado unahitajika hapo, lakini ninatumaini tumetambua uhusiano kubwa sana hapa wa maneno na mazingira au hali ya matumizi yao.

Kuna neno kwa Kiingereza la *politeness*. Neno linalo weza kwa *Dholuo* kulinganishwa nalo pengine ni *luor*, lakini ufananishi ninaoona haupo sana. (‘Mos’ au ‘muol’ yanazeza kutafsiri ‘polite’, lakini tena yapo mbali kiasi.)

Ila, neno hili la *politeness*, linaonekana lina umuhimu sana kwa Kiingereza, mpaka vitabu vimeandikwa juu yake, kwa mfano katibu cha Brown na Levinson, (1987). Hawa husema “the most subtle differences in ... pragmatic features of a linguistic variety are sufficient to engender mismatches in perceived politeness.” Yaani utofauti kidogo kwa isimu amali unaweza leta hali ya kutoongea na heshima (*politeness*) ambayo inatarajiwa. Lakini lengo la *politeness* ni kupunguza hali ya kuonekana mwenye ukatili. Maana yake, mtu asiyefahamu matumizi ya lugha yenye *politeness* (*luor* / heshima) hatawezakujenga uhusiano mzuri na watu, ambao watamdhania mkatili.

Mijadala imekuwa mingi juu ya *luor* au heshima. Mimi ninataka kusema msingi wake kwa sisi Luoni ni uoga wa vitendo vya wafu wakijisikia wanakosewa. Hali hiyo inayomsingi tofauti sana na hiyo ya *politeness* ya Kiingereza. Maana yake, mambo ya kujifunza aina ya *politeness* / *luor* (*heshima*) kwa mwenye Kiingereza akitaka kujua *Dholuo* (au lugha zingine za Afrika), au Mjalujo kujifunza ili afahamu matumizi ya Kiingereza ni

nyingi sana, na yaumuhimu sana, na ambayo hayafunzwi shuleni. Pasipo hayo, uhusiano wa karibu ambao unahitajika (kwa mfano) ili kufanya kazi pamoja, haumo.

Je, tunataka kujaribu kuwafunza watu *politeness* kwa matumizi ya Kiingereza, ambayo ni lazima tukitaka kuwasiliana kwa karibu na Wazungu kutoka nchi za nje? Au, tuendeleo kufunza Kiingereza ambacho hakitaweza kuleta uhusiano? Au tufanyeje kwa hayo?

Karibu na *politeness* ni *face-saving*. Ninavyoona mwenyewe tena, haupo sana kwa Wajaluo wala Waafrika. Kwa mfano, nikihitaji kuenda shuleni, na mvua inanyesha na wewe una gari, Kiingereza kinachotumiwa kwa Ulaya kina weza kuwa “*you wouldn’t mind giving me a lift would you?*” (je, hungeweza kutojali kunipa ubebaji au?) ili mtu asiabishwe akikataa. Lakini ninavyo sikia utumiza wa lugha kwa Kenya inakuwa “*give me a lift*” (beba mimi). Lakini sheria za *luoro* kwa Waulaya hawajui. Wanaweza kumwita mzee mheshimiwa “Bob” badala ya “Mzee” (Sir), mwalimu ‘*hi mate*’ nk.

Ogot anajadiliana sana juu ya hali ya usawa na hali tena ya utofauti kati ya Waafrika na watu wa Ulaya (Ogot 1999:79-88). Ogot anamaliza akisema hakuna kitu kama hali ya kipekee ya mawazo ya Mwafrika.

Bila kukosa kumheshimu Ogot, pengine kitu ambacho hakukitambua ni wenye mawazo ya kipekee sio Waafrika, ila Wazungu wa Ulaya wa magharibi! Historia inatuonyesha vile walipitia kwa mambo mengi kama ya *enlightenment* na *age of reason* (kwa mfano angalia Cragg, 1960) ambayo imewapa mawazo tofauti na watu wengine wote duniani mzima na kwa historia yote. Wanaolenga kuwaiga au kuwafahamu hawa watu (Wazungu) wanajitakia kazi ngumu mno. Hata Waafro-america wameshindwa kiasi kubwa kufanya hivyo, na wanaishi kwa nchi ya magharibi kama raia! Afadali kujiheshimu mwenyewe, kujifunza kwa wengine, lakini sio kujaribu kukuwa kama hao – kitu ambacho hakitawezakuwa rahisi. Kila watu ni tofauti, na mambo yanayowafanye vile walivyo ni mengi na aina ya kushindwa kufahamishwa.

Kusikiliza wakati wakalimani wanafanya kazi yao kinaweza kumfaidi mtu sana. Ninavyowasikiliza wenye kutafsiri *Dholuo* mpaka Kiswahili, ninaweza kushangaa. Kwa kweli maneno kadhaa ya *Dholuo* hayawezi kutafsiriwa kata kata. Badala yake *jachien mar homa* inakuwa tu ‘homa’, *chike mag dala* inakuwa ‘mambo’, *dala doho* inakuwa boma kubwa nk.

Ukweli wa mambo ni ukalimani unapoteza mambo mengi. Kwa njia ingine ukalimani ni uundaji, wa kitu kipya kabisa. Maana asili yakitafsiriwa na kusikilizwa na watu ambao hawaifahamu mila ya asili, yanapotea. Badala yake wanasikia juu ya ‘wageni’ hawa kama kundi la watu wao wenye hali ya juu wa ujinga! Wenye lugha na mila ya Kiingereza wakisikia ukalimani

wa *Dholuo* wataweza tu kuwagundua Wajaluo wakiwa aina ya watu wao. Hivyo ndivyo tena kwa Mjaluo akiwasikiliza juu ya watu wa Ulaya.

Sababu za hiyo kutokea ni nyingi, zingine ambazo zimeelezwa hapo juu. Mimi ninavyoona, kwa kiasi kubwa Mwingereza hawezi kumfahamu Mjaluo, na hivyo tena Mjaluo Mwingereza – kupitia kwa lugha peke yake! Kutoweza kumfahamu, maana yake ni kutomfahamu au kumfahamu kwa njia bure au mbaya. Ili uwafahamu watu lazima uishi nao! Waafrika (Wajaluo) wameunda mawazoni mwao vile wanafikiri juu ya Wazungu, ambao sio kikamilifu, na huo uundaji ambao haupo, ndio wanajaribu kuiga!

Ukalimani unawezekana tu kwa kiwango ambacho mila za lugha zote zinakuwa sawa. Pasipo hiyo – kiasi kikubwa ni uundaji.

Mimi mwenyewe nimekitafsiri kitabu cha Paul Mboya cha *Luo Kitgi gi Timbegi* (Wajaluo na Mila na Kitamaduni vyao) (1983). Baadaye nikagundua – Waingereza watakao soma utafsiri wangu hawataweza kufurahi na vitendo vya Wajaluo, jinsi msomaji Mjaluo anayeweza kufurahi. Ili kitabu kiwafurahishe Waingereza hivyo kinafaa kiandikwe juu ya “mila na desturi ya *Waingereza!*” Hii ni hali ya ukalimani ambayo unawezafaa!

Mfano wa ukalimani mbaya kwa mambo ya kanisa ni huo unayoitwa kwa Kiingereza *prosperity gospel*. Kuyatafsiri haya maneno kwa lugha za Kiafrika ni ngumu au hata hakiwezekani. Tukijaribu tunawezapata *injili ya maendeleo*, au *injili ya ufanisi* au *injili ya mali ya dunia*, ambayo inasikika tofauti sana na hiyo ya Kiingereza na kwa urahisi inapendeza!

Kwa hivyo ukweli wa mambo ni, utafsiri mbali mbali huthibitisha mambo ya uundaji ambao sio wa kweli, yaani *inventions!* Mkalimani anayefaa ni huyo ambaye ameshaishi na kuonja maisha ya ndani pande zote. Yaani, Mwafrika ambaye ameishi na Wazungu kwao au Mzungu aliyeishi kwa urefu na Waafrika kwao. Kawaida Waafrika wakienda Ulaya huishi shuleni, au na Waafrika wenzao, na Mzungu akija Afrika hivyo tena; anaishi na Wazungu wenzake mjini au kwa *mission station*. Anayeweza kufahamu pande zote mbili pia anayekazi ngumu zaidi, ambaye pengine hata itamshinda kutekeleza: kuwathibitishia watu juu ya kitu ambacho hawaoni na macho (ya nje au ndani) yao sio rahisi.

Kwa hivyo kwa hali tunayo sasa, ukalimani unadumisha ujinga mwingi.

Nikiongea juu ya ukalimani wenye ujinga, ninamaana pia Mwafrika anayesoma Kiingereza, au Mwingereza anayeweza kusoma lugha ya kiafrika, ambaye hajaweza kujiingiza kwa ndani kwa mila yao. Tuchukuwe mfano wa Mjaluo anayesoma Kiingereza. Kabla hajajifunza (kupitia kwa mazoezi na siyo darasani ambayo hayawezekani) hali ya maisha mengine, lazima atafsiri kila kitu anachosoma kulingana na mila na kitamaduni chake. Atawezaje kufahamu kumbe kunakuwepo kitu kingine tofauti na hiki

ambacho amekizoea, isipokuwa kina kuwa cha kukosa hekima? Akikubali uzuri wake, anakubali hali ya kujigonga kichwani kila mara; ni kukubali kitu ambacho moyo wake utaendelea kumwambia ni bure.

Kufikiri inakuwa kupitia kwa kujifunza lugha darasani mtu ataweza kuifahamu lugha kutoka mila ya ugeni kabisa, ni kujidanganya kwa hali ya juu. Kuifahamu lugha bila kujua juu ya matumizi yake ni kujifunza tena lugha ya tatu ambayo sio yako, sio ya mgeni, lakini ingine tofauti tena na ya kipekee. Tuseme ni sheng au *pidgin* ambayo kuisikia ungefikiri ni Kiingereza.

Nadharia ya Whorf (*Sapir-Whorf hypothesis*) imechunguzwa sana na wanaisimu (angalia Anon:nd). Je, lugha inamwundia mtu ufahamu wake wa dunia? Mjaluo ambaye hana neno kulitafsiri *challenge* (changa moto), je, hana changa moto? Mwingereza ambaye hana neno *okola* ni sababu sio lazima kuridhiwa kwa wajane wake?

Sina nafasi kuchunguza hayo maswali kwa ndani wakati huu. Ila nina-weza sema bila shaka Mwingereza ambaye anajifunza *Dholuo* anaingiza hali ya mila, kitamaduni na lugha zake kwa ufahamu wake wa *Dholuo*, na kadhalika Mjaluo anayejifunza Kiingereza. Kujifunza lugha haiwezi mara moja kubadilisha ufahamu wa mtu kwa dunia na binadamu (*worldview*), kwa hivyo *strong Whorfianism* (ushikishaji kwa nadharia ya Whorf sana) ninaona haiwezekani. Tena, mtu anaweza kuongea Kiingereza na sarufi yake safi sana, na bado kuwa mjinga kwa mila na kitamaduni cha Waingereza. Hivyo ndivyo kwa Kijaluo pia, ila sio rahisi kujifunza Kijaluo bila kuishi na Wajaluo na hivyo pia kuanza kuifahamu mila yao.

Maneno mawili yanaweza kuwa na maana sawa, lakini bado uzani ya haya maneno yanaweza kuwa tofauti. '*Min David*' (mama wa David) na '*min Elizabeth*' (mama wa Elizabeth) ni mtu moja mwenye watoto wawili. Kwa ukalimani atawezaitwa pengine '*Mildred*', jina ambalo halielezi yoyote juu ya watoto wake. (Ukimtafsirie Mwingereza '*mother of so and so*' msikilisaji ataweza kuchanganikiwa sababu gani kumwita na jina la mtoto wake?) Tena, maana yanapotea kwa ukalimani.

Ninashangaa ninavyo fikiria juu ya jinsi watoto WaAfrika wanavyo elimishwa na lugha geni kama Kiingereza, nikifikiria juu ya mambo aina hiyo ya hapa juu. Mimi ninadani kufahamu mambo yo yote ya ndani kwa masomo yao lazima kiwe kigumu. Ninashtuka pia ninavyoenda kutembea Ulaya – kukuta mashule ambayo yanafunza mambo yanayoenda (kwa ujumla) sambamba na maisha ya wanafunzi walioko. Kuenda shuleni ni kama mwongezo kwa mambo ya kawaida – na siyo mstuko ambao unampoteza au changanya mtu yanapogongana na hekima ya nyumbani.

Mwanafunzi anayetamani kuenda mbele hawezi kujali sana ikiwa mambo anayofunzwa hayalingani na mazoezi ya maisha yake, ikiwa

itampa cheti ambacho baadaye kitamsaidia kupata kazi na riziki yake. Mambo anayofunzwa yanawezakuwa kama akiwatambikia mizimu – hata asipo fahamu mambo muhimu ni nguvu inayotokea kufuatana na maneno yake. (*Abbra kadabra kadoo ...* hayana maana lakini yanafanya mlango ufunguliwe)!

Kwa kiasi panda ya semantiksi, na zaidi kwa isimu amali, Kenya inayo Viingereza viwili vinavyotumiwa kwa wakati na mahali moja. Hivi ni Kiingereza cha rasmi kinacho andikwa kwa kamusi (zinavyo toka nchi za nje, zaidi ninavyoona kamusi za Oxford), na Kiingereza cha Kenya ambacho kwa sehemu kubwa inatumia kulingana na lugha za watu wa asili.

Hitimisho

Utafiti wa isimu amali ambao unajaribu kuchunguza lugha ambazo sio za Ulaya bado haijafanywa sana (Hinnekamp 1995:15). Pengine inafanya huo utafiti wangu uwe mbele?

Ikiwa uvumbuzi wangu ni sawa, lazima mambo ya lugha yaendeleo kufikiriwa sana. Kupitia kwa utafiti wangu mimi mwenyewe ninazidi kufahamu ugumu unaokuwepo kwa kufanya utafiti kwa watu ambao sio ‘wako’. Pia kuona jinsi usomi wa mataifa unachanganya kwa kiwango cha kulazimishwa uchunguzi sana ili kuongezekwa na ujuzi ambao ni sawa kwa mtafiti. Mtafiti lazima afikirie sana juu ya mambo yanayoandikwa juu akitaka kusoma au kusikia na kufahamu mambo kutoka kwa mtu mwenye mila tofauti na yake.

Moja ya hali ambayo ni msingi wa utofauti kati ya Kiingereza na Dholuo, ni maelekeo ya Wajaluo wa Kenya kwa kifo na wafu, ambayo ni tofauti sana na hiyo ya Waiingereza wengi sana.

Hali aina hizi ninaona ni muhimu zaidi kwa kanisa na somo ya theologia. Haya masomo yanafaa yawe yamoyoni mwa ndani. Mambo ya moyoni mwa ndani hayawezi kujengwa pasipo uhusiani mzuri kati ya lugha na mila yake.

Bibliografia

AMUKA, PETER SUMBA OKAYO,

1978 ‘Ngero as a Social Object’ A thesis submitted in partial fulfillment for the degree of Master of Arts in Literature at the University of Nairobi

ANON,

(nd) *The Sapir - Whorf Hypothesis* <http://venus.va.com.au/suggestion/sapir.htm/> [www]

- AUSTIN, J.L.,
1962 *How to Do Things with Words* Oxford: Clarendon Press
- BROWN, PENELOPE and LEVINSON, STEPHEN C.,
1987 (1978) *Politeness: Some Universals in Language Usage* Cambridge: Cambridge University Press
- CRAGG, GERALD R.,
1960 *The Church and the Age of Reason 1648-1789* Middlesex: Penguin Books
- EGNER, INGE,
2002 *The Speech Act of Promising in an Intercultural Perspective* SIL International URL: (8-01-03) <http://www.sil.org/silewp/2002/001/silew P2002-001.pdf>
- HINNENKAMP, VOLKER,
1995 'Intercultural Communication' 1-21 In: Verschueren, Jef, Ostman, Jan-Ola and Blommaert, Jan, (eds) *Handbook of Pragmatics* 1995 Amsterdam / Philadelphia: John Benjamins Pub. Co.
- ITEYO, CRISPINOUS,
2002 'An Analytical study of the Doctrine of Materialism, with Reference to Selected African Conceptions of Reality' A thesis submitted in fulfillment for the degree of Doctor of Philosophy of Maseno University
- KEMPSON, RUTH. M.,
1977 *Semantic Theory. Cambridge Textbooks In Linguistics* Cambridge: Cambridge University Press
- KERBRAT-ORECCHIONI, CATHERINE,
2004 'Introducing Polylogue' 1-24 In: *Journal of Pragmatics* 36(2004) [PDF] www.elsevier.com/locate/pragma (03.12.03)
- LEECH, GEOFFREY H.,
1983 *Principles of Pragmatics* London and New York: Longman
- LEVINSON, STEPHEN C.,
1983 *Pragmatics: Cambridge Text Books in Linguistics* Cambridge: Cambridge University Press
- MHOGOLO, GODFREY M.,
1985 *Endelea Kukua Muadili ya Kristo* Dodoma: Central Tanganyika Press

MBOYA, PAUL,

1978 *Richo ema kelo Chira* Nairobi: East African Publishing House
(referring to my translation into English)

MBOYA, PAUL,

1983 *Luo Kitgi kod Timbegi* Kisumu: Anyange Press

OGOT, BETHWELL A.,

1999 'Racial Consciousness among Africans' 79-88 In: Ogot, Bethwell A., *Reintroducing Man into the African World. Selected Essays, 1976 - 1980* Kisumu: Anyange Press Ltd.

OMARI, C.K.,

1993 *Uchawi na Ushirikina* Mwanza, Tanzania: Inland Publishers

SPERBER, DAN and WILSON, DEIRDRE,

and *Relevance Theory* [www] http://www.dan-sperber.com/relevance_theory.htm (21-01-03)

3. Mzungu alisema, Mwafrika alisema: sera za lugha zinazotakikana kanisani kwa Bara ya Afrika

Siku moja nikiwa Zambia, nilipokuwa mwalimu wa shule ya upili, niliweka tangazo fulani kwa sehemu ya taarifa za shule. Baada ya siku mbili nilipitia hapo na Walimu wenzangu Wazambia wawili. Niliona mtu mwingine alishafunika karatasi yangu kwa kuweka karatasi yake juu ya yangu. Nilivyowaelezea wenzangu, wakacheka. Nilifikiri – kwa nini wanacheka kwa kitendo kibaya kama kile? Niligundua kwamba hata ukitumia lugha moja, bado jinsi inatumiwa inaweza kuwa tofauti. (Kwetu Ulaya mtu hangalicheka, angalisema pole na jinsi inatajikana hali irekebishwe.)

Nilipofika Zambia mara ya kwanza, nikaanza miradi mbali mbali ya ukulima hapo shuleni. Wazambia wenzangu walifurahie kuona maendeleo shambani. Lakini pia ilionekana kwa ufahamu wao ya kwamba miradi itaendelea tu nikiwepo au Mzungu mwingine akija kuiendeleza. Nilianza kuona hio dalili mahali popote nilipoenda. Nilitafuta piki piki ili nitembe nifanye uchunguzi zaidi. Sio miradi yangu midogo shuleni tu, lakini miradi mikubwa katika sehemu mbali-mbali ilikuwa inafanya kwa muda kidogo, lakini Wazungu walipoondoka miradi ikaanguka. Kufungwa kwa miradi yote hapa KIST mwaka uliopita (2005) inaonyesha hali ile ile ngumu pia hapa Kenya.

Watu hupenda kutoa sababu mbali mbali kueleza kutofaulu kwa miradi. Wengine husema ni ukosefu wa rasilimali. Huu ni ngumu kuamini vile pesa nyingi imemwagwa kwa bara ya Afrika na shirika mbali mbali za misaada. Wengine hutaja bahati mbaya, ufisadi, vifo vingi, hali ya hewa, kuwepo vita, ukosefu ya elimu n.k. Lakini sababu aina hizo kweli zinaharibu hii miradi yote? Hali ingine ya msingi inajificha na maneno aina hayo. Kwa nini miradi ya kuendeleza uchumi wa Kiafrika mara nyingi inakwama?

Tuangualie upande wa kanisa. Siku moja nilipokuwa Zambia niliambiwa ‘Mwafrika hawezi kuhubiri vile Mzungu anayehubiri.’ Baada ya miaka kadhaa nilipokuwa Kenya niliambiwa ‘Mzungu hawezi kuhubiri kama Mwafrika.’ Nilipuuza kwanza. Inawezekanaje Mungu kutofanya kwa njia sawa na hawa wote? Baada ya muda hapa Kenya, nilitambua ni kweli. Pengine sio haiwezekani kabisa, lakini ni ngumu sana. Tena inafanywa kupitia kwa uigaji. Nimeona pia Mwafrika akienda kuhubiri Ulaya. Waingereza hushangaa kwa urahisi; sio rahisi kuyafahamu maneno yake. Hapa Afrika mara nyingi Watu wanakuwa tayari kulisikiliza Neno la

Mzungu ikiwa Mhubiri anatumia lugha ya pesa. Pesa isipokuwepo kugawanya wakati ule anapohubiri, lazima asisitize maneno yake kupitia kwa mali yake kwa njia ngine. Wacha ajaribu kazi yake bila ugawanyaji ya fedha na bila kutumia lugha ya ugeni ambayo inataminikwa, na tuone.

Badala ya kusaidia, mara kwa mara mhubiri mgeni Mzungu analeta vita na ugawanyiko kanisani. Anawapa watu uamuzi ngumu – fuata Mungu na umaskini, au tii maneno yake na pokea mali. Haya yamewaangusha watumishi wengi wa ukweli wa Mungu. Huo ni uharibifu moja unaotokea tukimruhusu mgeni kutumia mali yake kulazimisha maneno ambayo hayalingani na mila iliyopo.

Mara nyingi nimejikuta katikati ya shida hii. Maana yake; mgeni kutoka Ulaya anaongea na kiongozi wa kanisa hapa Kenya, nikiwa ninasikia. Mgeni huyu Mzungu anavyoongea, ninayafahamu shabaha yake sababu mimi pia nimetoka mahali ametoka. Ninagundua pia vile Mwafrika akimsikia anakosa kumfahamu barabara. Halafu Mwafrika akiongea (tuseme anatumia Kiingereza pia) ninaweza fahamu kitu anacholenga zaidi ya huyu Mzungu sababu nimeishi hapa kwa miaka nyingi. Lakini jibu la Mzungu linaonyesha kukosa kufahamu kwake. Hivyo ndivyo mijadala inaendelea.

Ubaya ni; sio rahisi kuwasaidia hawa watu wawili. Kuwaambia hawasilizani barabara ni kuwakwaza. Mwafrika anaogopa kupotezwa kwa pesa ambayo anatarajia. Mzungu hawezi kubali hali ya kuwa mjinga na kutoweza kumwelewa mtu ambaye anatumia lugha yake (yaani Kiingereza).

Ninaweza toa mifano jinsi ufahamu unakosekana. Mwafrika akisema mkutano wa kesho yake utakuwa saa mbili, inafaa Mzungu aambiwe ‘10.00am’ na siyo ‘8.00am’. Mwafrika akisema ‘nitakuja kesho’ inatakatika Mzungu aambiwe ‘engine nitakuja kesho.’ Mwafrika akisema ‘tunayo shule za Biblia’ inafaa Mzungu aambiwe ‘tunataka utujenge shule ya Biblia’ (au hospitali, nyumba ya kutunza na kulea yatima, miradi n.k.).

Kujaribu kutatua kwa nini watu wawili wanaotumia lugha moja hawawezi kusikilizana barabara, kilinifanye nitafute kitabu juu ya semantiksi. Hio nilifahamu ilikuwa masomo juu ya jinsi maneno yanakuwa yanamaanisha kitu. Nilishangaa kwa ugumu wa kuhakikishia maana ya neno fulani. Kusema ‘majani ni mabichi’ ni sawa ikiwa ‘majani ni mabichi’ anasema Kempson (1973:24). Kumbema semantiksi peke yake haienzi maana! Kempson alinielekeza kwa masomo ambayo wakati ule wa 1973 yalikuwa bado mpya, yaani ya *isimu amali*.

Kuchunguza isimu amali kulinisaidia kufahamu jinsi maana yanatokea kwa kiasi kubwa kwa *mazingira* na hali ya *utumizi* wa neno fulani. Kwa mfano, nikisema ‘leta nguo’ ninaweza maanisha: a/ Ninasikia baridi. b/ Ile

nguo ni yangu. c/ Ninataka kukuwekea hiyo nguo. d/ Ninataka ubaki uji. n.k. n.k. Hayo maneno ‘leta nguo’ yanaweza kuwa na maana nyingi sana kushinda kuhesabiwa. Kila mara mazingira na mbinu wa utumizi wa maneno inageusha hivyo ndivyo maana ya hayo maneno.

Hii ni sababu Mwingereza anafahamiana na Mwingereza mwenzake kwa kiasi ambacho anakuwa sawa kwa mazingira au ufahamu wa msingi wa maneno yake. Mwingereza akiongea anaongea akidhania mazingira na historia fulani katika kila neno analotaja. Ataweza kuwafahamisha tu wengine kwa kiasi ambacho hawa pia wanayafahamu mazingira ambayo anakuwa nayo mawazoni (kichwani) akiongea. Hivyo ndivyo pia kwa Mwafrika anayeongea. Asipojua vile mazingira na asili ya hayo maneno inakuwa, mtu hataweza kuyafahamu maneno. Hivyo ndivyo tunaweza sema ukalimani hauwezekani.

Hauwezekani pengine sababu hamna maneno kwa lugha inayolengwa. Nikisema ‘*I threw the paper into the bin*’ inaweza kuwa ‘nilitupa karatasi kikapuni’, lakini ukweli ni kikapu na *bin* ni vitu tofauti. Lakini kutowezekana mara nyingi unatokea kwa hali ya isimu amali. ‘Mtu ambaye anaambiwa “njoo hapa haraka’ kwa barabara atahitaji kujua ni nani anamwita kabla hajaitika. Akiwa mzee anayeambiwa hivyo tutashangaa wote, lakini akiwa mtoto mdogo hatutastuka kwa maneno hayo. ‘Nilienda Kisumu kwa gari’ ikitamukwa na mtu ambaye hana mali nyingi, tunafahamu alichukua matatu. Tajiri akisema hayo hayo maneno, tutajua alienda na gari ya binafsi. Utofauti hayo sio kwa maneno, lakini ni nje ya maneno, na kuyatafsiri maneno hakitauelezea.

Kufahamu vile ukalimani unavyobadilisha maana ni muhimu sana ili uhusiano kati ya watu wa mataifa (mila) mbali mbali utawezalainishwa; ikiwezekana! Mifano itafafanua zaidi. ... Kuleta mifano lakini ni ngumu sababu wengi wetu kwa muda mrefu (au maisha yetu mzima) tunakuwa pamoja na watu wa mila fulani moja. Mtu anagundua utofauti wa ndani ya utumizi wa lugha akiweza kuifahamu mila mbili. Wengi wetu hatuna hiyo nafasi. Niruhusu kujaribu kueleza kulingana na mazoezi yangu.

Maneno ya kusema “nimejenga nyumba nzuri” hayatoshi kufahamu vile nyumba yenyewe inayokuwa. Nyumba ya matope moja inaweza kuwa nzuri kuliko nyumba ingine ya matope. MwInuiti akisema amejenga nyumba nzuri, nyumba yake inatengenezwa na barafu. Mfanya biashara penye mji wa New York akisema atajenga nyumba nzuri inaweza kuwa ghorofa ya juu kabisa, sababu New York ni mji wenye magorofa ya juu. Kwa hivyo maana ya hayo maneno “nyumba nzuri” yanategemea mazingira ya utumizi wa maneno.


Swali linakuja sasa kwa elimu kwa jumla. Kinakuwaje elimu ikitolewa nchi moja na kupelekwa sehemu nyingine pasipo na mazingira na mila

ambayo imetegemea kule mahali pa asili? Mfano ninaweza kuchukua ni elimu ya Uingereza na ya Amerika. Nimewasikia Waingereza wengi ambao wanasema elimu ya Amerika haifai kwao na Waamerika wengi ninadani wanahesabu elimu yao kuwa nzuri kulikwo hiyo ya Uingereza. Ikiwa utofauti unaonekana hivi kati ya nchi mbili wenye asili na lugha moja, itakuwaje kuhamisha elimu hiyo kwa watu wenye asili (na lugha) tofauti sana?

Kuihamisha elimu hiyo kutoka kwa watu na mila moja hati kwa watu wa mila na lugha tofauti ni kuifanya elimu ibaki bila mizizi. Vile baisikile bila gurudumu haitembe. Vile mti bila mizizi unakauka haraka sana. Vile kichwa cha mtu pasipo mwili wake ni bure kabisa. Vile nyundo bila mpini wa kugusa inakuwa na faida kidogo sana, n.k.

Tufikirie juu ya Mungu. Watu hufahamuje Mungu? Tuseme pengine Waafrika wanamfahamu akiwa kama nguvu ambayo inapatikana kupitia kwa vitu vingi (k.m. miti, milima, mito n.k.), au hata kila kitu. Hiyo nguvu ambayo ni Mungu inayo uhusiano wa karibu na mioyo ya wafu, pamoja na mioyo ya wenye hai. Tuseme tena Wazungu wanamwamini Mungu akiwa kama Mzee mkongwe ambaye anakaa sehemu za mbingu na ambaye sasa amechoka. Lakini vile watu siku hizi wanafanya na komputa, huyu Mungu wa Mwingereza ameitengeneza dunia ili ikingie 'peke yake.' Tofauti na hizi mbili tuseme ukweli ni katikati – Mungu sio kitu kimoja na dunia, na uhusiano wake na mioyo ya watu na wafu sio karibu kwa kiasi ambacho Waafrika wanaamini. Lakini anahusika na mambo ya kila siku duniani zaidi na vile Wazungu wangetuamini. Basi tunaona mafundisho yanayofaa kwa Mwafrika ili amfahamu Mungu ni kueleza utofauti ya Mungu na dunia, lakini Waingereza wanafaa kufundishwa juu ya hali ya karibu ya Mungu (Mungu yuko karibu nawe)! Kuchanganya hao wawili (km. kumsisitizia Mwafrika vile Mungu ni kama upepo ambao unakuwa kila mahali au kumsisitizia Mzungu vile Mungu hana nguvu kumtajirisha mtu) sio kusaidia ila kupoteza wasikilizaji.

Tunaona juu, ikiwa Mungu ni mmoja, na desturi na hali ya maisha yake ni mmoja, watu ambao wako tofauti lazima wafundishwe kwa njia tofauti.



Pikta 1. Jinsi mafundisho juu ya Mungu yanatajikana kuwa tofauti tukimlinganisha Mwafrika na Mwingereza

Tumeona juu vile neno moja linaweza kuwa na maana nyingi ya aina mbali mbali. Kwa ukweli – maana ya neno ni utumizi wake (Wittgenstein 1989: 42). Maana ambayo neno linaweza kuwa nayo lenye kamusi ni chache tu ukilinganisha na nguvu nyingi aina mbali mbali ambayo inafuruta ‘maana ya utumizi’ wa neno huko na pale. Sababu maana ya neno, hata sentensi, fungu la maneno (*paragraph*) au hata kitabu inabadilika kulingana na mazingira na utumizi wake, mafundisho juu ya Mungu au hata mambo mengine kutoka mbali yanaweza kubadilishwa kabisa na kuhamishwa.

Wazungu wengi siku hizi hawaongee hata juu ya imani yao kwa Mungu. Wengine wanasema hawamwamini Mungu. Hiyo hali ya kushangaza inatokeaje na inadumishwaje? Kwa ukweli, Waingereza wanayo ‘mungu’ mwingine lakini hawamwite mungu! Ila, wanamwita (au wanaiita sababu hawaamini hata yuko hai) *objectivity*. Nilikuja kwa Bara ya Afrika kwanza miaka kumi na nane iliopita. Wakati ule nilijaribu sana kuwafundisha Waafrika (Wazambia) juu ya huyu ‘mungu’. Lakini, sababu hakuna mungu ambaye alikuwa anafanana naye kwa tamaduni yao, sikuweza kuwafafanulia. Lakini huyu mungu anashika sehemu kubwa mno kwa maisha ya Waingereza, mpaka maisha yote yanaelekezwa kulingana na mahitaji yake. Hata wale wanaomwamini Mungu (tuseme Yahweh) wanamlinganisha (au tafautisha) kila mara na huyu mungu mwingine; *objectivity*. Kwa hivyo, haiwezekani kumfahamu vizuri Mwingereza na kufahamu vizuri theologia ya Waingereza pasipo kumfahamu kwanza huyu mungu ambaye anaitwa *objectivity*, kitu ambacho kwa ufahamu wangu ni ngumu sana au hata haiwezekani kwa Waafrika kwa ujumla sababu mila yao haina kitu kama hicho!

Hiyo ni muhimu sana. Mara nyingi wasomi, hata wakiwa Waafrika wenyewe, wanachunguza sana mila na kitamaduni yao, hata wakitumia

Kiingereza. Wengi hawajali kujiuliza kwanza – lakini mizizi ya lugha ya Kiingereza ambayo tunaitumia kila mara, inakuwaje?

Tofauti na Waingereza, Waafrika wanaamini kukuwepo kila mara na kila mahali wasikilizaje na waonaji wa vitendo na mazungumzo yao, ambao ni wafu (waloaga). Kwa majina mengine mapepo, majini, masaitani, mizimu, *demons*, *spirits*, nguvu za giza n.k. Inamchukua Mwingereza muda mrefu kugundua hali hiyo kwa Waafrika wenzake. Hata wakimwambia ni hivyo, hawezi kubali haraka sababu ni kitu chenye ugeni kwake kabisa. Kuwepo kwa hawa mapepo kunamfanya Mwafrika kufikiria sana kwanza kabla hajataja maneno fulani, ikiwa kusikia maneno kwa hawa mapepo kunaweza kumduru kwa njia yo yote maishani mwake. Hapa tunayo asili ingine ambayo inafanya kusikilizana na kufahamiana kati ya Waingereza na Waafrika kuwa ngumu sana. Hiyo pia inaonyehsa vile ukalimani hauwezakani.

Hitimisho

- 1) Kiingereza kweli inawezakana iwe lugha ya Kiafrika. Lakini, shida kubwa sana wakati huu kwa nchi kama za Kenya ni vile hairuhusiwe kubadilisha ili iwe lugha ya Afrika. Badala yake watu wanataka kuitumia Kiingereza ya Ulaya, na hiyo haiwezekani. Kwa hivyo utumizi wa Kiingereza hapa Kenya (Afrika) kwa theologia unaleta uchanganyiko. Hatua moja kubwa muhimu ili kanisa la Waafrika liendelea ni kuwacha kuitumia Kiingereza au lugha na hali ya ugeni kiasi kama hiyo kama lugha rasmi yake. (Inaweza kuendelea kufundishwa, lakini isiwe lugha ambayo inatumiwa kufundisha, kuongoza ibada n.k.)
- 2) Ukalimani sio kazi inaofaa kwa watu wote – k.m. watoto shuleni (ambao siku hizi wanakutana na Kiingereza yenye asili ya ugeni kabisa kwa vitabu vyao na kutoka kwa walimu wao). Watu waerevu (wasomi) ambao wanayafahamu mila ya Kiingereza na ya Afrika wanahitajika watafsiri maarifa kutoka nje ili yaweza kuwafaidi raia wa kawaida.
- 3) Ukalimani bado utakuwa ugeukaji. Maarifa kutoka sehemu mbali mbali duniani kweli yanaweza kutusaidia hapa Afrika, lakini haifai kuwekwa msingi wa elimu au maisha yetu. Lazima msingi ujengwe kwa Mungu, kupitia lugha yetu na mila yetu na kupitia kwa Biblia na historia / mila ya kanisa.
- 4) Waingereza pia lazima watambue haraka iwezekanavyo kusema – *objectivity* sio mungu. Wakiendelea kuchanganya imani ya Ukristo wao na huyu ‘mungu’ wanapoteza wasikilizaji kwa kuwatoa nje ya

ukweli halisi ya Mungu. Wakiendelea kumweka na nguvu huyu 'mungu' yao na mkaso kali vile wanavyofanya wakati huu, matokeo yatakuwa maafa kubwa sana kwa wenyeji wa nchi ambayo siku hizi tunaita 'nchi zinazoendelea.'

Bibliography

Kempson, Ruth. M.,

1977, *Semantic Theory*. Cambridge Textbooks In Linguistics.
Cambridge: Cambridge University Press

Wittgenstein, cited in Hanfling, Oswald,

1989, *Wittgenstein's Later Philosophy*. Basingstoke: Macmillan Press

4. Pasipo Kujua Mila yake Huwezi Kujadiliana na Mtu Barabara

Utangulizi

Kujadiliana, inafahamikwa na wengi, kunaleta ufahamu na usuluhisho wa mambo mbali mbali. Inaaminiwa kuwa hivyo hata kati ya watu wanaotoka kwenye mila tofauti. Ninapinga. Nasema mijadala kati ya watu wenye mila mbali mbali, wasipofahamiana kimila, ni kupoteana. Mara nyingi ni kuachana njia, na sio kufahamishana zaidi. Kwa hivyo mmisionari, ili awafikie watu wenye mila kigeni, lazima ajihusishe na hiyo mila yao, pamoja na lugha yao.

Watu wawili kujadiliana juu ya kitabu fulani kinaweza kuwafurahisha na kuwanufaisha wote wawili; ikiwa wote wawili wamekisoma kitabu kimoja. Lakini ikiwa vitabu walivyosoma vilikuwa tofauti hawataelewana, wasipo tangulia kwanza kufundishana au kurekebisha lile kosa. Wawili wakiongea juu ya mchezo, lakini mmoja juu ya mpira na mwingine juu ya voliboli, hawataelewana. Mmoja akiongea juu ya ufugaji wa kuku na mwingine uchungaji wa ng'ombe, hawataelewana.

Tena watu wawili wakiongea lakini kila mmoja akitumia lugha ambayo mwenzake hajui, kwa mfano lugha mmoja ni Kiluo na nyingine Kiluiya, hawataweza kuelewana. Mluiya akiongea na Mkikuyu ni afadhai sababu hizi lugha zinafanana. Bora kabisa waongee lahaja moja ya lugha moja.

Uelewano unahitaji vitu viwili – lugha iwe moja, na jambo litakalohusika katika mijadala liwe ni moja. Lugha moja na jambo (au mila) tofauti, au mila moja na lugha ikiwa tofauti, na mijadala italeta ufanisi kidogo.

Tufahamu pia; kuelezwa juu ya mchezo au kuambiwa juu ya kitabu fulani, ni tofauti na kuucheza ule mchezo au kukisoma kile kitabu chenyewe. Ni vigumu kuamini mtu anaweza kuwa mchungaji mwema wa ng'ombe kabla hajawachunga hata siku moja. Kwa uhakika – kukifahamu kitu kigeni kinatokea kwa kukifanya au kukiona na macho, na sio tu kwa kuambiwa kuhusu kitu hicho.

Tunaweza kusema mijadala inayonufaisha kawaida inatokea kati ya watu ambao ufahamu wao unalingana. Nataka tuchunguze kwa undani kidogo – hali inakuwaje?

Lugha iwe sawa/moja

Pasipo ukalimani, mjadala unatakiwa uwe katika lugha moja. (Tutaona – hata ukalimani ukiwepo, bado lugha moja itahitajika.) Uchaguzi wa lugha unaonekana kuwa muhimu.

Tutalinganisha Waluyia na Waluo tukiangalia tu maneno mawili – *dala / ingo* (boma) na *kuon / obusuma* (ugali). Tunajua jinsi Waluo wanapanga boma zao tofauti na ujenzi ‘ovyo ovyo’ wa Waluyia.¹ Tuseme (kwa mfano wetu) kuon inatengenezwa kwa mhogo, lakini obusuma kwa mahindi. Tukija sasa kwa uchaguzi wa lugha, tunatakiwa tujiulize maswali mawili: 1/ Lugha gani? 2/ Mila gani? Je, Mluo akiwa kwa Waluyia akiomba obusuma atafahamika, je anauhitaji ugali wa mhogo au wa mahindi? Akisharudi nyumbani akisema anataka kutoa ingo swali litakuwa – atajenga kimpango, au atatengeneza boma ovyo ovyo? Kumbema kitu muhimu sio lugha itakayotumiwa, lakini makubaliano juu ya mila itakayokuwa inafahamika lugha inapotumiwa!

Matatizo bado yanawezakuwepo hata watu ambao wanatumia lugha mbili wakikubaliana kwa mila moja (na wakiwa wanafahamu hiyo mila moja), kwa sababu jinsi vitu vinavyotajwa inategemeana na lugha. Mluo anayezuia kusema apenji (Kiluo: mimi-uliza-wewe) atakutana na kazi ngumu kupata maneno yenye maana moja kwa lugha zingine. Pengine Mluo akisema ‘hebu’ inafahamika kwamba anajaribu kusema apenji? (Ni vigumu kupata mifano ya aina hiyo kati ya Kiingereza na Kiswahili sababu Kiingereza cha Kenya kinafuata sana Kiswahili.)

Lakini, sababu ni mila inayodhaniwa kuwa muhimu hata kushinda lugha inayotumiwa, inakuwaje ikiwa wanaoongea wasipofahamiana kimila? Kusema ukweli, hata wakiwa wanajua ‘lugha moja’, bado hawataweza kufahamiana barabara. Mahali maelewano yanakosekana inaweza kuwa jambo la muhimu. Ugali unaotengenezwa na mhogo ukidhaniwa ni mahindi inaweza kuwa ni sumu. Mluo akitengeneza boma ya ingo badala ya dala itajulikana watu wake wataweza kufa kwa wingi.

Tunaweza kusema nafasi ya kushirikiana kilugha kwa watu wanaotofautiana kimila – ni nadra sana!

Wadukizi na Wasikilizaji Wasioonekana

Dialogue, kulingana na asili yake ya Kigriki, ni maongezi kati ya watu wawili. Kweli maongezi kati ya watu wawili yanaweza kuwa tamu. Lakini je, inawezekana?

Mkubwa wa shamba anaweza kuwa na wafanyakazi wake. Tuseme anamwita mmoja na kumwambia “unahitaji ulale papo hapo kazini” sababu siku hiyo ng’ombe fulani atahitaji msaada wake akizaa. Mfanya kazi atastuka na kujitetea. Ikionekana mkubwa wake hamsikilizi, ataweza sema: “nilimwahidi jirani wangu ili nimsaidie kutengeneza baisikeli ili kesho yake ampeleke mkewe anayeugua hospitalini”. Sasa, mjadala uliyokuwa kati ya watu wawili umehusisha watu watatu, au wanne (jirani na mkewe)! Ili mkubwa aweze kumshawishi mfanya kazi abaki hapo sasa haimhitaji tu kumfahamu mfanyakazi mwenyewe, bali pia wale watu na hali zao.

Hawa wawili wakishaletwa kwa mjadala, sasa itakuwaje kwa wengine? Pengine mke wa mfanyakazi hana ufunguo wa chumba chao cha sitor yao. Pengine mtoto wake alitarajia kupewa pesa ili alipe mtihani, na hiyo ilikuwa siku ya mwisho. Pengine mama mzazi alimwonya kutolala kazini sababu mkewe ni mwenye wivu sana. Lakini pengine baba yake ambaye ni marehemu alimwambia kazi ni maisha ya mtu na lazima iwe kitu cha kwanza kufikiriwa. Hata wafu wanaweza kuhusika katika mjadala ule! Akiwa anaongea na mkubwa wake shetani mwingine (mzimu) anaweza kuja kumwonya asilale hapo au atamwua! Kumbe, mjadala kati ya watu wawili tu, haupo!

Kawaida, nikimfahamu mtu ambaye ninajadiliana naye, na watu wake, na hali na mila yao, sitastushwa sana na hao watu wengine. Lakini nisipowafahamu itakuwa rahisi kwangu kushindwa kufikisha lengo langu (mfanyakazi awe karibu ili amsaidia ng’ombe akizaa) nikiongea na huyu mtu.

Tunaambiwa na watalamu; pesa ambayo inatumwa na wafadhii inatakikana kutumiwa kulingana na matakwa yao. Lakini tunagundua mara nyingi haifanyi hivyo. Kwa nini? Kwa sababu mgeni (Mzungu) anayetuambia kufanya hivyo ni wa hawa, lakini hawa siyo wetu. Tunaweza kusema, Mzungu anapojadiliana ‘wako naye’. Lakini mwenyeji atakaye-chukua uongozi kutoka kwake hatawaona hawa watu, kwa hivyo hatawajali kiasi cha huyu ambaye ni mtu ‘wao’.

Inakuwaje mtu akiwa na uhusiano na mizimu? Wafu huongee naye, wanamsikiliza kwa kila jambo, na wanao uwezo wa kumwumiza! Nadhani itakuwa kama mtu akiwa na wachumba wawili ambao hawajatambuliana, akikutana nao wote wawili sehemu moja. Wasipogundua siri ambayo mzee anajaribu kuficha, watashindwa kuvifahamu vitendo vyake vya kuhepa, kunyamaza, na kuwa na hofu anapojadiliana nao! Au tuseme mnamba wa matatu anamwelezea dereva wake kwa furaha jinsi wanakwepa polisi, na huku dereva anaona polisi akasimama nyuma yake, lakini mnamba hajatambua! Hata mwanafunzi wa KIST akiongea juu ya Mkuu wa chuo,

bila kujua mwenyewe kwamba amekuja na amesimama mlangoni mwa chumba. Mdukizi mwingine ambaye uwepo wake unakubaliwa na kila Mkristo ni Mwenyezi Mungu Yehovah. Uwepo wake ni lazima utaathiri hali za mijadala.²

Kujitakia Hali, au Siasa

Siasa (kushindana kwa uwezo ndani ya jamaa au umma fulani) mara nyingi haipo kwenye maneno, lakini kwa mazingira au muktadha. Bush hajasema anavamia Iraq sababu ya mafuta mengi yaliyomo, lakini bado watu wengi wanaweza kufikiri ni hivyo. Muuzaji halazimishwi kumwambia mteja wake “ninataka nipate mali nyingi iwezekanavyo kwako”, lakini mnunuaji awe macho akienda kununua kikapu sokoni Luanda akiambiwa alipe elfu tano! Mvulana akimpa msichana mandazi hakuna haja ya kumwambia “nina-kuchumbia”. Kwa kawaida mazingira yanatosha kumfahamisha maana ya kitendo.

Uhusiano kati ya makanisa hapa Afrika na ya Ulaya siku hizi unakuwaje? Mzungu akija Kenya akitafuta wachungaji ili ahusiane nao, je, mtamkaribisha kuhubiri kanisani kwako? Ukikutana naye utamwambia kitu utacholenga sana sana ni pesa yake, au utamwambia wewe unahaja na roho za watu sio mali ya dunia? Utamfanya mpaka pesa itoke (wewe usipofanya hivyo mwingine atachukua nafasi hii), na bora ajue ni wewetu unayempenda Yesu kwa ukweli (viongozi wa makanisa mengine wamepotea) inchini. Biblia haielezi jinsi Yesu alivyowafanyia wageni kutoka Ulaya walipofika kwake, lakini kwa sisi ni kawaida, ila hatusemi!

Mtu anaweza kusema kitu bila kugundua. Kuongea sana juu ya chakula mezani magharibi ya Kenya nimegundua kwamba inaweza leta tashwishwi au kukwaza watu. Lakini kufanya hivyo ni kawaida kwa Waamerikani. Wanafunzi wa KIST nimesikia wakijitetea wakimwambia mgeni kutoka Amerikani mama yao anaogua sana na hana pesa ya kulipa kwa ajili ya matibabu hospitali (ili amwombe) walishitakiwa baadaye kwa ajili ya kuomba omba wageni. Mtu akiniambia “mkutano wetu utakuwa ‘saa tatu kamili’” siku hizi mimi nachanganyikiwa tu (sijui utakuwa saa ngapi)! Nikipokea barua pepe inayonitarifu nitapewa Ksh6,000,000, ninahaki nikiwa na shaka sababu kawaida aliyenitumia email anahaja na pesa zangu – lakini hasemi hivyo!

Sababu ubishi mwingi wa siasa haupo kwenye maneno lakini kwa kufahamu muktadha, hayo mambo hayatafsiriwa hata lugha ikitafsiriwa.

Hali ya Mawazo

Kila mtu anakuwa na njia yake ya kipekee kuwaza. Kila mwanaume anajua – yeye ndiye sawa au hata bora. Watu fulani wanao mbinu au mawazo ambayo ni tofauti na watu wengine. Mbinu za kuwaza za watu wanaotoka Ulaya ni tofauti na mbinu za wenyeji wa Kenya. Kwa hivyo mawazo yanayo simamia (kuwa msingi wa) maneno yanakuwa tofauti.

Mtu kutoka Ulaya akisema “mnahitaji maendeleo kanisani” anamaanisha “fanyeni vile sisi tunavyofanya na tulivyofanya, na sisi tutatoa msaada”. Lakini Mkenya ambaye ameishi Kenya (Tanzania, Uganda n.k) hawezi jua jinsi mambo yanavyokuwa kule Ulaya! Yeye anajua maendeleo yanakuja wageni wakija kwa wingi, na yanatokana na baraka. Lakini hatakubali kutofahamu mambo ya Ulaya akihofia ataonekana mjinga, au ule msaada unaweza kutolewa.

Hali kadhalika tukiangalia neno la ‘dawa’. Dawa inatumiwa na mtu akiwa amelogwa, akiwa na *chira* (*chisila*), akisumbuliwa na mapepo au akiwa na bahati mbaya, ili izuie hizo nguvu za uharibifu. ‘Dawa’ ya mzungu inatumiwa kuwapiga vijimelea vidogo sana mwilini ambao hawaonekani hata kwa macho. Ni vitu tofauti sana, lakini jina linalotumiwa ni moja. Kwa hivyo Mtanzania anadhania hata dawa ya mzungu inapiga wachawi, na Mwulaya anadhania dawa ya Kiafrika inawalenga vijimelea hawa kama dawa yake!

Vitu vingine havifikiriwa hata, na haviongelewi. Pale Ulaya hakuna mtu ananiuliza jina la Baba na Babu yangu. Nikiwa Siaya watu huuliziana saa yote! Kuuliza juu ya watoto wa mtu kinaga ubaga ukiwa Ulaya kinaonyesha unawajali, lakini kuthubutu kufanya hivyo ukiwa Siaya na utadhaniwa kuwa mchawi.

Hitimisho

Mijadala kati ya watu wasiofahamiana kimila inaleta kubuni na kuunda hali fulani mawazoni juu ya mtu ambaye hayapo duniani. Kuitumia hali iliyobuniwa ili utoe shauri kwa lugha yako kuwasaidia watu hawa wa mila tofauti na wako, inawezakuwa upuuzi.

Ugunduzi huo unatubidi tufikirie tena kazi ya kanisa kwa bara la Afrika. Kanisa linawezaje kuongozwa na lugha ambayo mizizi yake iko mbali? Hali hii inaleta mchanganyiko. Ili mijadala iwe barabara lazima wahusika wawe na hali ya mila inayofanana. Inter-cultural dialogue ni ubunuzi na upotevu. Haiwezekani. Kazi ya umisionari ili ifanywe kwa ukweli na udhabiti sio kuyarusha maneno ili yavuke mipaka ya mila, lakini ni ya mtu mwenyewe

kuvuka mpaka ili aweze kupeleka injili kwa walengwa kupitia lugha yao na kulingana na mila yao.

Hatua moja inayohitajika ili kuwezesha hali hii, ni lugha ya Afrika kutumiwa kwa elimu ya theologia Kiafrika. Hii peke yake inaweza kuliokoa kanisa Afrika kwa mikono ya wale ambao, hata ikiwa wanadhania wanafanya kazi njema, wanaathiri maendeleo yake.

5. Jiwe lililochongwa bila kazi ya mikono: injili ilivyo leta mapinduzi kwa waganga

Mathayo 2

Baada ya kuzaliwa kwa Yesu, Mathayo anatuambia, wageni walikuja kumtembelea, waliotokea mbali. Tunajifunza mambo mengi juu ya hawa wageni. Walitokea mashariki, walimpitia Herode, maneno yao yakamstua Herode kabisa. Walimwambia Herode mfalme alizaliwa Bethlehemu. Herode na watu wake wakajaa hofu, hali ambayo waliwafichilia kwa wageni wao. Wageni wakamkuta Yesu na mamake na babake. Wakamtolea zawadi, dhahabu, uvumba na manemane.

Hawa ambao juu nimewaita wageni, Biblia ya Kiswahili inawaita *mamajusi*. (Lenyewe Mathayo 2:1 inaandikwa: maneno kama hayo: “*To de Yesu en Bethleem tes youdias en hemerais herodou tou basileus idou magoi apo anatoloun paregenonto eis yerosoluma.*”) Sione kama hilo jina mamajusi linatumika sana, au likiwa limejulikana sana na watu. Mamajusi ni wa kina nani? Hali ya hawa wageni haijasumbua Waswahili peke yao. Kiingereza pia inazoea kuwaita *wise men*, ambayo ingefaa kutafsiriwa watu wenye hekima. Kuweka mwanga kwa jambo hili inaonekana tutahitaji kurudi penye lugha asili ya Agano Jipya, Kiyunani. Kwa Kiyunani hawa watu huitwa *magoi*.

Tukiiangalia Agano Jipya, tuko na sehemu tatu ambapo mtu anaitwa *magoi*. Moja ya hizi ni Mathayo, waliomtembea Yesu (Mathayo 2:1). Wengine wanatajwa katika Matendo ya Mitume 8:9 na 13:6. Wanaotajwa kwa Matendo ni watu waliotumia nguvu isiyo ya Mungu ili wakomeshe huduma ya Injili. Hiyo inahitaji tufikirie; kwani *magoi* ni maadui wa Injili? Neno hili linafaa litafsiriweje kwa Kiswahili? Ni wakina nani wanaotumia mbinu za Shetani kujaribu kuiharibu Injili ya Yesu, isipokuwa waganga? Watu hawa katika Matendo 8 na 13, sawa na waliomtembelea Yesu, wafaa waitwe waganga, na siyo mamajusi!

Wangukuwa wenye hekima, jinsi tafsiri kutoka Kiingereza inajaribu kutuambia, tungefurahia kuwaona pamoja na Yesu. Lakini sasa wakiwa waganga, tunaweza jiuliza, kwa nini Mungu anawapelekea kumtembelea mwanawe mchanga zizini? Mimi naona njia mmoja tu; *magoi* waliomjia Yesu walikuwa maadui wa Injili, ambao walikuwa na hali wa kutubu. Kuja kwao kwa Yesu kunaonyesha kitu kimoja maalum: waganga wanashindwa, uganga hauthibitishwi, bali unadhihirishwa unakuwa haufai mbele ya Mungu.

Kutoka 22:18

Kuna mstari katika kitabu cha Kutoka uliowaletea watu shida kubwa tangu zamani. Mstari huo ni Kutoka 22.18, mahali ambapo Musa anaiandika sheria mbali mbali za Mungu. Mstari mwenyewe kulingana na biblia ya Kiswahili unasema: “Usimwache mwanamke mchawi kuishi.” Mstari huo lazima utusitue kidogo, au sana. Huyu mwanamke ni mwanamke aina gani? Ni vipi, asiachwe kuishi – maana yake auawe? Ni akina nani watakao amua mwanamke fulani ni mchawi?

Juzi karibuni wasomi wameuchunguza sana mstari huo. Wawili hawa wanaitwa Priest na Adu-Gyamfi.³ Wanaweka shaka juu ya mstari huo. Badala ya kuutafsiri *mchawi*, yeye Priest hutuambia unafaa utafsiriwe *mganga*. Yaani, ni mganga ambaye hatajikani kuishi. Yule ambaye Mungu hafurahishiwe naye siye yule anayedhaniwa amemwumiza mwenzake na uchawi, lakini yule anayehimiza imani hiyo, na yule anayewaambia wateja wake wamerogwa na mtu fulani. Ya pili, kutomwacha mtu aishi, ni ipi? Wengine wamedhani inamaanisha, huyu mpaka auawe, achinjwe. Lakini, sawa na kutomruhusu mtu kuishi, ni kutomruhusu kusitawi.

Sababu ya waandishi hawa kuyaweka maneno vile nimeeleza juu ni nyingi, ambazo hatuna nafasi ya kutosha kuzichunguza kwa ndani. Mimi binafsi nafurahia utafiti wao uliowafanye wahitimishe vile. Kusema mchawi achinjwe ninavyoona mwenyewe sio maneno tunayotarajia kwa Mungu. Swali moja nyeti; nani ataamtambua mchawi? Pengine wengine wetu tumeshadhani watu wengi ni wachawi? Ukiambiwa mtu amekuroga, ni mchawi, ni vizuri kweli kuenda kumchinja? La hash! Yule anayefanya kinyume cha matakwa ya Mungu, ninavyoona pamoja na Priest, ni anayewasitaki wachawi, bila uhakika ndio wanahusika. Maana yake, Kutoka 22:18 ni dhidi ya waganga.

I Samueli 28

Neno lile lile linalotumika kwa Kutoka 22:18, linatajwa pia kwa 1 Samueli 28:7. Hapo tunamkuta Saulo akiwa na wasiwasi sana. Mungu ndiye alimchagua awe mfalme wa Israeli. Lakini, Saulo hakufanya vizuri,

³ Priest, Robert J., 2018, Bible Translation, Theology, and Witches. 75-85 in: Yeh, Allen and Tienou, Tite, (eds), 2018, *Majority World Theologies: theologizing from Africa, Asia, Latin America, and the ends of the earth*. Pasadena: William Carey Publishing. Angalia pia: Adu-Gyamfi, Yaw, 2016, “Thou shalt not suffer a witch to live,” (Exod 22:18) and Contemporary Akan Christian Belief and Practice: A Translational and Hermeneutical Problem,’ *OTE* 29/1 (2016): 11-32.

alijiingiza katika dhambi, na Mungu akamchagua mtu mwingine, Daudi. Maadui wa Saulo ni wengi. Kesho yake ilionekana atapambana vita vikali. Mungu hakuwa anaongea naye, au kumjibu maswali yake. Hapo Saulo, kwa kushindwa hali, aliomba ili atafutiwe mganga, yaani *magoi*, aweze kumshauri. Akapatikana mwanamke, *magoi*, wa Endori. Saulo akamwendea bila kujitambulisha. Akamtolea mzimu aliyetambulikana kama pepo la Samueli.

Jina linalotumika kwa huyu mwanamke ni sawa na lile neno la Kutoka 22:18. Kulinganishwa na Agano Jipya, anaweza fananishwa na *magoi*. Lakini habari tunayopata hapo, siyo alitakiwa kuuawa, ila alitakiwa afukuzwe: 1 Samueli 28:9. Tena, kazi yake haikuwa ya mchawi, ila ilikuwa ya mganga; alikuwa mtu ambaye watu walimwendea ili washauriwa na matatizo yao, aweze kuwaitia msaada kutoka kwa wafu, msaada ambao tunadhani mara nyingi uliweza kuwa *magoi* huyu kumtaja mteja wake jina la yule mchawi anayemwangamiza. Tunaweza dhani Saulo, mfalme wa Israeli, alifahamu jinsi ambavyo Mungu hakutaka waganga kama huyu mama. Ndivyo Saulo akawafukuza nchini mwake. Hatua ya kufanya hivyo inaonekana ilikuwa ya kipekee – Saulo alikuwa anakataa msaada wao kwa nchi yake, ambao nchi ya jirani hawakufanya hivyo. Hiyo inadhibitisha Mungu wa Waisraeli hafurahii kazi za waganga.

2 Wafalme 25

Biblia inazidi kutuonyesha jinsi wafalme wengine, baada ya Saulo na baada ya Daudi, walipambana na hali ya kuwafanyia kazi waganga. Kwa kifupi, tunapofika mwisho wa 2 Mfalme, Mungu alikuwa amechoka na watu wake Wayahudi. Tayari WaIsraeli walishapelekwa uhamishoni. WaYahudi wali-baki. 2 Wafalme 25 inatuelezea jinsi jeshi la Babulon likaja Yerusalemu na ushindi mkuu! Wakabomoa, wakaua, wakachoma, wakaharibu, wakashika mateka watu waliobaki, na kuwapeleka mbali mpaka Babuloni wawe watumwa huko.

Yeremia 29

Yeremia ni mmoja wa wanabii wanaoheshimika sana kulingana na Agano la Kale. Mengi ya maneno yake wakati ule yalikuwa makali sana. Alikuwa anawaonyesha WaYahudi walipokuwa bado katika nchi yao, walitakiwa wakubali kushindwa na maadui zao – wajisalimiske kwao. Viongozi wakati huo hawakukubaliana na Yeremia. Matokeo yalikuwa WaYahudi wengi kufanyiwa ukatili, kuuawa, au kutekwa nyara wawe watumwa Babuloni.

Kwa Yeremia 29:4-10, tunakuta maneno ya ajabu. Ajabu hiyo ninaotaja, ni Wayahudi kuhimizwa na Yeremia, wakishafika Babuloni, wajitulize hapo kabisa. Tukumbuke, Wayahudi walifanyiwa ukatili sana. Walivamiwa nchini mwao. Wengi wao wakachinjwa bila huruma. Wengi wale watu walioenda Babuloni walipoteza jamaa zao kulingana na ukatili wa mabavu waliofanyiwa na jeshi la mfalme Nebuchadneza wa Babuloni. Watu wengine wangukuwa na uchungu, pengine madhumuni ya kulipa kisasi, na hawangekubali kujihuishia kwa amani na watu wenyewe waliowafanyia unyama mwingi. Lakini Yeremia anawaambia Wayahudi waishi kwa imani, wazae Watoto wao, wajenge nyumba zao, na wapendane na majirani mwao wakiwa Babuloni!

Ni maoni yangu kusema, mfalme Nebukadneza aliona hayo yote yaliotokea, na alishangaa. Yaani, alizoea kuona baada ya kuwashinda maadui wake, wakaja Babuloni na uchungu mwingi na hali ya kugoma na kuwachukia wenyeji. Haikuwa rahisi wakubaliane tu na hali mpya vile ilivyo. Sasa watu kutoka Yerusalemu walikuwa tofauti sana. Moja kwa moja, ni kama walishawasamehe Wababuloni kwa ukatili waliowafanyia. Wakawa na amani! Tunaweza kudhania tu vile WaBabuloni wangeweza kuwaona wanaishi kwa amani. Vile walikubali kizazi kilichowatangulia kilifanya dhambi, na ile dhambi ndiyo iliwasababisha maafa. Hawakuwalaumu WaBabuloni, na waliona kisasi ni cha Mungu. Mimi nadhani mfalme aliweza kuongea na Wayahudi juu ya imani yao. Alipofanya hivyo, alifunzwa juu ya wakina Musa, Daudi, Ibrahimu. Pengine aliweza hata kupata nakala ya maandishi ya Agano la Kale. Kupata maelezo aina hiyo na kuyasoma yangemshangaza zaidi. Kati ya hadithi aliyoelezwa au kusoma nafikiria ilikuwepo ya Saulo, tuliyoeleza juu, kuwa amefukuza Waganga wote kutoka Israeli. Nadhani Nebuchadreza alijiuliza sana sababu ya kufanya hivyo; kwa nini kuwafukuza watu ambao wenyewe walikuwa msaada kwa jamii, jinsi watu wengi walikuwa wanaamini juu ya waganga? Pengine, aliweza kuwa akajifikiria, waganga sio wazuri jinsi watu walikuwa wanafikiria, lakini walikuwa wadanganyifu?

Danieli 2

Nebuchadneza hakuwa mpumbavu, wala mjinga. Mfalme lazima awe mwerevu. Kupitia uerevu wake, akawaza sana jinsi kabla ya hapo haja pata kuwaza! 'Ingekuwaje,' alijiwazia, 'Mungu wa Wayahudi angalikuwa Mungu wa kipekee kweli?' ... Ingekuwaje, badala ya kulipiana kisasi, watu wangemwachilia Mungu alipe kisasi? Sio; watu wangeweza kuishi kwa maisha ya amani ya ajabu! Uwezo huo ungewapa hawa watu nguvu ya

ajabu, badala ya utawala wa mabavu kama ulikuwa kwa ufalme wake, ungekuwa utawala wa upendo!

Nebuchadreza alianza kuona maono kama hayo. Mpaka akaota ndoto kabisa juu ya dunia mpya, kwa hiyo dunia mpya nguvu mpya ya jiwe kidogo iliweza kuwashinda wafalme wakubwa! Msamaha na upendo utawashinda wafalme wakuu! Sasa, alitaka kuona ikiwa wengine wange-weza kuona jinsi alivooa yeye. Lakini, hakutaka kuwaeleza tu waganga wake ndoto ili wamtafsirie. Hivyo amefanya mara nyingine. Lakini sasa aliwashuku waganga. Aliwafahamu wanakuwa wadanganyifu! Mfalme akawaita waganga pamoja, halafu aliwapa majukumu. Yaani, aliwaambia wamtafisirie ndoto kabla hajawaambia alichoota! Hivyo alijua atawavuruga na kuwatoa penye udanganyifu wao! Alitaka ajue, kweli yupo mtu aliyeyagundua mambo ambayo alikuwa anaanza kuona!

Mfalme akawaita wote wenye hekima nchini mwake, maana yake waganga aina mbali mbali. Waliposimama mbele yake, akawaambia wamtafsirie ndoto yake. Kusikia hayo, waganga wakamwomba awaelezee kwanza ndoto hiyo. Alikataa! Waganga wakamwambia miungu pekee wanaweza hayo. Mfalme akawaambia, wasipomtafsiria, watakufa wote, atawakata sehemu sehemu, na kuharibu nyumba zao! Waganga wakao-gopa sana.

Mfalme alipokuwa anapanga utekelezaji wa mpango wake, alikuwa anatamani Wayahudi pia wapatikane, ili aweze kuwajaribu akili zao. Kumbe wakati huo Danieli akapata kueleza hayo. Yeye angekuwa moja wa wale watakaokufa! Aliomba nafasi apelekwe mbele wa mfalme. Mfalme akakubali – sababu nadhani ilikuwa mfalme alitamani sana kugundua mawaidha ya Wayahudi wao. Walipewa mpaka kesho yake. Danieli aliwaelezea wenzake Shadrack, Meshak, na Abednego. Akaenda kumwomba Mungu. Mungu alimfunulia! Mimi naamini alimwelezea kitu kama hiki: “Nebuchadreza amegundua mipango yangu vile ilivyo. Amesumbuliwa sana akitafakari jinsi ufalme wake utakuwa mbeleni, upendo na msamaha ukiwepo. Aliona upendo wangu wa agano langu jipya ulipoanza ukiwa tu jiwe ndogo, liliharibu wafalme wakubwa wakubwa na kukua mpaka dunia pote ikafunyiwa na jiwe lenye upendo huo! Mwambie hivyo, na mtaokolewa pamoja na waganga wote. Waganga wanatafikana waerevuke wabadilike waingie ndani ya agano langu jipya!”

Danieli alimjia mfalme. Mfalme alifurahi sana alipomwona, hata ikiwa nadhani mwanzowe bado alibaki na shaka; Danieli amegundua ndoto yangu kweli? Basi, Danieli alimwambia: “Mfalme, ulikuwa ukaota juu ya sanamu kubwa iliyotengenezwa kwa dhahabu, fedha, shaba, chuma na udongo. Wewe ndiye dhahabu, kichwa cha sanamu, mtawala mkuu! Lakini miguuni penye sanamu chuma ilichanganywa na udongo. Halafu,

ulipokuwa unaona, jiwe moja ndogo likatokea mlimani, lililotengenezwa siyo na binadamu, na likapiga sanamu chini ikaanguka yote ikawa kama makapi ya viwanjani vya kupepetea wakati wa hari! Lakini wakati huo jiwe likawa kubwa kama mlima ambalo likafunika dunia mzima!” Mfalme alimwambia Danieli: “Hakika Mungu wenu ndiye Mungu wa miungu, na Bwana wa wafalme, awezaye kufumbua siri, kwa kuwa wewe uliweza kuifumbua siri hii.”

Hitimisho

Ilikuwa baada ya miaka mingi ... Wengine wameshasahau ndoto ile ya Mfalme, na maneno yake, na maisha ya Saulo. Lakini, pale Babuloni, walibaki wengine ambao hawakusahau. Hawa ndio walizidi kutafuta jinsi Mungu atatekeleza mpango wake wa kuharibu wafalme wakubwa duniani ili habari njema yake ya upendo itawale duniani. Hawa walikuwa wanaendelea na shuguli zao za uganga, wakitarajia siku moja watapewa ufunuo upya ili waachane na shuguli hizo. Ilifika wakati ambapo Mungu akawatumia ishara. Akawaambia waende penye asili ya Wayadui ili wagundue mambo ya Mungu. Wakaenda Yerusalemu. Baada ya kuuliza uliza, wakaelekezwa Bethlehemu. Walipofika walimwona mtoto, alitokea siyo kulingana na kazi za binadamu, lakini kufuatia kazi za Roho wa Mungu. Wakamsujudia. Wakampa zawadi waliyobeba, wa dhahabu, uvumba na manemane. Tangu siku hiyo, wakaachana na uganga wao wenye udanganyifu wakijiunga na kazi za kuitangaza injili ya Bwana Yesu.

6. Mitume wa KiAfrika wawe wasikivu – majibu kwa upinzani wa utume wenye usikivu

Yesu ...

*“Akamwambia, Mpende Bwana
Mungu wako kwa moyo wako wote,
na kwa roho yako yote,
na kwa akili zako zote.”*

Matthew 22:37

*“Tunawezakuwa na hali ya usikivu
sababu ... hatuogopi.”⁴*

Mafupisho

Maandishi haya yanaleta jibu kwa wanaopinga huduma ya mitume wenye usikivu. Ni kweli, aina huduma nyingine sio rahisi kufanya na hali ya juu ya usikivu. Usikivu unaotajwa hapa unakuwa wa kuwepo au kutokuwepo, kuwa na usikivu, au kutokuwa na usikivu: Huduma ya mmisionari wa kawaida siku hizi haiwezi ongezewa usikivu sana pasipo huduma yenyewe kubadilika sana. Inatakikana wengine, hata wakiwa wachache, sisemi ni lazima wawe wote, wafanye huduma ya usikivu. Usikivu unamwezesha mtume kuhepa hali ya kuwa chombo cha dola. Unahitajika kurekebisha makosa yaliyofanywa awali. Unaleta hali inayomlazimisha mtume kujenga msingi wake wa huduma juu ya imani na siyo juu ya mali. Uhimizo wa huduma yenye usikivu kweli ni changamoto ngumu. Huduma yenye usikivu ni kinyume cha mbinu za pesa kutawala ambao wengi wamezoea. Huduma yenye usikivu inajaribu kuwanyang’anya wenye mali nguvu ya kutawala mioyo ya watu. Ni mbinu za kuhepa mitego inayowaangusha mitume, ya kuwafanya watu wamtegemea mtumishi wa Mungu badala ya Mungu mwenyewe. Kusema tu ‘nyenyekeeni’ haitoshi, usikivu unahitajika.

⁴ Willard, Dallas. *Divine Conspiracy: rediscovering our hidden life in God*. San Francisco: Harper. 181.

Maelezo juu ya Maneno

Ninatumia neno la Swahili utume au mtume kueleza Mwafrika anayefanya kazi ya kulinganishwa na hiyo ya *apostolo*⁵ kwa Agano Jipya, na mmisionari kwa panda ya Wazungu, yaani watu kutoka Ulaya. Wengine hupenda kufanya kazi za utume wakitegemea lugha na mali kutoka *nje*, kwa mfano kutoka Ulaya. Ubaya, ukiwajia watu kupitia lugha na mali kutoka nje, wanakuitikia kwa sababu ya mali hiyo unayo. Tena, usipotumia lugha ya wenyeji ambao wanafikiwa, hutawafahamu barabara. Ni sababu sasa nahimiza kufanya kazi za Mungu, hasa kupitia mipaka ya kabila na nchi, pasipo nguvu ya pesa ya nje, na kupitia lugha za wale unaotaka kuwafikia. Ndiyo tunaita *huduma yenye usikivu*.⁶

Natumia Kiswahili ya *huduma yenye usikivu* kutafsiri maneno ya Kiingereza ya *vulnerable mission*. Ni huduma inayofanywa kupitia lugha na rasilmali ya wanaofikiwa. Sababu ya kufanya huduma yenye usikivu ni mingi. Ni ngumu sana kutoa mali na kutoheshimika kwa ajili ya mali hiyo. Suluhisho ni mtume asiwe na mali matumizi ila yake binafsi kujitegemea, na asiwe na sauti kwa wenye mali wanaohusika na jamii lengwa. Pia atumia lugha ya wenyeji.

Utangulizi

Wengine hupinga mambo ya utume wenye usikivu. Wanasema, hauwezekani, haufai. Hapa nataka kuutetea. Siyo kama mbinu ya kuboresha njia za utume zinazotumika wakati huu, lakini kama njia nyingine tofauti inayotakikana kutekelezwa.

Ingekuwa vyema sana kuigundua mbinu itakayoweza kuwafanyie mitume wengi au wote kuwa na usikivu kwa wanaowafikia pasipo mabadilisho mingi kwa jinsi huduma inafanywa. Ugunduzi huo ungewafurahie watu wote! Ubaya, aina nyingine za njia zinazotumika za utumishi, hasa hizo zinayotegemea mali na lugha kutoka nje, hazitawezekana kuwa ya usikivu sana. Msingi unaohitajika ili mafanyikio yaje na usikivu, ni wa Neno la Mungu.

Hapa najaribu kuonyesha umuhimu wa kuwa na mitume wachache wasikivu. Ndivyo ingekuwa bora kuwasaidia wengi kuongeza usikivu wao, lakini mbinu za wengi za hudumu mara nyingi hauruhusu usikivu vile

⁵ Kwa mfano, Matendo 8:14.

⁶ Angalia pia: Harries, Jim, 2006. 'Vulnerable Mission as an Alternative to Failing Aid Paradigms.' <http://www.jim-mission.org.uk/articles/vulnerable-mission-as-an-alternative.pdf> (accessed 21st January 2011).

tunavyoeleza hapa. Wengine wakifurahia maelekezo yetu hata wasipoweza kuyatekeleza ni vyema, lakini hawa sio walengwa.

Kuwa msikivu kidogo, ni kutokuwa msikivu. Tukikaza tu usikivu kidogo, mahitaji mengine yatakuwa rahisi kuingilia kati na usikivu kusahaulika. Umuhimu wa usikivu tunaokaza usidharauliwe. Kazi mingi za wamisionari kutoka nchi za Magharibi zimejengwa juu ya kuwa na uwezo wa mali na uhusiano kilugha wa kushinda ile ya wenyeji wanaofikiwa. Uwezo huo unakuwa wa lugha, mali, ujuzi wa teknolojia, kitamaduni, elimu nk. Ukianza ukijua wewe ni bora, hujaweka msingi wema wa usikivu. (Ubora wa mtume unatajikana uwe wa ufahamu wa ndani na uhusiano wa karibu na Mungu. Swali la jinsi Mungu anataka kujidhihirisha kwa watu wengine ni swali lingine.) Je, nikishaamua njia inayofaa kwake kufuata kabla sijakutana na mtu, nikitaka kumfanya ili aifuata hiyo njia, naweza kuwa msikivu kweli? Lengo la huduma likiwa kumhusisha mtu na Mungu, lakini ukiwa ubora wa mtume (pesa, lugha, elimu n.k.) unawekewa msingi ambao ni pesa kutoka nje, itakuwa rahisi kumweleza anayefikiwa kumbe njia ya kumfikia Mungu siyo ya Mungu lakini ya rasilmali kutoka Ulaya.

Biblia, kulingana na fahamu yangu, haihitaji mtu nusu. La hash! Inamhitaji yule anayokubali kujitolea kwa ajili ya Mungu na wengine, asilimia mia. Kwa mitume wengine kufanyiwa masikivu ni mazuri, lakini sijui jinsi kuwafanya hivyo.⁷ Mapendekezo yangu ni, tuwe na mitume hata wakiwa machache, ambao ni wasikivu kweli, kushinda wengi wasiowasikivu kweli.

I. Kumtaka mtume awa masikivu, je, ni kupita kiasi?

Mara kazi ya Mtume inaelezwa kama ndiye yeye anafaa aongee, wengine kumsikiliza, na ndiye yeye kujua suluhisho kwa matatizo ya watu, pasipokujali mazingira. Kwa Mtume, kulingana na maono kama hayo, ujasiri ni muhimu zaidi ya usikivu. Je, hiyo ni kweli? Au usikivu ni muhimu kiasi gani?

Mtu anayetaka kuleta mbinu upya unaopinga ule wa watu wengi hukutana na upinzani. Waliokomaa kawaida hufahamikwa wanakwepa yasiokawaida na kufuata njia kuu. Vijana ndio wanahitaji kuelekezwa, ili wapunguze mbio zao kufuatilia ukweli ambao bado hawaujajua kwa ndani. Kukaza sana utumizi wa lugha na mali ya wenyeji, na hivyo kupinga

⁷ Lengo ni kumfanyia mtume afinywe na muktadha yaliopo ili maneno yake yafaa kwa mazingira. Ila, ni muhimu mtume amjue Mungu, na Mungu ni wa watu wote, na juu ya mazingira, lakini Mungu pia huongee na watu kulingana na mazingira, lugha, na mazoea yao, n.k.

Kiingereza na ufadhili kutoka Ulaya, kunawezaonekana kitendo cha upuuzi cha yule ambaye bado hajajua juu ya utekelezaji wa kazi. Itawezakuwa, yule atakayezidi kusisitiza umuhimu wa kuwa msikivu ataleta penyo nyingine kati yake na mitume wenzake ambao hawajali jambo hili.⁸ Lakini kwa njia nyingine, kinachowasumbua mitume ndicho hali ya kukosa usikivu unaofanya wagawanywe na kuchochewa vita mbali mbali kati yao. Wangeenda kwa njia pole pole ya kuwasikiza watu kabla hawajafikia uamuzi wao juu ya jinsi kuwafanyia huduma, naona ingekuwa afadali.⁹

Kinachosababisha kutokubaliana na hata 'vita' kati ya mitume, nataka kusema, hasa ni kitu kimoja; kukosa hali ya usikivu.¹⁰ Watu wanaotoka eneo moja na kuenda eneo lingine penye watu wenye mila tofauti hukutana na changamoto mingi na kali. Changamoto hutokee sababu wanajikuta wanafanya huduma zao chini ya mipangilio miwili; ya wenyeji wanaofikiwa, na wale kutoka kwao ambao wamekuja nao kuwafikia. Je, inafaa mtume afanye kazi yake chini ya maadili gani, hiyo ya kwao, au hiyo ya watu anaowafikia? Ikiwa ya kwao, wanaofikiwa hawatamfahamu, na atazidi kugongana nao. Ikiwa wa wanaofikiwa, watu kwao pengine hawatakubaliana nayo kwa rahisi. Nguvu za pesa na lugha ikitokea kwao, mtume hataweza kujiingiza ndani kwa maadili ya wafikiwa bila kupigwa vita na watu wa kwao, vita ambavyo ni rahisi vimshinde. Vikimshinda, anabaki na kuendelea kufanya ugenini kama angekuwa kwao.

Suluhisho wa hali inayotajwa juu ni kwa mtume kutotegemea mali mingi kutoka kwao, na kutotumia lugha za kwao. Kawaida ni ngumu sana watu wa jamii fulani kugundua jinsi mambo wanayoyafanya na kuyaamini siyo ya watu wote. Hivyo, wakiutawala uinjilisti unaoendelea, ni rahisi waufanye uwaige wenyewe na kitamaduni chao. Kuepuka na hali hiyo ni wa kwao kutogharamia kazi ya uinjilisti na pesa nyingi. Wasipoigharamia, hawatakuwa waangalifu sana kulazimisha mambo yatokee kulingana na mazoezi yao na mapenzi yao. Tena, mtume akiitumia lugha ya wale anaowafikia, wa kwao hawatagundua moja kwa moja mambo yakienda tofauti na mapendekezo yao, sababu hawataifahamu lugha.

⁸ Kutosikilizana kinacholeta magongano, hutokee zaidi kati ya mitume wenyewe badala ya kati yao na walengwa. Schultz, George, nd. 'Pre-Field Training: Your Missionary's Future May Depend On It.' <http://www.caminternational.org/index.cfm?go=page&pid=109> (accessed 23rd May 2007)

⁹ Njia moja ya mbio inayotumika sana siku hizi na wamisionari kutoka nchi za Ulaya ni hiyo ya kutumia lugha yao, hasa ikiwa Kiingereza, inayohesabika lugha ya dunia mzima, badala ya kuenda pole pole na kuchukua majukumu ya kujifunza lugha za walengwa.

¹⁰ Harries, Jim, 2009. 'Ducking Missionary Conflict in Africa and Beyond.' 272-274 In: *Evangelical Missions Quarterly*. July 2009. Volume 45, No. 3.

2. Mitume ni watumishi wa waliowatuma, au ni watumishi wa Mungu?

Jamii asili ya mtu inapomlea inampa maelekeo ya maisha. Lakini ni wamisionari kutoka Ulaya walioleta mbinu wa utekelezaji wa kufanya kazi ya mitume kwa bara la Afrika. Wamisionari kutoka Ulaya walikuwa wanafanya kazi zao kulingana na maelekeo waliopewa na jamii yao. Lakini je, mitume kutoka Afrika wanafaa wapate kujifunza mifumo yao yote ya huduma ya utume kutoka kwa Wazungu?

Wengi watu wa Ulaya hujifahamu kama watu wanaojitegemea. Wanafikiria hali hiyo inawapa ubinafsi wa njia ya kipekee. Wanafikiri inawapa kutowategemea wengine, kwa hivyo kwa njia nyingine kutowajali wengine. Ufahamu huo umetokea kulingana na uhuru waliopewa na imani yao ya Ukristo. Wakristo wanafunzwa kumcha Mungu na siyo binadamu. Kwa hivyo, Wakristo, na pia kwa ajili ya kuathirikwa kwao na funzo hayo hayo raia wa Ulaya ya asili wasiokubali kuwa Wakristo, hawaogopi uchawi wala mapepo jinsi watu wengine duniani wanaogopa. Mtu kutoka Ulaya anaweza kuishi maisha yake kwa uhuru fulani. Biblia pia inatambia tupendane. Kwa hivyo, yule asiyeogopa kufanya tofauti na mwiko unaowashika wenzake, pia anatafuta jinsi ya kujitolea ili awe msaada kwa wenzake hawa hawa. Mambo hayo mawili, haogopi mwiko, lakini anayemotisha wa upendo wa Mungu, yanaleta hali ya ajabu – watu wanaojitolea kwa kiasi kubwa kupendana kwa kutumikiana au kusaidiana, pasipo uoga huo ambao ungewalazimisha kufuata njia za mila. Uhuru aina huo umewasaidia Wazungu wenyejii wa Ulaya kutengeneza uchumi unaofanyikisha wa ajabu siku hizi.

Tunaweza sema, kwa kiasi ambacho ni muhimu, Wazungu, wanaoamini Kristo na hata wasioamini, huungana sio kwa sababu ya sheria wala mwiko, lakini sababu ya upendo wa Mungu. Hali inayotajwa juu inawafanye Wazungu wawe wanategemeana kabisa kabisa, bila kujitambua wanafanya hivyo! Yaani, wanasema kila mtu binafsi anauhuru kufanya apendavyo, ambayo ni kweli sababu miiko inayowafunga watu wengine duniani haiwagusi sana. Lakini wanasahau kiwango chao cha kujitolea kwa ajili ya wenzao kupitia mbinu ambazo wameunda pole pole baada ya kupata uhuru wa Ukristo kufanya hivyo. Maelekeo ya Mzungu yanamfanya asiwe anajali tu jamii au ukoo wake, lakini watu wote duniani, sababu anaamini majukumu lake ni kuwapenda wote, na wote wanapendwa sawa na Mungu.¹¹ Kwa hivyo, moyoni mwake Mzungu anasukumwa sana na sera

¹¹ Yohana 3:16

hizo za watu wake kujitolea kwa njia wanazoonza zitawafaidi watu wote duniani. Amesahau mahali msukumo huo hutokee (Biblia). Pia ni rahisi afikiri maelekeo yake ni ya kawaida; hatambue utofauti wa wengine wasio na msukumo kama wake huo. Sababu hatambue asili ya mabadiliko yaliomwathiri, Mzungu anashangaa kwa nini watu wengine duniani wasimsikize au wasimfahamu haraka ili wawe pia kama yeye.

Ujinga huo ninaoutaja juu humsumbua zaidi yule Mzungu asiyemwamani Kristo. Lakini, hata Wakristo, na hata Wamisionari wanakuwa na ujinga wingi. Wamisionari hushangaa ni kwa nini Waafrika, kwa mfano, wasiwafahamu na kufanya kulingana na maelekeo yao? Ni sababu historia yao, jinsi mababu yao waligeushwa na Injili, imefutwa penye kumbukumbu iliopo iliyowekwa rasmi na wasiompanda Yesu ambao wamepata nguvu kuisisitiza jinsi historia inatajikana kuandikwa. Huo ujinga wa Mzungu ni sababu moja maalum wa kutomsikiliza akija bara la Afrika na ushauri wake. Ubaya, makosa lake moja kuu nyingine, ni badala ya kuwaruhusu watu kukubali au kutokubaliana na ushauri wake, anajilazimishwa kwao kwa kutumia pesa zake, yaani anawafadhili wanaokubaliana naye na pesa nyingi.

Mambo ya juu ambayo yamefanya wamisionari wengi kutoka Ulaya kupotea njia yanahitajika kujulikana kwao ili wabadilishe maelekeo. Bado hawajayagundua. Kutogundua kwao hivi kinamaanisha mitume panda ya Afrika wanatajikana wajihadhari sana na kuiga mbinu za huduma za Wazungu. Badala ya mbinu wa kufanya utume unayodhania watu wote hufanana na Mzungu, unahitajika mbinu ya Biblia asili uwaelekeze Waafrika kwa mazuri hayo ambayo Mzungu amegundua. Maana yake, inabidii mitume wawajie watu kiBiblia, na siyo wa kiBiblia kulingana na Mzungu. Kufanya hivyo ni ngumu sana kupitia Kiingereza, sababu Wazungu ndio wanatawala lugha hiyo. Wanatawala lugha hiyo, sababu ni yao. Wako tayari kumrekebisha ye yote anayeitumia. Pili, sababu Wazungu ndio hutawala pesa inayotegemewa kwa miradi nyingi kwa kanisa la Afrika, kuihepa ni kutotumia pesa ya Mzungu, yaani pesa za nje.

3. Jinsi watu watakaomfahamu mtume

Watu watamfahamu Mtume kulingana na vile wanavyowafahamu waliomtangulia. Mzigo mmoja ambao mtume wa asili ya Kiafrika anabeba, ni kufahamishwa jinsi wamisionari kutoka Ulaya waliomtanguliza kwa kazi yake walifahamishwa. Watu wataweza kutarajia yeye afanye kama hawa walivyofanya, na asipofanya hivyo anaweza hesabiwa duni. Wamisionari kutoka Ulaya wameweka msingi kusema mtume anakuwa na mali nyingi, hatajali sana lugha ya watu lakini atependa atumie yake, atependa kuleta

teknologia mpya, n.k. Mtume MwAfrika akikuta hiyo hali, atafanyaje? Asipojali, bado ipo. Ataitikiaje?

Watu watataka kujua aliyetumwa kwao na Mungu ni mtu aina gani. Kuitikia kwa maneno yake kitategemea hali yake vile ilivyo. Km, wengine watakuwa tayari kumsikia mtajiri, lakini hawatakuwa na muda kwa mfukara. Wengine watafurahia yule anayekuja kuongea Kiingereza, lakini hawatakuwa na muda kwa yule anayeongea lugha za wenyeji. Hata wasiposema, hivyo maelekeo yao yanaweza kuwa yalivyo.

Watu wengine watawezakuwa wamechoka na Wazungu, na watakuwa tayari kabisa kumsikiliza Mwafrika. Lakini wengine watakuwa wanajua; Mwafrika hawezi kamwe kuwa mtume.

Swali moja muhimu, ni jinsi mtume atawaitikia Wamisionari kutoka ngambo. Akisonga karibu nao, wengine wataweza kumfahamu anajaribu kujifaidi kifedha. Ikiwa hivyo, basi wale anaowahudumia watahitaji pia kushiriki kwa pesa yake; asipowagawia pesa inao dhaniwa anapokea kwa Mzungu, watu wataweza, waseme au wasiseme sababu, kugoma.

4. Uhusiano kati ya mali na watu: urafiki au uadui

Kulingana na kitamaduni chake, Mwafrika hufanya hesabu kadhaa juu ya uhusiano wake na watu aina mbali mbali. Hasa, hataki kumtolea mtu zaidi ya kiwango anachopokea, au kupokea zaidi ya jinsi anayetoa. Sababu uhusiano wake unamhusisha na vitu mbali mbali, mahesabu yanakuwa ngumu. Kwa mfano, mtu akikubeba kazini kwa gari lake, na anakataa usimlpe pesa, utakuwa na deni. Utalipaje deni hiyo? Kwa njia moja au nyingine, lazima ulipe.¹² Wasiwasi juu ya kiwango cha deni yao kinawasumbua watu sana. Hii ni sababu deni ndiyo, pasipo tahadhari, itaweza kumletea mtu balaa. Maana yake, deni, na mapepo, na uchawi, ni vitu vinavyo na uhusiano. Deni isiyofaa, pengine ni kubwa, pengine ni kwa mtu adui wako, pengine umepewa deni pasipo kujua, ni hatari: Linamfungulia mwadui wako pengo anayowezakutumia kukuumiza.

¹² Barclay anaeleza jinsi siku hizi watu huangalia mambo ya zawadi, inayohusisha na neema ya Mungu. Nje ya kitamaduni cha Wazungu wa Ulaya, zawadi yote hutolewa kwa mataraji ya kupokee aina marudio. Ni wakati anayoita *modern* pekee, na watu wa Ulaya, wanaodhania zawadi inawezatolewa pasipo kuweka matarajiyo yote ya kurudishiwa. Waafrika basi ni kati ya watu wanaoamini kutolewa kwa zawadi ni kutarajia malipo. (Barclay, John M.G., 2017, *Paul and the Gift*. Grand Rapids, Michigan: William B. Eerdmans Pub. Co.)

Njia moja wazi kulipa deni, ni sifa. Mfukara anajishugulisha kuwatafuta na kufuata wenye mali.¹³ Anapowakuta, anaeleza msaada anayehitaji. Atalipa kwa njia mbali mbali, lakini hasa kwa kuwa mfuasi muaminifu, na sehemu moja ya uaminifu huo ni kumtolea mkubwa huyu sifa. Sifa hii inakuwa kinyume cha msingi wa Kiingereza kwa njia mbili. Moja, inakaribiana na hali ya kumwomba mungu asiye Yahweh, na msingi wa Kiingereza unakuwa kwa kumwabudu Yahweh Mungu wa kipekee. Ya pili, inayofuatana na hiyo ya kwanza, Kiingereza lina jambo linaloita *truth*. Hili *truth* lina msingi ndani ya Injili (kumwamini Yhwh.) Kwa hivyo *truth* ni kitu tofauti sana na *ukweli*, neno linalotumika kulitafsiri kwa Kiswahili. Ukweli siyo sawa na *truth*! Ukweli ni jambo linalomsaidia mtu kujiendeleza na kuepuka na balaa ya deni. Sehemu ya *truth* ni jambo geni Afrika. Kiafrika, kumjua mtu ni muhimu kushinda kukijua kitu. Ndivyo Waafrika wanavyomwelekeza Mzungu, ambaye kawaida ni mwenye kugawanya mali.¹⁴ Maneno wamaomwambia sio *truth* ila *ukweli*, maana yake, maneno wanayaona yatawaletea faida.

Wengine hufikiria, kukubaliana na hali aina hiyo ni kuwaheshimu WaAfrika.¹⁵ Lakini, kinyume cha hiyo, nataka kusema, kujiingiza katika mila aina hiyo siyo vyema na haleti faida, sababu mila kama hiyo siyo ya Mungu:

- 1) Nchi za Wazungu zimejulikana sana kwa kuwa eneo lenye uzaalishaji mali. Watu wengine wa nchi zingine hutamani mali yao. Mali hangezaalishwa Wazungu wasingekuwa na ufahamu wao wa *truth*, tofauti na *ukweli*. Wazungu kutoeleza msingi wa hali ya *truth* ni udanganyifu. Ili Mzungu afanye haki kwa Waafrika, lazima ahepe kitamaduni cha kulipa deni kupitia sifa, ambacho kinaleta ukweli badala ya *truth*.
- 2) Mtu kutoka nchi tajiri asiyejaribu kujifaidi na mali akitembelea Afrika, tayari ameenda kinyume cha mbinu za Kiafrika za kutafuta uhusiano na wenye mali. KiAfrika ni kinyume sababu Kiafrika ni mmaskini anayemtafuta mtajiri ili atengeneza naye uhusiano, sio mtajiri kumtafuta mmaskini.¹⁶ Mzungu mgeni Afrika asipopinga hali ya kulipa deni na sifa (ambaye ni *untruth*) anajitangaza yeye pia anakuja kujitajirisha. Ndivyo inaweza kuwa siku hizi Waafrika

¹³ Maranz, David, 2001, *African Friends and Money Matters: observations from Africa*. Dallas: SIL International

¹⁴ Harries, 'Vulnerable Mission.'

¹⁵ Nilikuta watu kadhaa wansema jambo hili nilipokuwa kwa matembezi USA 2013. Maranz mwenyewe anasisitiza hivi pia (Maranz. *African Friends*. 208.).

¹⁶ Maranz. *African Friends*. 74-76.

kadhaa wanaamini.¹⁷ Lakini imani hiyo ni kinyume kabisa na maono ya Wazungu wanaojiona wanaenda Afrika siyo kujitajirisha ila kuwatolea Waafrika msaada.

- 3) Ufunuo wa Biblia yenyewe unapinga mbinu za kimila cha Waafrika kulipa deni na sifa kwa mtu. Wakristo huamini Yesu alikuja kujitolea kwa ajili ya wenye dhambi ili kuwaokoa. Kwa nini Mungu ambaye ndiye mtajiri wa mwisho, anajishugulisha na binadamu, mmaskini? Kiafrika kiasili, jambo hili halieleweki. Ni jambo jipya, linaloletwa na Agano *Jipya*. Ni neema ya kipekee ya Mungu! Mungu anampenda hata mwenye dhambi! Yaani, anampenda mtu mwenye deni kabla hajapewa sifa (Warmi 5:8). Mungu hategemee ukweli, anategemea *truth*.
- 4) Mbinu za kujaribu kulipa deni na sifa ndio msingi wa ufisadi wingi Afrika. Ndivyo pia, ufahamu huo unaosema mwenye kusaidia lazima alipwe. Msingi huo unamfanya mhudumu wa serikali akatae kumsaidia raia asipopewa rupurupu, hata akiwa analipwa msharaha kutosha kwa ajili ya jitihada zake. Mzungu mgeni kujiingiza kwa mbinu za Kiafrika aina hii ni uwongo na uovu usiofaa mtu wa Mungu.

Ya juu haimaanishi wageni lazima wapinge au wapige vita dhidi ya mbinu za kulipa deni na sifa. Lakini, maishani mwao, waonyeshe msimamo wa kutojihusisha nayo sababu ni jambo moja ambalo ni kinyume cha injili.

5. Mtume kuwa na usawa na wenyeji

Wamisionari Wazungu kutoka Ulaya wamesumbuliwa sana na hali ya kujisikia kuhukumiwa kwa ajili maishani mwao wamezoea utumizi wa mali nyingi sana kushinda Waafrika. Kuja Afrika kinawafanya wasituke wanapowakuta watu ambao wanaendeleza maisha yao na rasilimali kidogo. Matokeo, hata wamisionari ambao wamekuwa na maelekeo ya kiroho, ni rahisi waanze kujishugulisha sana na kupokea na kusambaza rasilimali kutoka kwao, maana yake Ulaya. Ugawaji huo wa mali ya dunia umeleta matatizo sana; Wazungu kuhesabiwa kama miungu, utegemeo kwa Mzungu uliozuia maendeleo pasipo msaada wake, kusambaa kwa lugha ya Mzungu pale ambapo haiteti msaada kwa kweli, n.k. Mazoea hayo yanazidi kuathiri kazi ya mitume ya Kikristo, wakifahamikwa kuwa wenzi wa Wazungu. Yanawafanya wasiweze kuwa wasikivu kwa rahisi kwa watu wanaowafikia. Wengi mitume wa Kiafrika wakijaribu kufanya huduma zao,

¹⁷ Nasikia hayo mara kwa mara kwa Waafrika wenzangu.

wanajikuta kutarajiwa wafanye vile Wazungu waliotangulia hufanya. Matarajio hayo yanasumbua sana. Wenyeji wanawezakuwadharau mitume wanaowaiga Wazungu, wakigundua kiasi cha mali wanaotumia ili wafanye hivyo. Huduma unakwama kwa rahisi!

Napendelea tuangalie pikta tofauti ya huduma ya mitume. Badala ya kuifahamu huduma ikiwa kitu kinachofanywa na mali, tuiangalia kama michezo, kwa mfano wa mpira. Kwa michezo aina hiyo, rasilmali haifikii penye kiwanja chenyewe. Ni wachezaji tu, nguo zao, na mpira wenyewe, inayofika kiwanjani. Wachezaji kuitumia rasilmali nyingine kiwanjani ni kinyume cha sheria ya mpira. Ni kweli, aina rasilmali nyingi inaweza tumiwa panda ya maandalizi: chakula bora, usafirishiaji ya wachezaji, pesa kuwalipia mshahara, gharama ya maandalizi mbali mbali, n.k. Lakini, kiwanjani cha michezo chenyewe, hayo yote yanaachwe nyuma.

Pengine kazi ya utume, na hata ya umisionari, inatakikana iwe kama michezo ya mpira. Yaani, huduma huo wa uinjilisti unahitajika uwe wa kiroho (Zechariah 4:6) siyo ya kushindana mali! Hata gharama ikihitajika ili kumfikia mtu kiwanjani, kiwanjani michezo isitegemee hiyo gharama! Hivyo tunapata pikta ya jinsi kazi ya mitume inavyotakikana. Maana yake, kiwanjani (kwa huduma yenyewe) mtume asitumia mali ya nje, na atumie lugha za wenyeji. Ndivyo hali inayowezesha usikivu wake.

6. Mitego iloyopo, na jinsi kuihepa

Mitego mbali mbali inawezakumsubiri mtume.¹⁸ Moja ambayo Wamisionari siku hizi wanaangukia inafuatana na sera inayosema hekima ya mwenyeji ni bora kushinda ufahamu wa mtume. Wamisionari na viongozi wao hutamani kusikia kutoka kwa wenyeji wafikiwa, na kufanya jinsi wanavyoshauriwa nao. Shida iliyopo na maelekeo hayo ni mawili, ya lugha na ya utegemeo. Lugha inayotumika sana kwa kazi za umisionari ni Kiingereza. Wakubwa wa wamisionari pamoja na wamisionari wenyewe wanajua Kiingereza. Shida inatokea wafikiwa wakijua Kiingereza. Hali ya wafikiwa kujua Kiingereza inamwezesha mkubwa aliyebaki Ulaya kufanya uhusiano moja kwa moja na mfikiwa, yaani kujifunza kwao kupitia Kiingereza, sawa na anavyofanya mmisionari aliye 'kiwanjani.' Swali linalotakikana liulizwe hapo ni – ikiwa uhusiano upo kutosha kupitia Kiingereza, kwa nini mtume au mmisionari kujifunze lugha ya wafikiwa? Jibu la swali hili ni, uhusiano kupitia Kiingereza kati ya yule asiyejua

¹⁸ Harries, Jim. 2009. 'Pragmatic Linguistics Applied to Bible Translation, Projects and Inter-cultural Relationships: an African focus.' 75-95 In: *Cultural Encounters: a journal for the theology of culture*, Volume 5, number 1, Winter 2009.

kitamaduni cha wafikiwa, na wafikiwa, ni duni. Wengi hawajalitambua jambo hili.

Wengi wa wafikiwa wanaoweza kuongea na wakubwa wa wamisionari ni wale waliosoma kabisa mila za Ulaya. Wamejua kuiga jinsi watu wa Ulaya huongee na kujieleza, na wanategemea Wazungu na mali yao. Mara nyingi, wanafaidika sana na mali kulingana na uhusiano wao na Wazungu. Sasa, watu aina hawa, wakitoa shauri, watahakikisha wasimkwaze Mzungu, na wasizibe njia za pesa kuingia kwao.

Kwa kifupi tunaweza sema Waafrika wengi wamejiendeleza kwa kuwategemea watu kutoka Ulaya. Kuendelea kuwategemea siyo shida kwao. Siyo rahisi wauumize mkono unaowalisha. Vile nimeshasema juu, ni rahisi Wazungu wenyewe wasijione wanaajibika sana kwa ajili ya wenzao Waafrika, sababu wanawaafrika 'wao' wanaowategemea kuwashauri. Ila hapa ninasema: haifai mfadhili kuwachukua watu kama hawa kumwelekeza. Kufanya hivyo ni Mzungu kutojiajibisha. Ni kuhenga majukumu yake. Ni kinyume cha haki. Badala yake, mfadhili anatakikana yeye mwenyewe awafuatilia na kufanya utafiti wake, ili ajue cha kufanya. Yeye mwenyewe, au isipokuwa mwenyewe, moja wa watu wake wakitamaduni chake ambaye atakuwa mtegemeo, lazima waajibike. Kuajibikwa kunahitaji yule mtu wa jamii ya wamisionari mwenyewe kujifunza lugha za wafikiwa, kusonga nao karibu, kuwafahamu, yaani kuwa msikivu kwao. Huyu basi anafaa asikizwe na wakubwa wake, wasimtegemee mwenyeji kuwashauri!

Mitume wanatakikana pia kujifunza kutoka kwa mambo yanayoelezwa juu. Maana yake, maelezo juu ya kazi za mitume wanayopokea kutoka kwa wamisionari kwa lugha za Ulaya, au yaliofafiriwa kutoka kwa lugha za Ulaya, yasiaminiki sana. Yameundwa kulingana na kitamaduni kigeni sana na hicho cha Kiafrika. Lazima mtume aombe Mungu, asome Biblia, awe na hekima jinsi anaendeleza uhusiano wake na wenzake, na ajifunze kulingana na muktadha uliopo, sio kutoka kitabu cha wasomi wa Ulaya. Ndivyo ataweza kuwa msikivu kwa kazi yake.

7. Uajibikaji uzidi kukaswa

Masharti ambayo nimeanza kueleza juu, ya mtume kufuata ili huduma yake ufue dafu, sio rahisi. Ugumu uliopo ndio unawafanya wengine wafikirie wakaze tu masharti hayo kwa *kiasi*. Maana yake, badala ya kulenga huduma yenye usikivu, wanataka wafanye huduma wanayofanya tayari ibadilike kidogo ili hali ya usikivu uongezeke. Kufanya mabadiliko siyo mbaya. Kweli, hali ya usikivu inaweza ongezeka. Pengine shauri tunalotoa hapa litamsaidia mtu. Lakini kwa hakika, njia inayoweza kumfanya mtume awe msikivu ni njia kamili na siyo nusu ya njia

tunayotaja hapo juu. Yaani, ni kufuata masharti yote, na siyo nusu: Ili mtume awe na huduma yenye usikivu, afuate kanuni kabisa, aanze huduma upya, siyo kubadilisha tu kidogo kile alichokuwa anafanya.

8. Kufanya huduma na mitume na wamisionari wengine

Sijasema lazima mitume wote, au wamisionari wote, lazima wafanye vile tumeleza hapa ili wawe wasikivu. Ila tunahimiza wengine wafanye, hata ikiwa wenzi wao wakiendelea na mbinu za 'kawaida.' Wale wachache wanaojitolea kuwa na usikivu basi ndio wanaohitaji wajikaze ili mbinu hiyo ifuatwe kamili. Wale wachache wanaweza kuwa, kwa njia mbali mbali, wategemeo wa wenzao wafanyao kazi kwa mbinu ambayo kwa wengi imekuwa ya kawaidia. Hekima inahitajika kujua jinsi kufanya huduma pamoja, wasikivu na wasiowasikivu.

Moyo ametambua jinsi wamisionari kutoka nchi za magharibi wanashindana. Kumbe badala ya kuhimizana, wanaweza wanashindana.¹⁹ Mambo hayo ya watu kushindana kwa kazi nachukua kama ni kawaida kwa binadamu. Ubaya, mara nyingi, kinachoshindaniwa, siyo hali ya usikivu, lakini mali: Mmisionari anayehesabika kufanyikiwa ni yule anayeweza kuwashurutisha wenye mali kumsaidia, na siyo yule anayeweza kuleta hali ya usikivu kwa anaowafikia. Hivyo ni kama mali yanatawala hata kazi za utume. Tunaweza sema mambo hayo yanahitajika yabadilike. Lakini ubaya, kuibadilisha ni kuwaingilia wamisionari au mitume wa 'kawaida', pengine kuwakwaza, kuwakasirisha, kuonekana kujaribu kuwashusha, kuwaaibisha, n.k. Ndivyo sababu wanaweza kuwadharau wenzao wanaojaribu kufuata mbinu za kuleta usikivu. Basi, mtume anayejaribu kufuata njia ya usikivu unaoelezwa hapa anawezachukuliwa na wenzake kuwa mwadui wao! Hivyo wanaweza kumstaki; kusema hafanyi bidii, anashindwa kupata msaada wa wafadhili, hawapendi wenzake (sababu muda wake mwingi anakaa na wenyeji wanaofikiwa badala na mitume au wamisionari wenzake), hahudhurie mikutano yao, hawasaidie wanapojikuta tabuni n.k. Kwa mfano, mara nyingi wamisionari wa kawaida hujiwekee mizigo mingi kikazi, yaani wanajikaza sana ili waifanyikishe kazi nyingi, na ili wafadhili wao wawasaidie mali kwa wingi. Mizigo hiyo ikiwa ngumu kubeba, wanatafuta sana wanaoweza kuwasaidia. Lakini wenzao wanaoeleka kuwa msikivu mpaka wahepe majukumu kama hayo.

¹⁹ Moyo, Levy, 2006. *The Gloved Handshake: Christian or Christianised Missions?* UK: Chosen Graphics Ltd., 90.

Mijadala hii ya juu nahesabu kuwa ya msingi sana. Uhusiano kati ya mitume wenye kutumia fedha na lugha za nje na wale wenye kutafuta usikivu unahitajika uwe schwari sana. Wanahitajika wasaidiane iwezakanavyo. Hasa mtume anayetafuta hali ya usikivu anawezajikuta anategemea sana wenzake, kwa mfano akigonjeka ili wasaidia kumtibu. Hali iliyokuwa kwa wamisionari kutoka nchi za magharibi kufanya mambo yao yote na mali ya nje n.k. inahitaji ibadilike, ili waweze kuwasikize wenzao wenye usikivu na kutambua umuhimu wa kuingilia kati ya watu wenyeji na siyo kupima ushindi kupitia tu kwa uwezo wao wa kusanya pesa kutoka nje. Yaani, kushindana kiwe kwa uwezo wa kuwa na usikivu, siyo kwa uwezo wa kuyapokea mali.

Mitume wenye usikivu wanahitaji wenzi wao kuwahimiza na kuwasikiliza. Wenzao wanaotumia rasilimali au lugha za nje wasipokuwa tayari kuwa karimu kwao, mbinu nyingine inahitajika kuwasaidia wenye usikivu. Pengine wenzi wao wakabila zao walikotokea, watu wanaowezakuwafahamu vizuri, wawe karibu kama washauri na wakarimu kwa ajili yao. Majukumu maalum ya hawa wakarimu yatakuwa kuwahimiza na kuwatia moyo wenye usikivu, ili waendeleo na bidii. Na pia kuwasaidia kufahamu, watakapokuwa wanapitia kwa ugumu, umuhimu wa kuendelea.

Mitume au wamisionari wanaotegemea lugha na msaada kutoka nje, wanakutana na changamoto nyingi kwa huduma zao. Changamoto moja kinachowasumbua sana, ni haba wa ujuzi juu ya kinachoendelea kwa mazingira yao. Maelekeo yao kwa mali kutoka nje ndiyo yanawanyanganya nafasi mengi kujifunza kwa watu wafikiwa. Mtume akiwa na mali nyingi, na akianza kuwagawia wenyeji, wataanza kumtegemea. Halafu itakuwa rahisi kwao kuanza kumdanganya mgeni wao ili upokezi wao wa pesa udumishwe.

Mitume au wamisionari wanaotegemea lugha na msaada kutoka nje wanahitaji kusaidiwa ili wafahamu kinachoendelea kwa jamii lengwa. Wanaweza tamani wasaidiwe na wenzao 'wasikivu'. Lakini, hapo msikivu mwenyewe asipotahadhari, uhusiano wake na 'mtajiri' mwenzake unaweza kuishusha usikivu wake! Kwa ajili wengi wa wenyeji wanahitaji ya mali, lazima wawe wanashindana kuwa karibu na mtume mwenye mali, na wajaribu kuaminiwa naye, ili waweze kumshawishi juu ya njia ya kutumia pesa yake. Mmisionari au mtume 'mtajiri' akionekana anamtegea masikio yake mtume au mmisionari mwenzake msikivu, huyu msikivu atapata sauti juu ya ugawaji wa mali. Ubaya, hiyo nguvu juu ya mali ya wenzake ni karibu sawa na kuwa na mali yake mwenyewe! Sasa, badala ya kuaminika kwa ajili hana mali kugawanya, atatambulika sawa na mwenye mali. Kwa mfano, akimsaidia mtajiri kuamua mahali pa kuelekeza mali

fulani, mali hiyo yanakuwa kama mali yake yakusaidia nayo watu, lakini msingi moja ambao tumejadiliana juu, ni asiwe na mali!

Sababu ya hatari ya kulaumiwa akimsaidia mtume au mmisionari mwenzake anayetumia mali kutoka nje kuamua jinsi mali inatumika, hali ambayo inafanya mali iwe kama ni yake mwenyewe, mtume anayetaka awe msikivu lazima ahepe uhusiano wa karibu sana na mitume wenzake wanaofuata mbinu za huduma za 'kawaida'. Maana yake: mtume msikivu hatakikana amsaidia yule ya kawaida anayetumia pesa na ujuzi wake! Akimsaidia, ni kama anajiunga na mwenye mali huyu, na ndivyo yeye siyo msikivu tena, sababu wenyeji watageusha maelekeo yao kwake wamchukue kama mwenyewe ni mwenye mali. Ndivyo ni ngumu kumsaidia mtume au mmisionari anayetumia mali kutoka nje, panda ya wenyeji na hata na wenzake wasio na mali, hali ambayo inaharamisha huduma inayotumia mali kutoka nje kwa jumla.

Kwa Ufupi na Hitimisho

Maandishi haya yanatetea hali ya usikivu kwa mtume au mmisionari, kwa wale wanaoipinga. Kuwa msikivu kwa Mungu ni kitu kimoja muhimu kwa mitume. Kingine kinchochunguzwa hapa ni usikivu kwa watu. Neno la Mungu ili wafikiwa walifahamu lazima lihusike na muktadha wao waliopo. Pasipo usikivu unaopatikana ukitumia lugha yao, na kutokuwa mkubwa kila wakati sababu ya kuwa mwenye asili ya mali, mtume mgeni hataweza kuwafahamu vizuri watu anaowalenga. Atabaki akiwasikia wachache ambao wamejifunza lugha yake, ambao kawaida wachache hawa pia wanahamu ya kupokea mali kwake. Amri ya Yesu ilikuwa tofauti. Angalia Luka 10:1-4. Aliwaamuru wanafunzi wake, wakienda kufanya huduma, wasibebe mali! Kwa nini? Ili wawe masikivu. Huduma ya kiroho inaweze shwa na usikivu wa mhudumu.

Asipojitahidi, ni rahisi mtume aiangukia hali ya kuwa mtegemeo wa mali yake kutoka nje kwa huduma yake. Ikiwa mali ya nje peke inamwezesha kufanya huduma, wenyeji wasionayo watawezaje kufanya anavyo fanya? Hali ya Kiafrika, kulipwa fadhili na sifa, inamaanisha mfadhili anadanganywa. Ufisadi na usio-*kweli* ambao unajitokeza ni kinyume cha mapenzi ya Mungu. Ili awasaidia wenyeji kumwiga, mtu kutoka nje lazima ajifunze ku 'cheza' kwa mazingira sawa na yale ya wenyeji. Tumelinganisha huduma ya utume na uchezaji wa spoti, kama ya mpira. Sera za utume zisitegemee ushauri wa wenyeji wanaotumia lugha isiyo yao na rasilmali kutoka ugenini. Kuwawezesha mitume kuwa na usikivu kunahitaji wenzake, mitume wala wamisionari wasio wa usikivu, kumkubali, kumsaidia, kumhimiza, na kumkubalia asimame mbali nao kidogo sababu

mienendo ya wamisionari wa kawaida anayetumia pesa kutoka nje kusu-
kuma huduma wake ni sumu kwa mtume msikivu akiwa nao karibu.

Hali inayoleta usikivu siyo kufanya mabadiliko kidogo kidogo kugeusha
huduma ya kawaida, lakini ni kuwawezesha wenye sera tofauti sana
ambayo ni kinyume cha kinachoendelea.

7. Kiingereza ni lugha itakayotuokoa? Kiingereza siyo lugha ya Mungu.

Mafupisho

Kulingana na uzoefu wangu wa kimaisha, na kazi za wasomi, najaribu hapa kupinga wazo linalohesabu Kiingereza iwa lugha ya dunia, na hivyo kufaa kwa matumizi ya watu wote. Kiingereza cha asili kimejengwa juu ya mizizi ya imani kibiblia. Kiingereza zingine zozote sivyo. Wanaozidi kusesitiza ubora wa Kiingereza hudhani lugha zote zina uwezo sawa ya kueleza mambo, pasipokujali mazingira na aina watu wanaotumia lugha hiyo. Ni wenyeji wa nchi nyingi hasa waliotamani na bado wanatamani sana Kiingereza. Wenye asili ya Kiingereza wanaweza kutumia nguvu nyingi kusambaza lugha yao bila kufikiria kutosha cha ndani juu ya athari ya kufanya hivyo. Siku hizi Kiingereza husambaa jinsi ungefikiria ndiyo Mungu! Ndivyo kumbe lugha imechukua nafasi ya Injili ya Yesu.

Utangulizi

Kuwa mzaliwa wa UK, kunanifanya kuwa mmoja wa wanaojua Kiingereza cha asili. Kuishi Afrika, Zambia halafu Kenya, 1988 mpaka sasa, kimenipa mazoezi ya utumizi wa Kiingereza zingine kwa mazingira ya wasiojua lugha asili. Kwa miaka 20 nilifunza Neno la Mungu kwa bara la Afrika kupitia lugha ya Kiingereza. Baadaye niligundua ya kwamba kufanya hivyo hakukuwa na msingi mzuri. Nataka kueleza hapa sababu zilizofanya imani yangu kwa Kiingereza kufifia. Ni kweli, sio wote wamefurahia msimamo wangu wa kutoithamini Kiingereza kama lugha ya mataifa na lugha ya kuleta maendeleo.

Kuna watu wanaotumia Kiingereza kama lugha ya pili ili kuwaweze-shea uhusiano wa mataifa. Siwezi kuyapinga matumizi hayo sana, lugha nyingine (au zingine) zikiwa zinazidi kuwa msingi wa maisha yao. Hatari ninayoashiria ni kwa wale wanaothubutu kuitumia Kiingereza badala ya lugha zao kujiongoza na kutekeleza mambo yao, ikiwa kanisani, katika elimu, n.k.

Wanaojua Kiingereza ya Asili wako mbele

Kumbe Kiingereza kile ambacho kinachacha watu zaidi, kulingana na Ha, ni hiyo ya wanaoongea kiasili (2016:352). Pia Morrison anasisitiza; vile wanaoongea Kiingereza ya asili huharibu maongezi!²⁰ Yanasikitisha kwa mba wengine wanaokitumia Kiingereza, hawafurahishwi na wanaokitumia Kiingereza cha asili! Wenye lugha ya asili ndio wanaoweza, kuathirika kwa njia hiyo kwa ajili ya Kiingereza kutumika duniani pote. Ni ngumu kwa wenye asili ya Kiingereza kujiingiza kwa mijadala ya wengine bila kuleta hali ya kutokuelewana. Ni ngumu kwao kugundua anachomaanisha anayeongea Kiingereza za kienyeji zisizokuwa za asili.

Kwa nini nasema wenye Kiingereza ya asili wanashindwa hivyo? Vijisababu ni vingi. Wenye Kiingereza za kienyeji (yaani, zisizo za asili) hupokea maneno ya Kiingereza, na kuyaweke maana kulingana na asili zao. Kwa mfano, wanatumia neno fulani la Kiingereza kutafsiri neno fulani lao. Kwa hivyo wenye asili ya lugha wanadanganywa; wakiwa wanafikiri wanajua maana ya maneno yanayotajwa, lakini kwa hakika, hawajui. Ubaya, Kiingereza ikiwa lugha ya mawasiliano, ukalimani haupo. Wenye asili ya Kiingereza huendelea kudanganywa wanafahamu mambo ambayo kwa hakika hawajajui, yanayoelezwa kutoka sehemu nyingi duniani.

Wenye asili ya Kiingereza wakiongea nje ya mazingira yao, ugenini, ni rahisi wakose kufahamu kwa sababu zifuatazo:

- 1) Wengi wao wanajua tu lugha moja.
- 2) Wengine wanaotamani kujifunza Kiingereza cha kiasili wanaogopa kuwarekebisha wanaoongea Kiingereza hiyo ambayo wengi wao ni wenye nguvu za mali na uwezo wa kuathirisha.
- 3) Wanaoongea kiasili hufahamu mambo mengi na maneno yao hushinda yanayoelezwa na kamusi.

Kinachosababisha shida inayotajwa juu ni Kiingereza cha asili kuchukuliwa kuwa ni ya dhamani sana. Wengi wanaojifunza Kiingereza hujaribu kuiiga lugha ya asili kama mfano bora (Ha 2015:240)! Watu wengi kwa nchi mbali mbali hasa Afrika hawapendi kuwakwaza wenye asili ya Kiingereza. Badala yake, wanaweza tumie ujanja usio wa kweli; kwa mfano kukubali tu wamefahamu maneno yote yanayotajwa. Kwa hivyo, panda ya uhusiano kupitia Kiingereza, sababu mwenye asili ya lugha anahesabiwa hawezi kosa na anaigwa, wengine huendelea tu bila kueleza makosa yanayoingia

²⁰ <http://www.bbc.com/capital/story/20161028-native-english-speakers-are-the-worlds-worst-communicators>

kwa panda ya kufahamiana.²¹ Uhusiano hauwi barabara, lakini asiyejua hiyo kumbe ni mwasilu wa Kiingereza!

Mambo yanayotajwa juu yanaonekana wazi kwangu kila siku nina-poishi Afrika ya Mashariki: Kama yule anayejua lugha mbili za Kiafrika, nawezachagua lugha ya kutumia kuongea. Nikitumia Kiingereza, kuongea kwangu huathirika kulingana na asili yangu. Yaani, naongea na kufahamu lugha kiasi kubwa kama mtu mwenye lugha asili. Hii inafanya lahaja yangu, utamushi wangu, sarufi yangu, na hata uamuzi wa neno la kutumia, yawe tofauti na ya wenyeji wenzangu. Nikiwasikia wenyeji wakiongea, ninapewa kazi ngumu nikijaribu kugundua jinsi maneno yao ya Kiingereza huhusika na maisha yao. Lakini, kinyume cha hiyo, tukitumia lugha yenye asili ya Kiafrika, kwa mfano Luo au Swahili (lugha ninazozijua) shida hiyo haitokee. Hii ni sababu natumia maneno niliyojifunza Afrika, vile hutumika katika mazingira ya wenyeji. Naweza kujua moja kwa moja kile ambacho mwenzangu anajaribu kusema, bila kuchanganywa na vile neno linatumika Ulaya. Utumizi wa Kiingereza unaleta hali ya kuchangan-yikiwa, watu wakiyataja maneno ambayo wamejifunza shuleni lakini ambayo hawawezi kuyahusisha na mazoea yao ya kila siku maishani.

Hisia za mwenye kutumia lugha zinafaa pia kutajwa. Nikiongea na Waafrika kupitia lugha ya Kiafrika ninatambulika moja kwa moja kama yule ambaye ametumia muda wake ili ajuane na watu, amekawia Afrika, anawajali watu n.k. Kinyume cha hayo, nikitumia Kiingereza, ninasikika kama mgeni asiyejua na asiyejali maisha ya ndani ya wenyeji.

Ukiwauliza watoto wa Afrika sababu zao za kufurahia kujifunza Kiingereza, majibu ambayo nimezoea yanafanana; ili siku moja waongee na Mzungu, au ili waweze kutengeneza uhusiano na watu kutoka nje ya nchi, na hata siku moja wasafiri nje ya nchi (linganisha na Tupas and Rubdy 2015:13 na Ha 2015).

Wenyeji kutoka sehemu mbali mbali wanaoongea Kiingereza wana-weza pia kutofahamiana vizuri. Wanaweza kulinganisha neno fulani la Kiingereza na zaidi ya jambo moja. Yaani, neno moja kwa Kiingereza linaweza tafsili jambo au neno fulani kwa lugha ya mtu mmoja, lakini jambo lingine kwa lugha ya mtu mwingine. Utofauti na wenye asili wa Kiingereza, wanaotumia Kiingereza kama lugha ya pili, wanayolugha nyingine pia. Sababu wanayo lugha nyingine kutumia kwa mazingira kadhaa, Kiingereza zao hutumika tu kwa mambo kadhaa, na mambo mengine hutajwa na maneno ya lugha zao. Mara nyingi Kiingereza hutumika kwa mijadala kinachokuwa rahisi tu na ya juu juu. Ili waeleze jambo kwa ndani, wanaingia kwa kutumia lugha zao.

²¹ Nasema kulingana na mazoezi yangu ya kuishi miaka mingi Afrika.

Utumizi wa Kiingereza unaweza kuwa na maana moja kwa wanaoongea lugha fulani. Maana hiyo wanawezakuwa wanajua ni yao tu na wengine wasiojua hio lugha kiasili fulani yao hawataigundua. Kwa mfano, Waluo wa Kenya wanalo neno *chira* kwa lugha yao (Mboya 1978). Kulitafsiri hilo neno kwa Kiingereza ni ngumu. Pia, mambo yanayotajwa na hili neno hayakubaliki na Wazungu.²² Badala ya kulitafsiri basi, mjaluo akiongea Kiingereza, anafahamutu jinsi mjaluo mwenzake atagundua haraka juu ya uwepo wa hicho kitu, *chira*, hata asipolitaja neno *chira* lenyewe. Wasiowenyeji wa Luo hawatagundua jambo hili, kwa hivyo kwao Kiingereza kinachotumika kitabaki na pengo; kitakuwa na fumbo kisichogundulika (Harries 2012:47).

Mara, wenye asili wa Kiingereza huwafikiria wasio wenye asili, kwa mfano Waafrika wengi, kukosa hekima na uwezo fulani kwa ubwongo wao (Chowdbury 2014: 9). Wenye asili huwapokea wasiowaasili ya Kiingereza kama wasiotafakari jambo vizuri, wasioweza kuchangia kwa mjadala hata kwa mambo rahisi, n.k. Wenye asili wa lugha huwaona wengine kuwa na upungufu. (Mara nyingi jambo hili husababisha ubaguzi wa rangi.) Swali nyeti linatajikana kuulizwa hapa. Je, lugha moja, Kiingereza, ni kipimo kifaaacho cha akili za watu wote duniani? Je, siyo inawezakuwa hawa watu watahesabika wenye akili timamu kabisa wakiitumia lugha yao kati ya wenzao? Mazoea yangu yamenionyesha, nikiongea na wenyeji wa lugha ya Kiswahili au Kiluo, ni mimi ninayeonekana kukosa akili. Kuongea vyema na wenye asili wa lugha kupitia lugha yao wakiitumia ya ndani kulingana na muktadha wao, na wewe siye mwenye asili ya hiyo lugha, ni ngumu sana! Tuseme basi, Kiingereza cha asili kinatumika kulingana na mazoea fulani ambayo wasio wenye asili ya lugha hawawezi kugundua, ila kwa ugumu sana!

Biblia

Wengi wanaochunguza Kiingereza zinazokuwepo siku hizi hawajali na hawabali jinsi lugha iliyotengenezwa na imani ya wenye asili ya lugha hiyo kupitia Biblia na Ukristo. Swali linalofaa liulizwe ndilo hili; kwa nini ni Kiingereza kinachopendeza dunia mzima? Wengi hudhani tu ni mambo ya pesa, na Kiingereza ni lugha kujifunza ili upate mafanyikio kiuchumi au kisiasa. Hapo mambo yanaishia kweli? Kwani kitamaduni cha wenye asili ya Kiingereza hakina umuhimu wo wote? Lugha hiyo ilipataje kuwa na sifa ya ajabu vile ilivyo? Ukiangaliatu kidogo, utaona wenye asili ya Kiingereza

²² Maana yake, neno linataja mambo yanayohusika na ushirikina.

waliathiriwa sana na Ukristo, hasa Ukristo wa Uprotestanti.²³ Kiingereza imejitokeza kuwa lugha ya kipekee duniani, nasadiki, kwa sababu imekuwa lugha ya WaKristo, tena WaProtestanti, wenye bidii kuchunguza Neno la Mungu, yaani Biblia.

Nitaangalia sehemu chache tu la Biblia. Kwa hivyo, msomaji wangu afahamu nagusa tu maada hii. Kitabu cha Kwanza cha Biblia, ambacho ni kitabu chenye msingi sana kwa Wayahudi pamoja na Wakristo, kinasema, Mungu akiongea na Ibrahimu: “nami nitakufanya wewe kuwa taifa kubwa ... na katika wewe jamaa zote za dunia watabarikiwa” (Mwanzo 12:2a na 3b). Katika Galatia 3:8, Paulo anatumia baraka huja kupitia imani. Kwa hivyo, Wakristo kwa jumla huamini uaminifu wao kufuata Biblia utamfanya Mungu awatumie kusambaza baraka zake kwa dunia mzima.

Wakati huu, watu wengine hawaoni jinsi msingi wa mafanikio duniani unatoka penye Neno la Mungu (Vattimo and Girard 2010). Jinsi wenye asili ya Kiingereza wameathirika sana na Injili ya Yesu kwa vizazi vingi haitambuliki. Kwa wanaofahamu, kusambazwa kwa Kiingereza duniani basi tunaweza sema kunakuwa:

- 1) Aina moja ya utekelezaji wa unabii uliomo Biblia.
- 2) Au, matokeo ya hali ya kutofahamu, sababu wakati huu ni Kiingereza kinachositawi na kusambazwa badala ya Neno la Yesu.
- 3) Kuhimiza hali ya kutumia Kiingereza kinafahamika kuwa mbinu za kuleta baraka duniani pote.²⁴
- 4) Matokeo ya nchi za Ukristo kubarikiwa na Mungu, ambao sasa wanataka baraka hiyo iende kwa dunia mzima.

Maneno yanayo juu yanaweza kutufanya tujiulize, je, ni sawa kuisambaza lugha badala ya Injili ya Yesu? Binafsi nasema la; siyo vizuri kuipa lugha nafasi ya Injili.

Katika sura kumi na moja ya Mwanzo, tunasoma juu ya Babeli. Tunachojifunza hapo ni vile Mungu hafurahi na jitihada za binadamu kuhimiza utumizi wa lugha moja popote duniani (Mwanzo 11:6-7). Mungu

²³ Mekanisa mengi yaliyoanzalishwa na wamissionari nje ya nchi za Magharibi hujiiita Protestanti. Lakini, hata wakijiita vile, wengi wa makanisa hayo wanakiuka msingi moja thabiti ya Uprotestanti, ambao ni kusema Neno la Mungu linafaa lichunguzwe kwa lugha za watu wenyewe na siyo lugha geni. Utumizi wa Kiingereza sana nchi za Africa unakiuka msingi huo sababu Kiingereza siyo lugha yao.

²⁴ Ndivyo Amerikani, nchi yenye msingi wa KiProtestanti, inajifahamu kuwa na wajibu wa kubadilisha na kuboresha maisha ya watu dunia mzima.

alishuka ili achanganye lugha yao, Biblia inatuambia, baada ya wakina WaBabeli kujaribu kusambaza lugha moja tu. Hapo Mungu hueleza wazi kufurahia kwake panda ya utumizi wa lugha nyingi.²⁵

Wanao haribu umoja wa Watu

Wengine hujaribu kuvunja utawala wa Kiingereza ya asili, wakijaribu kuingilia ushikamano wake na uhusiano wake na wenye asili yake. Kachru ni msomi moja aliyesisitiza sana kusema Kiingereza ni nyingi, na kila aina ya Kiingereza inakuwa na thamani sawa na nyingine (McKay 2002:50). Kulingana na Kachru wenye asili wa Kiingereza hawawezi kuzilainisha Kiingereza zote popote duniani (1985:30). Kwa hivyo, lazima wakubali tu hali ya Kiingereza kuwa nyingi. Kachru alitabiri mbeleni Kiingereza zitakuwa nyingi dunia mzima, *na hakuna Kiingereza moja itakayohesabika bora au ya msingi kushinda nyingine*. Lakini bado alisisitiza pia, uhusiano kati ya watu utakuwatu sambamba, pasipo matatizo (McKay 2002:51). Ni kama alifikiria kila aina ya Kiingereza kitafahamiana kwa rahisi na Kiingereza kingine; yaani, utumizi wa lugha haujaliki kuwa na makini.

De Costa, Park na Wee hupinga jinsi uhalisi wa Kiingereza unao hesabiwa siku hizi (2018). Wanatueleza vile mbinu za kuipima Kiingereza imekuwa imeegemea sana kuithamini Kiingereza kulingana na jinsi itakachompa mtu uwezo wa kujitegemea (2018:3): Yaani ubora wa Kiingereza siku hizi hupimwa kupitia mbinu fulani ya kuithamini iwe lugha ya kumfanyikisha mtu kibiashara (2018:10). Watu hulinganishwa duniani pote kulingana na uwezo wao wa Kiingereza (2018:13), hali inayowafanya wengine kutamani Kiingereza zaidi na zaidi, hasa nchini Korea (Park 2009). Kwa ufupi; mbinu zinazotumika kupima Kiingereza na kuzilinganisha kulingana na utumizi duniani nzima siku hizi, unafanya tamaa ya kujua Kiingereza iwe hali ya juu zaidi. Ni kama; anayefanyikiwa kuongea Kiingereza safi atatajirika, anafaa heshima nyingi, na asiweze kudharauliwa. Kulingana na ufahamu huo, Kiingereza ni lugha yenye nguvu sana. Pasipo Kiingereza huwezi fanyikiwa sana nchini Korea, kwa mfano (Lorente and Tupas 2014:72). Watu hujihesabu kuwa wa kiwango cha chini wasipoweza kuishika Kiingereza. Na kipimo cha Kiingereza kwa uhakika ni kiasi ambacho kinafanana na ile ya wenye asili wake. Mbinu kama hio ya CEFR²⁶ unahesabika unasimamia ujuzi na ukweli wa haki (De

²⁵ <https://jimsayers.wordpress.com/2016/06/15/babel-nations-and-empire-builders/>

²⁶ The Common European Framework of Reference for Languages: Learning, teaching, assessment. (Mpango wa mataifa ya Ulaya juu ya jinsi ya kupima

Costa, Park and Wee 2018, 17). De Costa, Park and Wee hawafurahie hali hiyo. Wanataka kuweka wazi mizizi ya hali ya kuinuliwa kwa lugha ya Kiingereza ili kuwasaidia watu wajiepushe na balaa inayokuja.

Alogali (2018) anamfuata Kachru (angalia mjadala wa juu). Anacho lenga Alogali ni mema; watu wasiojua Kiingereza (ya asili) vizuri wasikose kusikika. Yaani, Kiingereza zote zisikike sawa duniani pote (2018:55). Anatuambia kweli kwamba; utawala wa Kiingereza unakuwa ukoloni wa kisasa (2018:56). Anachosahau Alogali ni kazi wanaofanya wenye Kiingereza cha asili. Hajagundua jinsi, pasipo kazi zao, mambo mengi mazuri yanayofanywa duniani yangukuwa hatarini.²⁷ Kinachowawezesha kufanya wanavyofanya ni uwepo wa lugha ambayo ni yao kutumia kulingana na ufahamu, mila, na lengo lao. Alogali akifanyikiwa, watu wote wenye Kiingereza mbali mbali watalazimika kusikika sawa na wenyeji wake wa asili. Kiingereza itageusha maongezi kufanana na hiyo ya mwendawazimu, sababu kueleweka hakitakuwa msingi wa kubalika maneno yako rasmi! Alogali anasema Kiingereza inatakikana iruhisiwe kutumika kwa mbinu nyingi tu (2018:69), bila kujali jinsi kufanya hivyo kutavuruga msingi wake kabisa.²⁸

Ni rahisi kuona sababu gani Alogali anasema asemavyo kufuatana na maelekeo aliyopata kutoka Kachru. Lakini Kachru amesikika na watu wengi. Alogali yu sawa kusema wasiojua Kiingereza cha asili wako nyuma. Lakini sioni ikiwa mbinu anataka kutumia kuwapa nguvu sawa na wenye asili ya lugha itaweza fua dafu (Alogali 2018:55).

Kiingereza zinazotumiwa sehemu mbali mbali duniani, tunaweza sema kwa njia nyingine, siyo lugha. Hazifiki kiwango cha 'lugha' hasa, kwa sababu zinatumiwa tu kwa eneo fulani ya maisha ya mtu. Zinawezesha uhusiano kati ya makabila na mataifa mbali mbali kwa kiasi, sawa. Lakini hazifiki kilindini penye maisha ya watu wala hazileti ufahamu wa kamakini. Kwa hivyo, haziwezi chukua nafasi za lugha za wenyeji za

kiwango cha ujuzi wa lugha.) <https://www.coe.int/en/web/common-european-framework-reference-languages>

²⁷ Ushirika unaojaribu kuwasuluhishia watu shida zao za jamii, kutoka nchi za Magharibi, wamefunyika dunia, kulingana na Bronkema (2015:211). Hali hiyo inaleta na kuongeza utegemeo wa nchi zingine kwa hizo za Magharibi, kwa hali na mali. Ila, utegemeo huo hufichwa machoni pa watu. Baada ya kuishi bara ya Afrika miaka zaidi ya 30 - naona hali hiyo ya kutawala kutoka mafichoni inazidishwa kila wakati. (Wazungu wanaotawala hawapendi kutambulika ili wahepe kuitwa wakoloni, au kuchukuliwa kama wenye ubaguzi wa rangi.)

²⁸ Anachotushawishi kufanya Alogali ni sawa na kutoa kipimo chenye uchapishaji wa vitabu na majarida, ili kuruhusu uchapishaji wa maandishi ambayo wakati huu watu wangepinga. Hatua aina hiyo, ni kuvunja msingi wa usomi.

wanaozitumia. Mbali na hiyo, tunachoona mara nyingi ni vile utumizi wa Kiingereza huharibu nguvu ya lugha za wenyeji zingine kwa sababu uwepo wa Kiingereza unafanya lugha hizi pia zinakosa kutumika kwa sehemu zote za maisha.²⁹

Wasio wenye Kiingereza asili wanazo lugha zingine za kujaza pengo ambazo Kiingereza haziwajazie. Lakini, wenye asili ya Kiingereza hutumia lugha hicho hicho kwa yale pia. Hapo ndipo, napendekeza kusema, upo utofauti moja wa msingi kati ya Kiingereza za watu wengine, na Kiingereza yenye watu wa asili ya Kiingereza. Tunaweza sema pia, tunayoangalia hapa ni sehemu ya lugha isiyo funzwa darasani, ila maishani. Inabeba mambo kama ya pilka pilka za nyumbani, na yanayoeleza au kufafanuliwa na vitamaduni vya watu ambavyo pia hutofautiana. Lakini sehemu hiyo ya lugha ya ndani ni lazima iwepo ili maisha ya kawaida ya akina binadamu yaendelee.

Kuiweka kando Kiingereza ya asili na badala yake kuziweka Kiingereza zingine zote kama ziko sawa, ni kujaribu kuharibu maisha ya wanaotumia Kiingereza ikiwa lugha yao. Yaani, kujaribu kuyaangusha mambo yao. Ni kama kujaribu kuwanyang'anya lugha yao! Kwanini kubomoa kimoja ili tukijenge kingine? Suluhisho nyingine inahitajika; isiyo kuharibu Kiingereza asili ili zijengwe Kiingereza za wenyeji mbali mbali. Kwa nini kutowachilie watu lugha yao, na kupanga msingi mwingine uwe wa watu wote? Hata wenye Kiingereza asili, wanatakikana wajenge wengine bila kujiharibu wenyewe, yaani wafahamu umihimu wa kuwasaidia watu wasio wenye asili ya Kiingereza waitumia lugha yao na siyo hiyo ambayo siyo yao. Kiingereza za wasiokuwa wenye asili wa Kiingereza, pengine siyo suluhisho hasa. Kwa hivyo, kulingana na mimi, maneno ya Kachru na ya Alogali yanakosa msingi thabiti na ya maana.

Wasomi wenyewe, Ha anatuambia, hutumia kiwango cha Kiingereza cha juu (2016:355). Kwani kuwaambia wengine kubadilisha Kiingereza zao siyo shida, wenyewe wakitahadhari wasifanye hivyo wenyewe kwa kazi zao? Kachru akisikika sana, hata mjadala uliopo juu ya Kiingereza mbali mbali, kumbe utakwama.

Kiingereza ya asili kipambau mbele

Kumbe ukweli wa mambo ni, watumizi wa Kiingereza wanazidi kujikaza ili waige ile Kiingereza ya asili (Tupas and Rubdy 2015:15)! Waliotamani Kiingereza ziwe nyingi zaidi na zaidi wamekwazwa na hali ilivyo hii. Siku

²⁹ Kwa mfano, Kiswahili ya Kenya haifiki kiwango cha kutawala nchi, sababu uamuzi wenye utawala wa juu wa nchi unafanywa kutumia Kiingereza

hizi wanaotaka Kiingereza zao zikaribiane na ile ya asili, wameongezeka. Sababu yake inaweza kuwa vile utandawazi unawawezesha watu wengi zaidi mbali mbali karibu pote duniani kukutana na Kiingereza ya asili (Ha 2016:354). Ndivyo wanavyojifunza kutamani kuijua!³⁰

Mizizi ya Lugha imo penye jamii, na siyo kwa mashirika

Ni akina sherikali ndio waliopanga lugha za watu kwa karne ya ishirini (Blommaert 2019:1). Nchi mbali mbali wakatumia sera inayofanana, sehemu yake moja ikiwa nchi kuweka lugha moja ya Ulaya iwe lugha rasmi, hasa kutumika kwa kuhusika na maendeleo. Lakini, sera hiyo sehemu nyingi haijafanyikiwa (2019:1). Kwa nini? Sababu wasomi wa mambo ya lugha wameendelea na hitilafu ya kutofahamu jambo ambalo najaribu kueleza hapa. Hali ya maisha yao imekuwa kinyume cha lengo lao (2019:1). Yaani – wasomi kwa mfano kati ya wananchi wa Afrika wanaendelea kuegemea kwa Kiingereza, hata wakijua kufanya hivyo ni kuelekea penya balaa.

Blommaert mwenyewe anaorodhesha shida tatu maalum panda ya sera za lugha zinazoendelea kutumika mpaka sasa nchini mbali mbali (2019:1-3). Uwezo wa kujiendeleza kumbe haupo ndani ya lugha (Blommaert 2019:4); siyo kutumia lugha ya walioendelea kunacholeta maendeleo, ila kunaleta hali ya kuwategemea. Kudhani sababu Kiingereza ni lugha ya walioendelea, wengine wakiitumia hawa pia watafanyikiwa vile vile, ume-kuwa udanganyifu. Uhusiano kati ya lugha fulani na kitamaduni chake unatajikana uchunguzwe zaidi, sababu uhusiano huo ni wa kilindini.

Lugha zote siyo Sawa

Sera za lugha za kisasa zimepangwa na waaminao juu ya usawa wa lugha zote (Tupas and Rubdy 2015:1). Ndivyo umekuwa msingi wa sera za usambaji wa Kiingereza. Kulingana na Tupas and Rubdy, imani juu ya usawa wa lugha imewapofusha wengi ili wasigundue athari za Kiingereza kwao (2015:1). Imeaminiwa Kiingereza zote ziko sawa, na Kiingereza haziwezi kuegemea panda moja au nyingine. Lakini – ukweli ni Kiingereza zote siyo sawa (2015:3). Uhimizo wa utumizi wa Kiingereza badala ya lugha

³⁰ Hali ya kutumia lugha moja kuwaunganisha watu mbali mbali ni sawa watu hawa wakiwa chini ya utawala moja, kwa mfano wenyeji wa nchi moja. Hali haifai kwa watu wa nchi tofauti. Kwa mfano, inawezafaa waTanzania wote watumie Kiswahili, lakini siyo kuwalazimisha watu wa nchi nyingine kutumia Kiswahili, isipokuwa wakiitumie tofauti na WaTanzania.

za watu unaweza kuwa usiwe na haki. Sababu Kiingereza ya asili inahesabika na wengi kuwa bora kushinda nyingine, kujifunza Kiingereza kwa wale ambao isiyo lugha ya asili yao, ni kujidunisha mbele ya wenye asili wake. Hayo, inaonekana kwangu, yanayo sababu yake yenye msingi.

Ubaya, sera za lugha zilizotengenezwa miaka ya juzi baada ya vita vya pili ya dunia, zinaonekana hazitafua dafu. Ni sababu zilijengwa juu ya msingi wa Ulaya ambao siku hizi hauaminiki tena: msingi unaodhania watu wote duniani wanafanana kiufalsafa na wenyeji wa Ulaya, wenye Kiingereza ya asili, jambo ambalo siyo la ukweli (Comaroff and Comaroff 2004:331).

Wanaosema lugha yo yote inaweza tumika po pote na iwe sawa, wamedanganywa (Tupas 2015:2)! Ukweli wa mambo ni, Kiingereza inahimiza mada za Ulaya (Ha 2015:223) na inaleta mafanyikio ikitumiwa kwa mazingira ya Ulaya. Kweli, Kiingereza ni lugha ya mafanikio bara la Afrika. Lakini, hiyo sio sababu wenyeji Waafrika wenyewe wanaiweza, ila sababu inafanyikisha kuingiza mali na miradi kutoka nje, hasa kutoka Ulaya.³¹

Kiingereza ya asili ikiwa mfano ambayo Kiingereza zote zinaiga ni shida sababu inamaanisha wenye asili wa Kiingereza watazidi kufaidika kwa hali ya kipekee Kiingereza zikiongezewa kutumika duniani popote (Ha 2015:228). Walimu wa Kiingereza kutoka nchi za asili watazidi kutaminika kushinda wengine. Watu dunia pote watabakishwa nyuma ya wenye asili ya lugha. Hii haimaanishi wenye asili ya lugha peke yao watafaidika. Hawa pia huweza kuumia: isicho haki ikizidishwa wote huumia. Kwa mfano, hali yao ya wenye asili ya lugha kutojua kunaweza ongezeko.^{32 33} Kuathirika kwa Kiingereza kwa nchi nyingi duniani kunapowazuie watu kujiendelea, wote huathirika.

Miaka ya karibu, watu wengi kutoka nchi za Magharibi, wamejitoa ili wahimize haki kwa binadamu duniani kote. Wamisionari wamekuwa ndani

³¹ Mambo hayo hudhihirika kwa njia nyingi. Kwa mfano, nchini Kenya, ushirika wa simu ulikuwa unasumbuka sana na ufiada. Ushirika uliopo wakati huu, aina ya Safaricom, huangaliwa kutoka nje ya nchi, na hivyo huendelea. Mfano wa pili ni jinsi mara kwa mara Kenya huhesabika kuwa na maendeleo kushinda hayo ya Tanzania. Sababu moja ya hali hiyo, ni Kiingereza kutumika zaidi sana Kenya kushinda Tanzania, hali ambayo inasaidia ushirika wa nje kutawala na hivyo kudumisha mambo ambayo nchini Tanzania huwaangukia wenyeji.

³² Tukumbuke jinsi tangu 1880 Esperanto ilitengeneza ili iwe lugha ya mataifa (http://esperanto.50webs.com/EsrGrammar-1_01.html). Esperanto haina wenyeji, sababu ni lugha iliyoungwa tu. Lakini wengi huona nguvu ya Kiingereza ikaishinda, na siku hizi Esperanto hutumika na watu wachache sana.

³³ Kwa mfano, nchi zinazoendelea zenye Kiingereza ya asili zinaweza lengwa na wahamiaji, ikiwa kwa uzuri au kwa ubaya.

ya mipango hiyo.³⁴ Inafaa tustaajabu, ikiwa kulingana na mjadala wetu hapo juu, kusambaza Kiingereza ndicho ugeukaji wa maadili, jitihada zao za kujaribu kufanyikisha haki kupitia Kiingereza lenyewe ni ugeukaji wa haki.³⁵

Ugeukaji wa haki mwingine ni kuitangaza Kiingereza kama lugha ambayo haina dini. Hivyo mizizi yake inayotokea penye injili na biblia inafichwa (Harries 2015:5). Yaani kufanya hivyo naona ni udanganyifu. Ingekuwa haki kuitangaza Kiingereza vile inakuwa; lugha ambayo imeathirika sana na Ukristo. Kwa hivyo, Kiingereza ni lugha ambayo, ili itumike vile inatumika na wenye asili wake, inahitaji imani ya Ukristo.

Wenyeji waliohusika na usambaji wa Kiingereza

Brutt-Griffler ni msomi anayedhihirisha jinsi wenyeji wa nchi za Afrika na penginepo ndio walitamani Kiingereza sana. Maana yake, hawakulazimishwa kuifunza, ila walipendezwa wenyewe kufanya hivyo (2015:14). Kwa hivyo, haikuwa tu sera ya lugha rasmi iliyowekwa ikafanya Kiingereza isambae hata wakati wa koloni, bali pia wenyeji waliopendezwa na kujifunza hiyo lugha (Brutt-Griffler 2002:65 & 73-74). Wakati huu ni vile vile kulingana na zoezi langu. Kwa mfano, wanafunzi fulani wa chuo Kenya nilichofanya kazi wakataa lugha nyingine isiyo Kiingereza, hata ilipokuwa lugha ile ingewasaidia kihuduma.³⁶ Kiingereza kilitamanika. Hadi wakati huu, yeyote atakayepinga ufunzaji wa Kiingereza, ni rahisi akutane na upinzani kali kutoka kwa wanafunzi wengi duniani pote. Wenye dunia pote hawakulazimishwa Kiingereza, bali wenyewe waliitamani sana!

Mwajibika kumbe ni nani? Ni nani anafaa alaumiwe kwa kuwashurutisha watu wazitupe lugha zao waipokee nyingine kutumia? Hata ikiwa ni wenyeji waliopenda sana kutumia Kiingereza, bado tunaweza kujiuliza ni akina nani walioandaa muktadha uliowaathiri ili wafanye vile?

Wanafunzi pia wana uchungu juu ya kutawaliwa kwa lugha geni?

Kulingana na Ha, wanafunzi wengi duniani pote, hata wakiwa wanapendezwa na utumiaji wa Kiingereza, kwa njia nyingine kupendezwa kwao ni shingo upande. Hali hiyo naona iko Afrika ya mashariki, hata ikiwa chini

³⁴ Angalia kwa mfano IJM, International Justice Mission (<https://www.ijm.org/>).

³⁵ Alexander (1999) anaeleza mambo hayo kwa njia nzuri.

³⁶ Shule ya biblia huko Kenya kati ya 2000 na 2010.

chini kidogo. Watu wangukuwa wanafahamu jinsi kujitegemeza kwa lugha geni kunawaumiza, wengi wangeweza kupendekeza mambo yabadilike! Ya ajabu pengine, wanaojaribu siku hizi kuleta haki duniani pote, kwa njia nyingine wakiitumia Kiingereza, ndio wanaoongeza hali ya kinyume cha haki! Kiingereza, ambayo siku hizi inahesabika ni mwokozi, bado inaweza fahamika kinyume kuwa ndiye Shetani.

Ni vipi wanafunzi duniani pote hutamanishwa kusoma kwa Kiingereza badala ya lugha nyingine, na hivyo kuchunguza mila na kitamaduni ya watu wageni badala ya kujaribu kujifahamu wenyewe? (Chowdbury and Ha 2014:4). Msingu huo ni wa kukosa haki, na ni msingi ambao mimi binafsi ninauona sana unaendelea. Watu wenye ujuzi nyingi na mazoezi ya huduma ya muda mrefu, nimeona mwenyewe panda ka Kanisa Afrika, wanaweza kuhesabiwa kuwa na hali ya watoto, sababu ujuzi unaodhaminika rasmi ni hiyo ya Kiingereza kutoka Uzunguni, na mila na kitamaduni cha kanisa la Ulaya. Ha anatupa mfano; nchini Malaysia wanafunzi wanaotoka nje hawajali hawabali kitamaduni chenye wenyeji wa hapo lakini wanafuatilia tu kujaribu kupokea ya mataifa, maana yake ile ya nchi za magharibi (2015:239).

Kiingereza kama lugha ya Mungu

Pengine kwa kutojua afanyavyo,³⁷ lakini kwa makini, Ha anatumielekeza kwa msingi mwenyewe uliowafanyisha kwa ukweli watu kuiegemea Kiingereza sana. Wanafunzi kutoka nchi za Asia, anatumambia, huunda jinsi Wazungu bora wanaokuwa, uundaji ambao ni tofauti na vile walivyo (Ha 2016: 238-9). Maana yake, wanawaza na kuwazua mpaka wanaweka kumbukumbu hali yasiwepo ila mawazoni, Mzungu vile anatakikana kuwa siyo vile alivyo. Wanafunzi mbali mbali kutoka Asia wanamwunda Mwaustralia (mtu kutoka Australia) hewani, ambaye kwa hakika hayupo (Ha 2015:240). Wanatheologia kumbe pia wanatambua utumizi aina huo; watu kujiwazisha au kufikiria hali inayoshinda jinsi ilivyo. Ndivyo pia tunamfahamu Mungu (McCormack 1984:452). Maelezo ya Ha yanatutoa penye eneo la

³⁷ Naandika 'kutojua afanyavyo' sababu siwezijua Ha alikuwa anawaza nini alipoandika. Pengine mwenyewe ametambua jinsi injili ndiyo msingi moja kubwa wa Kiingereza? Hata asipokuwa amegundua mwenyewe, anatupa sana maelekezo hayo!

secularism na kutuelekeza kwa mambo ya Mungu. Dini ndio inayotufahamisha juu ya mambo yasioonekana na macho.³⁸ Mambo yanapoonekana ‘hewani’, yasio na msingi kando ya Mungu, bado yawezakuwa na msingi thabiti kulingana na Biblia (1 Corinthians 3:18-20). Ha anapolinganisha Yoga na Kiingereza (2016:349), anasonga karibu zaidi na mada yetu: kwa msingi uvutaji wa Kiingereza hutokee sababu imekuwa lugha ya Wakristo, waliokaza sana imani yao kwa Mungu aliye juu. Kusema hiyo tena kwa maneno tofauti: utandawazi wa Kiingereza sasa ni matokeo moja ya Mungu kunge kupitia Yesu kujivutie watu wote duniani pote (John 11:25).

Siku hizi, Chowdbury na Ha wanatuambia, ni soko na muungano mengine mbali mbali, ambayo yanahesabiwa ‘Mungu’ (2014:16). Msimamo huo hutuelekeza panda ya uMungu, lakini unatubidi tufikirie pia; inayosimamia maendeleo ya kisasa, ya soko na penginepo, ni ipi? Miaka nyingi, watu hawakuishi vile wanavyoishi sasa. Maendeleo yanazidi kupamba moto duniani mzima: kwa nini? Kwangu naona ndiye Mungu, anayetufunulia kupitia neno lake la Biblia, na utatu wa Baba, Mwana na Roho Mtakatifu. Hayo yamefanya mpaka sasa nchi za Magharibi zihesabiwa walimu wa wengine (2014:15). Karasa za Biblia zinatueleza jinsi tangu zamani za kale watu wa Mungu (Yahweh) walijitolea kuwavuta wengine waingie ndani ya Ufalme wake.³⁹ Tamaa za wengine kuwaiga wenye asili wa Kiingereza kumbe inatokea kwa ajili mababu wa Waingereza walijizama kilindini katika kufahamu Ufalme wa Mungu. Jinsi awali wenye asili wa Kiingereza walijitolea kuwavuta wengine kwa Ufalme wa Mungu, ndivyo wakati huu wanatumia bidii kuwashurutisha wengine wajifunze Kiingereza! Bidii ile ile inahimiza watu. Ni kama, Kiingereza yenyewe, kama lugha, inafahamika na wenye asili ya Kiingereza inahali ya *kuokoa*, yaani ni mbinu ya wokovu, yaani ni badala ya Mungu, ni lugha ya Mungu. Kosa la wenye asili ya Kiingereza limekuwa, kulingana na Girard, kutokuwa na hali ya Ukristo wa kutosha.

Kulingana na yaliyo juu, suluhisho ya matatizo yanayoletwa sasa na Kiingereza kuwa lugha ya dunia mzima ni kujikumbusha juu ya na kuitikia hali ambayo inahitajika kurejeshwa, ya Mungu kurudishiwa hali ambayo sasa ni eneo ya lugha. Siyo lugha yenyewe lakini ni habari njema ya Yesu Kristo ambayo ni nyuma ya lugha inayofanya lugha idhaminiwa duniani pote. Hapo ndipo asili ya imani kwa Kiingereza iliyofanya isambae duniani. Bidii ya wenye asili wa Kiingereza kuisambaza, na jinsi lugha inasimamia

³⁸ Nachukua neno la dini kama tafsiri ya neno la Kiingereza *religion*, neno ambalo linaeleza hali ya Ukristo, ambayo ni msingi wa fahamu wa dini zingine, kulingana na Cusack (2015:5).

³⁹ <https://www.britannica.com/topic/Kingdom-of-God>

aina ya hali ya Umungu, ni kama tunamwona Mungu kwa Kiingereza “kwa kiyoo kwa jinsi ya fumbo” (1 Corinthians 13:12), jinsi wanafunzi wa Ha walivyogundua nchini Malaysia (Ha 2016:239-240).

Hitimisho

Kutafuta kufahamu vitendo na hali ya Mungu peke yake kunachoweza kusuluhisha ugongaji unaoendelea kati ya watu wanaoathamini Kiingereza bila kugundua asili yake ya KiMungu. Kumbe, ukweli ni msingi moja thabiti uliopo unaofanya lugha ithaminiki sana ni Ukristo vile ulivyoaminika na wenye asili wa Kiingereza (Mangalwadi 2011)! Wafalme wenye falsafa wanaotajwa na Chowdbury and Ha (2014:5), ndio walioathirika na maono ya kiBiblia. Siyo Kiingereza yenyewe ambayo ni ya uMungu. Mungu anaweza kuongea na watu kupitia lugha nyingine pia. Mungu mwenyewe ambaye Biblia inatueleza juu yake anatakikana arejeshwe utukufu wake, utukufu ambao umepewa lugha. Kwa nini nchi za Waprotestanti wamekuwa wakihimiza utumizi wa lugha zao sana? Sababu wameihamisha bidii ya msingi iliyokuwa wa kulisambaza neno la Mungu, na kuitulisha penye kusambaza lugha zao, pamoja na mambo mengine kama ya maendeleo kwa mbinu zao. Nguvu ya Kiingereza inatokea sababu Kiingereza imekuwa na asili penye watu ambao awali waliichukua manani sana ukweli wa Mungu (Mangalwadi 2011). Ukweli huo unatakikana kukumbukwa pahali ambapo sera za lugha duniani zinachunguzwa. Mungu mwenyewe anapendelea watu wazitumie lugha zao badala ya za wageni (jinsi Babeli hutajwa juu), ili wawezechwe kujifahamu na kumfahamu Mungu kulingana na vile walivyo, siyo kulingana na vile wasivyo ambao hutokea wanapotumia lugha ya watu wengine. Maono ya kusema utumizi wa lugha moja duniani pote utasawazisha watu wote yameonyeshwa kuwa ubunifu usio na msingi.

Lengo la maandishi haya, sio kuwafikia waakina sherikali au wakubwa watawala. La hashu. Ninavyowalenga, ni watu binafsi popote walipo wanaojali maisha ya binadamu, na lugha utumizi. Natumai wasomi wataona upungufu kwa hali ya sasa ya kusambaza utumizi wa Kiingereza, na badala yake watajitolea kuziua na kuzitumia lugha za wenyeji wa nchi mbali mbali. Mahali ambapo nchi za magharibi zimeajibika sipo kwa kuinua Kiingereza, lakini kuinua Injili ya Yesu: Injili inayoweza kutafsiriwa kwa kila lugha duniani. Injili ya Yesu siyo dini moja kati ya dini kadhaa tu, pia ni msingi unaokamilisha dini zote duniani pote (Vattimo & Girard 2010). Uhusiano kati ya mataifa, mbinu za kuwafikia wamaskini na waliopotea, ni

kupitia wanao kuwa tayari kujitolea maishani mwao.⁴⁰ Ndivyo injili inayo-weza kuokoa, Yesu ndiye Mwokozi, na siyo Kiingereza. Kiingereza siyo lugha ya kipekee ya Mungu.

Bibliography

- Alexander, Neville, 1999. 'English Unassailable but Unattainable: the dilemma of language policy in South African Education.' Paper presented at the Biennial Conference of the International Federation for the Teaching of English (University of Warwick, England, UK, July 7-10, 1999). <http://eric.ed.gov/ERICWebPortal/recordDetail?accno=ED444151> (accessed 28.08.08).
- Alogali, Azizah, 2018 'World Englishes: changing the paradigm of linguistic diversity in global academia. Research in Social Sciences and Technology.' (RESSAT), 3(1), 54-73.
- Blommaert, Jan, 2019, *Foreword*. 1-7 in: Haque, Shazamen, and LeLièvre, Francois, (eds), 2019, *Family Language Policy: dynamics in language transmission under a migratory context*.
- Bronkema, David, 2015, 'Flying Blind? Christian NGOs and Political Economy.' 211-245 in: Cheong, John and Meleses, Eloise, 2015, *Christian Mission and Economic Systems: A Critical Survey of the Cultural and Religious Dimensions of Economies*. Pasadena: William Carey Library.
- Brutt-Griffler, Janina, 2002. *World English: a study of its development*. Bristol: Multilingual Matters.
- Chowdbury, Raqib, and Ha, Phan Le, 2014, *Desiring TESOL and international education: market abuse and exploitation*. New perspectives on language and education. 37. Bristol: Multilingual Matter.
- Comaroff, Jean and Comaroff, John L., 2004, 'Notes on Afro-modernity and the Neo World Order: an afterword.' 329-347 In: Weiss, Brad, (ed.) 2004, *Producing African Futures: ritual and reproduction in a neo liberal age*. London.Boston: Brill.
- Cusack, Carole, M., 2015, 'Vestigial States: secular space and the churches in contemporary Australia.' *George Shipp Memorial Lecture* given at the Workers Education Authority (WEA), 72 Bathurst Street, Sydney, 1st October 2015.

⁴⁰ Yohana 3:16.

- De Costa, Peter, & Park, Joseph, and Wee, Lionel, 2018, 'Linguistic Entrepreneurship as affective regime: organisations, audit culture and second/foreign language education policy.' *Language Policy*. Springer Publication online.
- Girard, René, 2010, *Battling to the End: conversation with Benoît Chantre*. (trans. By Mary Baker) East Lansing: Michigan State University Press.
- Ha, Phan Le, 2015, Chapter 12. Unequal Englishes in Imagined Intercultural Interactions. 223-243 in: Tupas, Ruanni, (ed.) 2015, *Unequal Englishes: the politics of Englishes today*. Basingstoke: Palgrave MacMillan.
- Ha, Phan Le, 2016, 'English and Identity: a reflection and implications for future research,' in: *Journal of Asian Pacific Communication* 26(2), 2016, 348-355.
- Harries, Jim. 2012, 'The Great Delusion: post-colonial language policy for mission and development in Africa reviewed.' *Transformation, an international journal of holistic mission studies* 29/1, January 2012, 44-61.
- Harries, Jim, 2015. *Secularism and Africa: in the light of the Intercultural Christ*, Eugene, Oregon: Wipf and Stock.
- Kachru, B.B., 1985, 'Standards, Codification and sociolinguistic realism: the English language in the outer circle' in Quirk, R. and H. G. Widowson (eds): *English in the World: teaching and learning the language and literatures*. Cambridge: Cambridge University Press. 11-30.
- Lakoff, George, and Johnson, Mark, 1980, *Metaphors we Live By*. London: University of Chicago Press.
- Lindbeck, George A., 2009, *The Nature of Doctrine: religion and theology in a postliberal age*. 25th Anniversary Edition. Louisville, Kentucky: Westminster John Knox Press.
- Lorente, Beatriz P., and Tupas, T. Ruanni F., 2014, '(Un)emancipatory Hybridity: selling English in an unequal world.' 66-82 in: Rubdy, Rani and Alsagoff, Lubna (Eds.) *The Global-*
- Mangalwadi, Vishal, 2011, *The Book that made your World: how the bible created the soul of western civilisation*. Nashville, Tennessee: Thomas Nelson.
- Mboya, Paul. 1978. *Richo ema kelo chira*. Nairobi: East African.
- McCormack, B.L. 1984, 'Divine Revelation and Human Imagination: must we choose between the two?' in: *Scottish Journal of Theology*, 1984, 37, 431-455.

- McKay, Sandra Lee, 2002. *Teaching English as an International Language: rethinking goals and approaches*. Oxford: Oxford University Press.
- Park, J. S. 2009, *The local construction of a global language: Ideologies of English in South Korea*. Berlin: Mouton de Gruyter.
- Sharifian, Farzad, 2015, *Cultural Linguistics*, in Sharifian, Farzad, (ed.) *The Routledge Handbook of Language and Culture*. Abingdon: Routledge, 473-492.
- Tupas, Ruanni and Rubdy, Rani, 2015, 'Introduction: from World Englishes to Unequal Englishes.' 1-15 in: Tupas, Ruanni, (ed.) 2015, *Unequal Englishes: the politics of Englishes today*. Basingstoke: Palgrave MacMillan.
- Vattimo, Gianni, and Girard, René, 2010, (edited by PierPaolo Antonello, translated by William McCuaig, *Christianity, Truth, and Weakening Faith. A Dialogue*. New York: Columbia University Press.

8. Maendeleo ya Kiroho: kulisaidia kanisa kujitegemea na kujiepuka na utegemeo wa nje usiofaa

Muhtasari:

Somo la Kwanza	Umuhimu wa uaminifu.
Somo la Pili	Wafu hulala, tu.
Somo la Tatu	Bidii isiyotokea penye Uchawi.
Somo la Nne	Sherehe.
Somo la Tano	Mijadala: juu ya sherehe.
Somo la Sita	Midaharo: asili ya hela inayofaa.
Somo la Saba	Mijadala.

Somo la kwanza – Umuhimu wa uaminifu.

Mwalimu kujieleza Maneno ya utangulizi

Somo hili litaingalia pengo inayobaki ambayo wengi hawajali, kati ya Kiingereza na Kiswahili. Pengo hii ni muhimu sana kuangaliwa, kwa ajili ya mambo mengi Tanzania siku hizi yanayoangaliwa kupitia Kiingereza, hali ambayo haizangatii utofauti unaokuwa kati ya lugha na utamaduni wa Kiingereza na wa Kiswahili.

Sana sana Kenya, tuna makanisa yaliyoanzishwa bara hii ya Afrika, ambayo hayawategemeo Wazungu kwa mali au maarifa. Uhusiano na makanisa hayo yanaweza kutusaidia kufahamu jinsi ya kuujenga msingi usiokuwa na utegemeo/tegemezi wa nje na usiofaa kwa kanisa la Afrika.

Wamisionari wazungu wengine wanahitaji kuhimizwe wafanye huduma zao kupitia lugha na utamaduni wa wale wenyeji ambao wanajaribu kuwafikia na injili.

Lengo la mwalimu pia ni kwamba ajifunze kutoka kwa wanafunzi kulingana na uzoefu wa muda mrefu walio nao wengi wao.

Mafunzo juu ya Uaminifu

Somo la Biblia: Mathayo 25:14-30 na pia Luka 19:11-27

Askofu / mfalme mtarajiwa alienda safarai. Aliwaachilia watu wake majukumu, kwa njia nyingine aliwaachilia pesa. Kumbe wengi

hawakumtarajia huyu tena arudi, na hawakumtaka. Wengine walimjali, na wakatekeleza majukumu vizuri. Wengine hawakujali. Mkubwa aliporudi, walizawadiwa kulingana na jitihada zao.

Kipimo kilikuwa uaminifu wao. Ni vile sasa, je, tutakuwa waaminifu kwa utendaji wetu kwa huduma zetu? Uaminifu kumbe una umuhimu wake!

.....

Mtu mwenye mahindi alitaka apate ng'ombe ampelekee penginepo, ili anunue naye mabati. Alikubaliana na mwenye ng'ombe, na akalipa kwa mahindi. Mwenye ng'ombe alikuwa na wazo tofauti, akamwamwuliza akiweza kukubali kitu kingine badala ya ng'ombe, achukue karatasi ambapo aliandika ahadi ya ng'ombe? Maana mwenye ng'ombe aliaminiwa, ndipo mwenzake akamkubali. Mwenye ng'ombe akaandika karatasi kama ifuatavyo:

Mimi, mwenye ng'ombe nakubali kumpe mtu ng'ombe yangu moja kwa moja akija kwangu na kunipa hiki karatasi.

Yule akaenda na hicho karatasi. Alipomfikia muuzaji wa mabati ambaye pia alimwamini mwenye ng'ombe, alikubali kukipokea karatasi na kampa mabati. Baadaye aliendelea kuitumikia karatasi yake ili avinunue vitu vingine.

Baada ya muda, mtu mwingine alimjia mwenye ng'ombe, ambaye alitaka ampe mahindi ili apewe ng'ombe kununua naye saruji. Mwenye ng'ombe, ambaye bado alikuwa na ng'ombe yake huyu, alimwambia huyu tena, badala ya kuenda na ng'ombe, kwani asiende na karatasi kama ile ya kwanza? Alikubali, akaacha mahindi yake, na akatumia karatasi aliyopewa kununua saruji. Muuzaji wa saruji pia aliweza kuendelea kuitumia karatasi kuvinunua vitu vingine.

Baada ya muda, mtu mwingine alimjia mwenye ng'ombe, ambaye alitaka ampe mahindi ili apewe ng'ombe na kununua magodoro. Mwenye ng'ombe, ambaye bado alikuwa na ng'ombe yake huyu, alimwambia huyu tena, badala ya kuenda na ng'ombe, kwani asiende na karatasi kama ile ya kwanza? Alikubali, akaacha mahindi yake, na akatumia karatasi aliyopewa kununua magodoro. Mwuzaji wa magodoro pia aliweza kuendelea kuitumia karatasi kuvinunua vitu vingine.

Baada ya muda, mtu mwingine alimjia mwenye ng'ombe, ambaye alitaka ampe mahindi ili apewe ng'ombe kununua naye maharagwe. Mwenye ng'ombe, ambaye bado alikuwa na ng'ombe yake huyu, alimwambia huyu mtu tena, badala ya kuenda na ng'ombe, kwani asiende na karatasi kama ile ya kwanza? Alikubali, akaacha mahindi yake, na akatumia karatasi aliyopewa kununua maharagwe. Mwuzaji wa maharagwe pia aliweza kuendelea kuitumia karatasi kuvinunua vitu vingine.

Kumbe, baada ya muda, mwenye ng'ombe ambaye bado alikuwa na ng'ombe yake, pia alikuwa na mahindi ya thamani ya ng'ombe nne. Watu wengine wanne waliweza kupokea vitu vyao walivyohitaji, na walifurahi kwa sababu badala ya kutembea na mahindi mazito au ngombe, waliwezeshwa upokezi wa vitu vyao kwa kuibeba tu karatasi moja. Kumbe ng'ombe moja, kwa sababu mwenye ng'ombe alikuwa mwaminifu, alizaa nguvu za ununuaji ya ng'ombe wengine wanne! Hakuna mtu ambaye hakuifurahie hali!

Jadiliana. Uaminifu unaweza kuzalisha mali mingi.

Somo la Pili – Wafu hulala

Somo la Biblia: John 11:1-44

Kwa nini watu wakalia?

Watu walimfahamu Lazarus kama mtu aliyekufa. Yesu alijua amelala tu.

Vitendo gani vya watu vilitokea kulingana na imani yao juu ya kifo cha Lazarus (ambavyo wasingevifanya kama wangalijua kumbe alilala tu)?⁴¹

Vitendo vya hawa watu, ni kama vilitokea kulingana na mashaka yao juu ya uwepo wa ufufuo.

Je, vitendo vyetu baada ya kifo cha mtu vinadhihirisha imani ipi?

Tujibadilishaje?

Somo la Tatu – Bidii isitokee penye Ushirikina

Nilipokuwa penye mji fulani ya Tanzania, niliona nyumba kadhaa ndani ya mji ambazo hazikupakwa rangi kwa siku nyingi. Kuta za nyumba hizo zilikuwa zinaonekana zimechakaa sana. Baada ya muda nikamwuliza mwenzangu sababu ya watu hawa kutokuweza kupaka rangi mpya badala ya kuziacha kwa hali hii mpaka zikiwa zimeharibike hivyo. Alinjibu: Ni uzembe wao.

⁴¹ Viliikuwa kwa mfano: kumlaumu Yesu, wasiwasi, woga, kusema Lazarus atanuka, shaka juu ya kifo cha Yesu, hasira na dharau, kukosa subira.

Baada ya kutafakari juu ya jibu lake, nilijaribu kufikiria asili ya uzembe huo ungekuwa nini? Kupitia mijadala zaidi, niligundua kumbe ni woga fulani. Aliyepaka rangi mpya wakati wenzake wasijali kufanya hivyo, anaweza kutambulika kuwa ni mwenye mali nyingi au anayejivunia. Wengine wanakuwa na wivu juu ya mtu kama huyu. Wenye wivu wana-weza hata kumloga. Kwa hiyo, kinachosababisha nyumba isipakwe rangi mpya ni woga wa watu kwa ushirikina. Maana yake, ushirikina unafanya watu wawe wazembe, wasiwe na bidii!

Swali nyeti basi ni hilo: je, wachungaji wanafaa kuwa na woga aina huo? Na tena, Wakristo kwa jumla, je, wanakuwa na woga namna huo? Wakiwa nao, tumejua basi msingi mmoja wa umaskini na ukosefu wa maendeleo. Tufanyeje basi?

Somo la Biblia: 1 Sa. 18:7-8 inaeleza juu ya wivu wa Sauli, iliyomsababisha kumfuatilia Daudi siku nyingi akiwa anataka kumwua. Haelezi wivu ni kitu njema, bali ni kitu cha upumbavu. Wema hasa siyo kujitetea na yule anayokushinda na kitu, wala kumloga mtu, ila ni „kuvumilia huzuni“ (1 Pet. 2:19). Maeneo mbali mbali ndani ya Biblia yanaeleza juu ya bidii ya watumishi wa Mungu. Daudi hakuacha kufanya ushujaa baada ya wivu wa Sauli kudhihirishwa. Sijui akiwepo mtu kibiblia ambaye tunaelezwa anakuwa mwenye woga wa ushirikina, ambaye pia ni mtumishi wa Mungu ambaye Mungu humtumie?

Somo la Nne – Sherehe

Watu wetu hupenda sherehe. Tunafanya sherehe nyingi, aina mbali mbali. Kwa mfano, tuna sherehe za arusi, mazishi, ushindi fulani (k.m mahafali), hata sherehe inayoangaliwa kuzuie balaa fulani.

Swali kuu: kwa nini watu hufanye sherehe? Majibu yanaweza kuwa ni: Kuwakusanya watu. Kuleta furaha. Kupata mafanyikio. Pongezi. Kufuata matakwa ya kitamaduni. Makubiliano. Kutengeneza mali. Kuonesha uwepo wa Mungu. Kumaliza uadui. Kuonesha uhuru wa watu. Kusahaulisha. Kujionesha. Kufanya kafara. Kuonesha nguvu. Kuwalisha watu maskini. Kutengeneza uhusiano wa kiroho. Kutoa zawadi. Kumtambua mchawi au mlogaji. Kupata marafiki.

Somo la Biblia: Yohana 2:1-11.

Kufafanua somo hili:

Mstari wa kwanza: arusi imapangwa siku ya tatu, na Yesu alifufuka siku ya tatu. Kuna uhusiano hapo?

Mstari wa pili: Kwani, walioenda ni wale walioalikwa pekee?

Mstari wa tatu: Divai ilipokwisha, ni kana kwamba furaha ikaisha pia, ni kana kwamba Mungu ameondoka kutoka kwa Watu, hali inayotangaza mwisho wa wakati wa Agano la Kale, na kuingia Agano Jipya ya Yesu.

Mstari wa nne: Kusema kwake Yesu 'saa yangu haijawadia', ni kama alionesha yale aliyoweza kufanya kwa arusi yalikuwa tu kielelezo juu ya jambo lile atakalokamilisha katika kifo na ufufuo wake.

Mstari wa tano: Wanafunzi waliambiwa 'Lo lote atakalowaambieni fanyeni', maneno yanayofaa kutajwa na kusikilizwa kwa sisi mpaka sasa!

Mstari wa sita: Yesu alijishugulisha na mabalasi ya maji aina ya kawaida tu.

Mstari ya saba: Mabalasi yakajazwa maji mpaka juu.

Mstari wa nane hadi kumi: Maji yanapeleka kwa mkuu wa meza. Alipoonja, kumbe yamegeuka kuwa divai, na tena divai ya mwisho ni tamu kushinda ile ya kwanza. Divai ya mwisho kuwa tamu kushinda ile ya kwanza kinaonesha vile furaha juu ya Yesu kwa watu wote itakavyokuwa tamu kushinda furaha iliopatikana kwa kupitia Agano la Kale.

Mstari wa kumi na moja: Hivyo Yesu akaudhihirisha utukufu wake. Kumbe utukufu wa Yesu ulidhihirishwa kwa kupitia matumizi wa kitu kile cha kawaida sana, kilichopatikana bila hata malipo! Hiyo ikawafanye wanafunzi wake wamwamini yeye.

Mambo makuu:

- 1) Kafara haielezwi, sababu kafara kilichotangazwa na sherehe kumbe kilikuwa kusulibiwa kwa Yesu.
- 2) Yesu alileta furaha mpya, baada ya furaha ya asili ile kwisha.
- 3) Yesu kumbe huleta maji ya uzima (tunasoma zaidi juu yake katika Yohana 4).
- 4) Maji ni kitu kinachopatikana bure. Kujitoa kwa Yesu kulikuwa bila malipo! Maana yake ni: upendo wa Yesu ni ya neema, na haute-gemei wema wa watu.
- 5) Utukufu wa Yesu ulidhihirika kupitia kujitolea (kuyatolea maji), kile kilicho zawadi isiolipwa.
- 6) Sababu gani maalum vitendo vile viliwafanye wanafunzi wamwamini Yesu?

Mijadala

Ibada zetu za Kanisa, je ni sherehe, na zawadi ya bure inayotolewa hapo anapokuwepo Yesu, Mwana wa Mungu?

Kumtii Yesu siku hizi ni kufanya nini?

Inafaa tumwamini kiviipi Yesu siku hizi?

Sherehe inabadilisha hali ya watu, kwa mfano sherehe ya arusi inawafanya bibi na bwana arusi kuwa mume na mke wakati walipokuwa msichana na mvulana tu kabla ya sherehe.

Mambo makuu

- 1) Sherehe zetu siku hizi hazihitaji kafara, kwani Yesu ndiye kafara kuu wetu.
- 2) Sherehe ya kitamaduni inahusika wafu na inahusika maisha ya watu. Ni vipi sherehe zetu zinahitaji zikadilike kwenye kiini chake akiwepo Mungu badala ya wafu (mizimu)?

Somo la Tano – Mijadala: juu ya sherehe

Jadiliana juu ya sherehe na hali yake.

Somo la Sita – Debate: asili ya hela inayofaa.

Inafaa kanisa lipate hela yake kutoka wapi:

- 1) Mradi wa kanisa.
- 2) Fungu la kumi ya washirika.
- 3) Wageni.

Makundi matatu yatengenezwe. Kila kundi lijiandae kutetea moja ya haya mambo tatu hapo juu. Kila kundi lipewe dakika kadhaa kueleza utetezi wake. Muda unaobaki ni kujadili njia bora ni ipi ya Kanisa kuipokea mapato yake.

Somo la Saba – Mijadala.

Wanafunzi waambiwe kila mmoja andae na aandike maswali matatu au mawili juu ya mada hii – jinsi ya kujiendeleza kiroho ili kanisa lisaidiwe kujitegemea. Jadiliana juu ya hayo maswali ndani ya kundi lako kisha wote kwa pamoja.

9. Masuhulisho ya hali za kulaumiana na kushitakiwa wachawi bara la Afrika⁴²

“Ukristo haukubaliane na dini zinazo unganisha watu ili waandae pamoja kumwua au kumfukuza mlaumiwa, jinsi dini zote zimekuwa zikifanya tangu jadi, ila dini hizo zinazofuata Biblia,” (Kaplan 2016).

I. Utangulizi

Uoga juu ya kazi za wachawi, hali ya kulaumiana, na tamaa ya vitu vya wenzetu, ni mambo yanayo tambulika kuwepo sana bara la Afrika. Wengine husema WaAfrika huogopa uchawi sababu hawana akili timamu. Wasomi wengine wamegundua kabila wote duniani pote walifungwa na huo ufahamu ambao siku hizi kwa wengine unatambulika kuwa wa udanganyifu. Wengine waliweza kujiepuka nayo, lakini jinsi walijiepusha limesahaulika.

Kumbe, ni Ukristo unaotupa uwezekano wa kujiepuka na udanganyifu unaotuvuta ili tulaumiane na shitakiane kama wachawi. Ukristo kumbe sio dini moja kati ya dini kadhaa sawa na zingine. Mbali, Ukristo ni ufunuo wa Mungu unaotupa njia ya kipekee ya kujiepuka na hali za uoga juu ya uchawi. Naamini waumini wengi wa makanisa mbali mbali bara ya Afrika wanafahamu hiyo. Lakini sababu elimu ya kisasa haitambui hiyo na wenzetu wengi huikimbilie elimu, ni jambo lisilodhihirika rasmi. Kusema njia ni Yesu, ni kuwakwaza waundaji wa elimu wa kisasa, inayosambazwa bara la Afrika, ambao wameamini sana uweza wa *usekula* au *umodeni*.⁴³ Inahitaji mtu mwenye ujasiri kuwatangazia watu wa dunia kama hawa juu ya ukweli wa Mungu ambao hawataki kuusikia. Inahitaji mtu mwenye hekima sana kugundua badala ya kupuuza jinsi Injili ya Yesu ni, kwa wanaomwamini, uepukiko kutoka kwa mikono ya Shetani.

Wasomi wanaoamini Ukristo ni dini moja tu kati ya na sawa na dini nyingi duniani wamekosa! Tukitaka kuuita Ukristo dini, basi tufahamu dini ni mojata duniani pote. Ikiwa dini ni nyingi, ni kosa kuuita Ukristo dini.

⁴² Kwa wanaopenda kugundua uhusiano wa maandish haya na Kiingereza, nimetafsiri *religion* na dini, *victim* na mlaumiwa, *modern* na modeni, *secular* na sekula, *scapegoat* na uchawi, *anthropologist* na mwanaanthropologia. Kwa mswada huu wa Kiswahili, sijayataja majina ya wasomi husika ambao nimetoa maono mengi kwao ila kwa bibliografia.

⁴³ Angalia futnoti namba 1.

Ufahamu huo unaosema Ukristo ni dini moja tu sawa na zingine ni upotofu unaoendelea mpaka sasa kuficha na kufanya isiyo halali usomi ufaaa (Masuzawa 2005, Jindra 2014:316).

2. Kifo na Maafa, lazima isababishwe na mtu fulani

WaAfrika wengi hujishugulisha sana na ubunifu wa mwuaji au yule aliyesababisha maafa. Kufanya hivyo inakuwa mbinu ya usuluhishaji wa matatizo yanayodhaniwa yanaletwa na watu. Mchawi akigunduliwa, pengine watamwua moja kwa moja. Akigunduliwa mtu anayekuwa kinyume cha jamii, wanaweza kumfanyia maisha yake iwe fupi, na vibaya. Mara nyingi WaAfrika wanashangaa; ni vipi Wazungu wamejiepuka na kufanya hivyo! Wanashangaa vile Wazungu wameweza kujiepuka kutoka kwa usumbufu unaowasumbua sana WaAfrika wenzao. Mara Wazungu wanafikiria WaAfrika wamerukwa na akili; kwanini kupenda kutiririsha damu ya mwenzao juu ya muuaji mara kwa mara, na hujamwona akiua! Hapa sasa tunataka tuanze uchunguzi kwa kulinganisha wachawi wanaouawa bara la Afrika, na jinsi mbuzi walichinjwa na kufukuzwa katika kitabu cha Walawi kwa Agano la Kale (sura 16).

Tamaa, kumbe, inakuwa na sehemu tatu. Hiyo imewashinda Wazungu kufahamu kwa ndani kwa miaka mingi! Sisi binadamu hutamani vitu, lakini kila mara vitu tunavyotamani ni vya mtu mwingine! (Vitu ambavyo watu wengine hawanavyo hatuwezi kuvitamani sana.) Halafu, vitu vinavyo tamaniwa vikiwa haba, tunagongana tukishindana. Kushindana hivi kunachotokea, suluhu lazima itafutwe. Kawaida, tunamtafuta yule ambaye tutaweza kumlaumu. Halafu anauwawa, au anakufukuzwa kutoka kwetu. Jinsi kuuzuie ukatili huo kumewashinda binadamu kwa miaka mingi sana. Kuuzuie ni ngumu! Ni Ukristo peke yake unao kuwa na uwezo wa kuleta ukombozi kutoka kwa marudio rudio ya uuaji na ukatili. Unafanya hivyo ukiwa unadhahirisha jinsi uaji aina huo, au kumfukuza mtu, unaofanywa kama ulipizaji kisasi, ni bure. Ni kama sisi binadamu tunapona kitu kibaya kinatokea tunadanganywa na mioyo yetu ili tumtafute haraka mlaumiaji!

Raia wa nchi za Magharibi wanadhani wameachana na mambo hayo ya juu: wanajiamini wanaitambua hali ya kumshitaki mtu mwingine kujifaidisha na watu wako kuwa udanganyifu (Kaplan 2016). Hiyo inakuja na hali inayoitwa *modeni*.

Neno la *modeni* linachacha: *Modeni* linaweza maanishatu 'wakati huu'. Pia linaweza ashiria falsafa fulani inayoleta aina ya maisha ambayo watu huishi, maisha tofauti na ile ya zamani. *Modeni* inaweza tafsiriwa kwa Kiswahili kama *kisasa*, au maisha kulingana na falsafa fulani! Ndivyo shida ya ukalimani inaingia. WaAfrika wakidhani wanaishi *modeni* sababu wakati

huu ndio wa sasa, wakifikiri wamefika kiwangu cha maisha ya *modeni* ya raia wa Ulaya, yaani Wazungu, wanajidanganya. Modeni kweli ni wa kisasa, lakini siyo kisasa cha kiAfrika! Ni maisha ya kisasa cha Wazungu chenye falsafa fulani.⁴⁴

Ikiwa ni vile nimeandika juu, na WaAfrika hawana *modeni* (sio *modeni*), lakini kuwa *modeni* kungekuwa msaada kwao, swali linakuja: watapataje kuwa *modeni*? Wengi husema elimu ndiyo inaleta mtu kuwa *modeni*. Lakini hapa siwezi kubaliane nao. Elimu inasaidia *wamodeni* wajiendeleze, sawa. Lakini elimu haiunde *modeni* yenyewe. Inadhania wanaoelimishwa kuwa tayari *modeni*! Wasipokuwa *modeni* tayari, elimu hiyo itawezakuwapitia tu juu ya vichwa vyao hewani bila kuwagusa kwa ndani.

Hata wanatheologia Wazungu hudhania uwepo wa *modeni*. Kwa hivyo, wanafahamu Biblia kupitia hiyo *modeni*, ambayo WaAfrika hawana. *Modeni* inamaanisha (lakini hiyo haitaeleweka na WaAfrika sababu kata asili yake hawana) kitu ndicho msingi wa maisha, na cho chote kisichowekwa msingi wa kitu kinakuwa kisihesabiwe cha uhakika. Yaani – theologia ya nchi za magharibi haiwezi kuwa na maana halisi kwa WaAfrika sababu imejengwa juu ya msingi wa *kitu*. Angalia Kaplan (2016).

Binadamu *modeni*, ambaye siye Mwafrika, anatofautisha vitu viwili, yaani vitu vilivyomo (*kitu*) vinahesabika tofauti na vitu visivyomo. Wengi wao wanaona Mungu anakuwa katika kundi hili la visivyomo. Vitu vilivyomo vinaendelea kuwepo na kuwa na uhusiano kama mashini, kwa mfano mashini inayosukuma piki piki. Mambo hayo, ya kugawa vitu vyote ambavyo viko duniani kwa kundi viwili, vilivyomo na visivyomo, ni msingi wa ufahamu wa Wazungu (Harries 2015b:ix, xiii, 15).

Ugunduzi wa juu ndio umewasaidia Wazungu kuunda teknolojia na kuchukua hatua mbali mbali za maendeleo. Ugunduzi huo umewasaidia waweke ushirikina kando. Kuweza kuweka ushirikina kando kimewasaidia kugundua vile mambo yanavyoendelea bila kuwahusisha watu wenzao. Nilipokuwa bado mdogo nilidhani watu wote duniani pote ndivyo wanawaza hivyo kama Wazungu. Lakini kumbe sivyo. Ugunduzi wa utofauti wa ufahamu wa WaAfrika ulinishitua sana. Elimu yangu hakuni-saidia kugundua hayo, sababu yote ilijengwa juu ya msingi wa *kitu*. Kumbe, elimu yangu niliyopewa Uingereza ilikuwa ikanidanganya! Elimu rasmi iliyopo karibu popote duniani bado ina shida iyo hiyo. Maana yake, badala ya kumsaidia mtu awe na hali ya *modeni*, elimu inayotolewa rasmi na

⁴⁴ Tukisema ni maisha ya kisasa pia ya WaAfrika, sawa, lakini ikiwa hivyo, hatutaweza tena kusema ina hali ambayo WaAfrika hawanayo. Hii ni sababu, kulingana na maandishi yangu haya, ninasema WaAfrika hawana *modeni*, na siyo *wamodeni*.

shirikali zetu na muungano wa watu rasmi, inamdhaniana mwanafunzi ameshakuwa navyo! Asili ya ufahamu huo wa *modeni* ni kama ni siri kuu! Hii inamaanisha elimu haimsaidii sana mtu asiye MwUlaya. Hapo ndipo shida.

Nje ya *modeni*, watu huendeleo kuishi kulingana na kulaumiana. Yaani, wanafahamu kosa au haba ya riziki, afia, nk, lazima isababishwe na mtu au watu fulani, na haiwezi tokea pasipo hayo. Hata wanaomwamini Mungu ni kulingana na hayo. Kwa mfano, msaada wa Mungu hutokea juu ya uwezo wake wa kutusaidia kugundua asili ya shida ni mtu gani. Halafu Mungu anawezakutuambia jinsi ya kuwa washindi juu ya shida aina hiyo. (Walio na *modeni* wanaweza pia kulaumiana, lakini siyo kwa kile kiwango cha wasio *modeni*.) Hali hiyo ya kulaumiana, utamu wake unapatikana mlaumiwa akigunduliwa na kuchukuliwa hatua. Mlaumiwa akifa, kwa mfano, watu hujisikia amani, utumaini, wema, na utulivu, wakitarajia sasa kuendelea kufanyikiwa.⁴⁵ Ubaya wa mbinu huu wa kupokea amani, ni kwa mlaumiwa anayeangamizwa! Yaani, kila mara amani huja kupitia kuangamizwa kwa mtu au watu fulani. Mbinu huu unahitajika kila wakati kumtafuta na kumwangamiza mtu. Mara nyingi, kwa hakika, yule mshitakiwa, hana hatia. Swali letu sasa ni – ni vipi *wamodeni* waliweza kuepuka mbinu huo na kuanza kuutafuta msingi wa matatizo yao penginepo, pasipo mtu mlaumiwa? Jibu la lile swali la juu linaweza kuwakwaza *wamodeni*, na *wasekula*.

Pasipo kuwazuia, watu wanaweza kuuana kabisa. Dini za jadi ndizo zinapambana na hali hiyo. Na *wamodeni* wamekuwa wanaamini dini za jadi ni vitu bure tu (Kaplan 2016)! Dini za jadi zinasaidia ili watu wasiangamizane na kuuana waishie kabisa! (Kaplan 2016). Dini za jadi zinakuwa mwitikio kwa udanganyifu huo unaosema kila shida inayo msababishaji, ili kupambana na matokea yake. Yaani, mtu akiamini shida lake limesababishwa na mtu fulani, pasipo msaada, anaweza aende kumwangamiza moja kwa moja. Lakini, akiwepo mganga anayeheshimiwa, mganga huyu atamshauri atumie mbinu nyingine kumwangamiza yule anayehesabiwa muovu. Kwa mfano anaweza sema, atumie dawa kumwua, amchinje mnyama fulani, ataje maneno fulani, au amwachilie mganga mwenyewe ammalize huyu mtu baada ya kumpa malipo yake. Ndivyo mganga, na dini za jadi kwa jumla, zimeweza kuokoa maisha ya watu wengi. Gharama ya uokozhi huo imekuwepo: Gharama ni, hata watu wasipouana kamili, wanasisitizwa imani ya watu ya kusema fulani kumbe ni kweli anayo hatia. Kwa hivyo, mganga na dini zake za jadi, wanadumisha hali ya watu kutoaminiana au kutumainiana. Dini hizi zinafanya watu

⁴⁵ <https://www.standardmedia.co.ke/kenya# 21st February 2019, vile nimetaja juu.>

washuke sana, lakini badala ya kumchinja mwenzao 'kimwili', wanaenda kufanya hivyo wakitumia dawa.

Kuchukua hatua ya pili, na kutoshitakiana, bado ni ngumu. Wengi wanaamini ni imani kwa Kristo peke yake inayoweza kuangaza nuru kwa mambo hayo, kuonyesha msingi huo wa kusema kuuawa kwa mlaumiwa kutanipa amani, ni udanganyifu na uongo tupu (Girard 2001:2). Hii ni sababu Biblia imepangwa kinyume cha hadithi nyingine zote duniani! Badala ya kufanya vile mganga anavyofanya na kusema mtu fulani anakusababishia shida yako lakini usimvamie na shoka, *inaeleza jinsi mdhaniwa hatia hana hatia*. Sio hiyo tu; pia inasimama na mdhaniwa na mara nyingi ndiye mtu anayebarikiwa na Mungu. Yule ambaye kulingana na imani ya jadi ni msababishaji wa shida, Biblia inamfahamu mdhaminiwa na Mungu. Kwa maneno mengine – Mungu anampenda kwa njia ya kipekee yule anayeshitakiwa kuwa mchawi! (Girard 2010).

Lakini, Wazungu *wamodeni* hawayafurahie mafunzo kama hayo! Wame-shaamua mambo ya dini ni msaada bure kwa watu, na ni mbinu tu wa makuhani kujitajirika! (Nongbri 2013). Siku hizi wengi huchukiza Ukristo sababu WaKristo wanasema ni Mungu anayewafanyikisha binadamu. Watu *modeni* wanataka kuamini wanajifanyikisha wenyewe. Kwa hivyo ni Ukristo wenyewe unaolaumiwa juu ya matatizo yanayopatikana kati ya watu (Dreher 2019). Wasomi hawafurahi kuyasikia hayo (Dreher 2019). Yesu alishitakiwa kama mchawi, halafu alisulubishwa, lakini Biblia inatuambia hakuwa na lawama, na ndiye Mungu mwenyewe! Ndivyo Biblia inadhihirisha jinsi maelezo hayo yanayosema mtu auawe ili tubaki tuwe na amani, ni uongo. Kwa hivyo, maendeleo yanayopatikana wakati huu yanatokea penye msingi moja tu, ile ya Injili ya Yesu!

Naweza ongea juu yangu binafsi. Kabla sijaja Afrika mara ya kwanza (1988), nilikuwa nikadanganywa na udanganyifu huo wa *umodeni*. Nilikuwa Mkristo, sawa. Lakini, kusema ukweli, mambo mengi juu ya uhusiano kati ya imani yangu na kazi zangu za umisionari sikuwa nikaona. Nilikuwa nafikiria ujuzi wangu wa Ukulimo niliojifunza UK utakuwa msingi wa huduma wangu kuwasaidia WaAfrika.⁴⁶ Haikutumia muda mpaka mishituko ilianza kunijia. WaAfrika wenzangu hawakuwa wanafanya sawa na matarajio yangu kulinga na mazoea yangu, ya kutafakari mambo yote juu ya msingi wa imani juu ya uhakika ya uwepo wa kitu (jinsi *wamodeni* wafanyavyo). Badala yake wenzangu walikuwa wakawaza sana juu ya uchawi. Wakati ule sikuwa na ufahamu wa ndani vile ninavyo wakati huu, lakini niligundua ndivyo imani ya Ukristo iliyowawezesha watu wangu (Wazungu) kuwa vile walivyo. Ndivyo nilikuwa niligundua, ufunguo

⁴⁶ Nilikamilisha shahada ya kwanza katika Ukulimo 1987.

unaoweza kuwasaidia WaAfrika wapate maendeleo haukuwa siensi wala teknolojia, ila Injili ya Yesu! Kwa hivyo, niliachana na kufunza ukulimo, nilijiingiza kwa kufunza Biblia. Sasa nazidi kuona zaidi na zaidi jinsi ndivyo ni imani kwa Biblia inyowawezesha watu kujiepuka na marudio tena na tena na uchawi, na kuwashitaki wachawi.

Sikuweza kuyafanya mabadiliko hayo juu kwa urahisi. Yaani, ufahamu huo niliopata kulingana na jinsi nilivyolelewa Uingereza haukufa moja kwa moja. Hata nilipojihesabu mwamini wa Kristo, bado niliona afadali kuuamini uhakika wa siensi badala ya 'udanganyifu' wa Biblia. Lakini, pole pole niligundua; ndio Biblia inayoweza kuwatoa watu penye imani potofu wa kuwashitaki watu wasio na hatia (Harries 2015b:102-135)! Tangu hapo niligeuka ili nifunze Biblia (angalia Harries 2018c).

3. Mpaka Utubu

Kwa binadamu, kujitoa penye hali ya kushitakiana wachawi ili kujisuluhisha shida zako, kumbe ni kitu kinacho hitaji toba (Cowdell 2013). Wanafunzi wa Yesu ambao wakati ule walikuwa wamesambaratishwa baada ya kufufuka na kupaa kwake Yesu, hawakuwa na nguvu ila ya Roho wa Mungu. Lakini walikuwa wanajua, kwa mfano angalia jinsi Petro alimsaliti Mungu, wenyewe walihusika katika njama hiyo ya kumwua Yesu. Lakini, ilikuwa kupitia Roho ndivyo walipewa imani hiyo iliyoweza kuvunja imani juu ya nguvu za wachawi (Dreher 2019). Binadamu vile alivyo kumbe hawezi kujisaidia. Anashindwa kujiepuka kutoka kwa udanganyifu. Hawezi kujiepuka pasipo Mungu kuongea naye (Kaplan 2016), na kukubaliana na Mungu kunahitaji kutubu.

Wazungu walipoanza kuzungukia dunia mzima na kufanya utafiti wao juu ya maisha ya watu wengine, walishangaa kugundua watu walitumia hadithi nyingi mbali mbali kuwa misingi ya maisha yao. Jinsi hadithi hiyo ilitajwa mara kwa mara, ni kama ilikuwa na umuhimu maishani mwao. Halafu wakaona hadithi hizo zilifanana na hizo za Biblia. Kwa hivyo walidhania kumbe Ukristo hauna kitu kutuambia tofauti na hadithi zingine. Kosa lau kumbe lilikuwa kutoangalia vizuri, na kutogundua hali ya kipekee kabisa ya maelezo ya Biblia! Utafiti wa ndani uliofanywa baadaye ulidhihirisha kumbe kwa hali fulani hadithi za Kristo zilikuwa na ya upekee! Upekee wa Biblia inalingana na jinsi katika maelezo ya Biblia, yule ambaye kwa watu wengine angekuwa mlaumiwa anayefaa kuawa au angamizwa anahesabiwa mtu wa Mungu! Maelezo katika Biblia kumbe ni mbali sana na maelezo ya hadithi zingine (Gerard 2001)! Kilele cha hayo yote, ni kifo cha Yesu. Sababu Yesu mwenyewe aliyeshitakiwa kuwa mchawi na hakuwa na kosa lolote, kifo cha Yesu kinamnyima mganga

nguvu. Tena Yesu ni Mungu! (Cowdell 2013). Ukristo uliweka wazi fumbo ambayo anategemea mganga (Harrison 2018:5). Matokeo moja ya hayo, Ukristo umeleta maendeleo ya elimu ambayo kabla ya kuja kwake Yesu hayangeweza hata kufikiriwa (Girard 2010). Ukristo unatusongesha kwa Mungu kiwango kinachohitajika (Girard 2010). Kumbe Mungu alimtuma Yesu atusaidie tusingamizane mpaka tumalizane kabisa, na pia tusishitakiane mbali tupendane! (Girard 2010).

Mangalwadi, aliyezaliwa na kulelewa India, anatumieze mfano sawa na ule wa juu. Vitabu vitakatifu vya India vilieleza juu ya uajabu na uzuri wa viongozi wao wa awali. Lakini kinyume nao, Biblia inaeleza juu ya uovu wa viongozi wa Wayahudi. Mangalwadi akajiuliza, ilikuwa kwa nini? Aligundua kumbe Mungu wa Biblia anasimama panda ya yule anayelaumiwa, yaani hutetee yule aliyeshitakiwa mchawi!

Ukristo kumbe siyo dini moja katika ya dini mengi ambayo ni sawa na zingine! Ukristo unapenya mioyo na kutoa uongo (Vattimo and Girard 2010). Wazungu wengine kuutupa Ukristo huo uliowalea umekuwa upuzi kubwa (Harries 2016). Kuwachukua wakina Waislamu, WaHindi, WaSikh na 'dini' zingine sawa na Ukristo ni, kwa panda za nchi za Ukristo tangu zamani kama Uingereza na Amerikani, kufikiria juu ya hizo 'dini' zingine kama wakiwa aina Wakristo! (Harries 2016). Kwa nchi za Ulaya, kuufunika Ukristo umekuwa udanganyifu wa kiajabu (Masuzawa 2005:313).

Jambo moja kufikiria kidogo kabla hatujaenda mbele, ni jinsi ufahamu juu ya Mungu ule unaotokea kwa Wazungu unakuwa. Kumbe ufahamu wa Wazungu umelingana na kitamaduni chao, na mambo mengi ambao Wazungu hufunza juu ya Mungu yanawezakosa uhusiano wa karibu moja kwa moja na muktadha wa Afrika. Yaani, Mungu wa Afrika ni yule anayeleleta baraka kupitia mbinu za kuwaangamiza wasiofaa, lakini Mungu wa Wazungu anapenda 'wasiofaa' kushinda wale ambao KiAfrika wangehesabiwa wafaa! Hio ndiyo sababu siku hizi uchunguzi wingi wa wasomi wengi kwa mambo ya Mungu kwa bara la Afrika, ukiwa unafanywa kupitia lugha ya Kiingereza, unakosa udhabiti. Lakini sababu ya utawala wa Kiingereza, uchunguzi wa ndani katika jinsi Mungu hufahamika na WaAfrika siku hizi haufanywi. Ufahamu wa Mungu wa WaAfrika na ufahamu wa Mungu wa Wazungu (yaani *God*) unadhaniwa tu ni kitu kimoja, au isipokuwa kitu kimoja ni sababu WaAfrika bado wako nyuma.

4. Upekee wa Injili

Elimu ya sherikali ya nchi nyingi siku hizi hueleza mambo mengi, lakini ukiangalia kwa makini, nje ya elimu ya dini, yote inatokea penye shina moja. Yaani, yote inadhani dini ni nyingi, na sababu dini ni nyingi, tunafaa

tuzi sahu zote. Elimu inajengeka juu ya msingi wa kutokuwepo kwa cho chote ila 'kitu' (jinsi tumeshajadiliana juu). Ukristo, uliofanya Wazungu wawe vile siku hizi walivyo, unasahaulika tu (Trenery 2014:315)! (Ni ngumu kufahamu upungufu wa uangalifu wa Ukristo, uliyekuwa msingi wa maisha wa wale waliogundua mambo ambayo siku hizi tunaita *modeni* (Cummins 2016).) Msimamo huo unachukua kila dini kama mambo ya binafsi ambayo haina maana katika jamii. Mambo hayo ni ngumu sana kwa WaAfrika: Maisha ya WaAfrika inaonekana kwa Wazungu kuwa ni dini. Kwa hivyo, hekima yote ya KiAfrika ni rahisi sana ihesabiwe kwao ni bure!

Siku hizi, katika sehemu kadhaa ya viongozi wa juu wa dunia, mtu anayesema imani kwa Kristo lazima iwe msingi wa maisha, anachukuliwa kama mpungufu au mwendawazimu asiye na cha kusema! Hata ikiwa kile anachotaja kinaeleza msingi wa ushindi juu ya uchawi, bado ni hivyo! Wasomi wajuu waliopo kwa jumla hawataki sifa lolote kwa dini yoyote! Hawataki Mungu ahesabiwe kuwa na maana yo yote. Hii inafanya wasomi kuwa wauongo. Sababu wanakataa kutambua msingi wenyewe uliowafanya wenyewe wale vilivyo, wanaweza fananishwa na watu wanaofunga macho yao kwa hiari, au kujichimbia shimu ufahamu wao.

Miaka ya nyuma haikuwa hivyo. Rudi nyuma miaka kama 150, na wasomi wakuheshimika wengi walikuwa wanafafanua upekee wa uzuri wa Ukristo na jinsi Ukristo ndio msingi wa mazuri mengi sana wa maisha ya binadamu (Masuzawa 2005:103-104). Usomi huo bado ulikuwa unasimama, ila wasomi wa Ulaya waliona aibu kutambua dini kuwa msingi wa wema wao. Walitaka wasifike wenyewe. Kwa njia nyingine, ilikuwa kupitia unyenyekevu, kuwapa dini zingine za dunia, zilizokuwa wakati huo zikaundwa, nafasi ya kushindana na Ukristo. Wakati huu, dini zingine duniani zilizoahirika na Ukristo zinazidi kuitumia uadhirisho huo kujitetea (Thatamanil 2015:61).⁴⁷

Wanaozidi kudanganywa wana zidi pia kupinga Ukristo; wanasema Ukristo hauna nafasi katika usomi wa kisasa.⁴⁸ Hata tukiwa tunafahamu jinsi inabidi wasomi waseme kulingana na sherikali zao, jinsi Ukristo siku hizi hudhoofishwa nao imezidi kupita kiasi! Kwa sababu iliyotajwa juu, nchi zenyewe zenye asili ya Ukristo kamili kama za Ulaya wanajaribu kusahau jinsi walipofikishwa mahali walipo na imani ya mababu yao kwa Ukristo.

⁴⁷ Hisia za watu ninaotaja kwa fungu la maneno haya ni vile ninavyo dhania ilikuwa wakatu huo.

⁴⁸ <https://www.cbc.ca/radio/ideas/the-scapegoat-the-ideas-of-ren%C3%A9-girard-part-1-1.3474195> Anayepingwa hapa hasa ni msomi René Girard, aliyetetea jinsi Ukristo ni mbinu ya kipekee kushinda uchawi.

Msimamo huo unaokosa kuiheshimu Injili ya Yesu umetengenezwa juu ya msingi wa uongo na unaonekana yanaweza kutuletea balaa siku zijazo.

5. Kazi ya Dini

Kulingana na Kaplan, duniani pote kaburi ni msingi wa mila ya watu (2016:35). Yaani, ni kifo ndicho kilianza kuunganisha watu tangu zamani. Aina amani inayopatikana mtu akifa, ambaye tunadhania kifo chake kinasaidia kutusuluhishia matatizo zetu, ni aina amani ya jadi. Hali hiyo ya kumshuku mtu mwingine kuwa asili ya tatizo lako inafanya watu watafute msaada. Yaani, tangu jadi, dini imehitajika. Dini ni sehemu ya kawaida na lazima kwa maisha ya binadamu. Dini haijapitwa na wakati, jinsi wengi *wamodeni* wanapenda kuamini. Dini ni lazima sababu watu hulaumiana na kushitakiana wachawi. Dini ni njia ya kuutambua uchungu wao, na kuwahusisha watu na suluhisho usio kuu kabisa (Vattimo and Girard 2010). Kwa hivyo dini ni mbinu ya kuzuie watu wasiuane wamalizike kabisa (Girard, aliyetajwa na Kaplan (2008:10)). Imani katika Kristo, ya kusema Mungu alikubali kutufia msalabani, ni mbinu ya kipekee ya kupunguza ukatili kati ya watu (Girard 2011).

WaAfrika mara kwa mara hushangaa sababu gani WaUlaya hawashitakiane kuwa wachawi.⁴⁹ Kulingana na zoezi langu, WaUlaya wenyewe hawajui msingi wa mazoea yao hayo. Wanajua tu uchawi haupo. Wanajua katika jamii yao, hakuna kurogana. WaUlaya wenyewe hawajui jinsi ya kueleza sababu ya kutokuwa na uchawi.

Yesu alisema; “jiwe waliokataa waashi ... limekuwa jiwe kuu la pembeni” (Zaburi 118:22, Mathayo 21:42). Ninavyo fahamu, jiwe hilo ndilo Yesu, na Ukristo unadhihirisha upungufu wenye dini za jadi (Harrison 2018). Kosa la dini za jadi, na hasa kila dini isipokuwa Ukristo (na kwa kiasi Uyahudi) ni kukubaliana na wazo la kusema mlaumiwa anakuwa anasababisha kila kosa linalotokea. Ukristo umejiepuka na hiyo kupitia kumfanyia Yesu mwenyewe, ambaye ni Mungu na hajafanya dhambi, kushitakiwa mchawi na kuhukumiwa kifo kwa ajili ya binadamu. Imani ya Kristo inawawezesha binadamu kujiepuka na hali ya mambo kuharibika mara kwa mara, watu kupigana na kuuana, ambayo imewasumbua watu tangu jadi (Kaplan 2016), sababu ya hali ya kulaumiana inayokuwa mioyoni mwa watu. Ndivyo utofauti kati ya imani ya dunia na hiyo ambayo Yesu alileta (Johana 8:36, Yohana 14:27 angalia Girard (2001:186)): Ya dunia, inatokea baada ya mhusika anayedhaniwa ameleta balaa kuuawa. Ya Yesu inapitia kujua kifo cha Yesu kimetosha, na uaji wa wachawi hauhitajiki tena.

⁴⁹ Kulingana na mazoea yangu.

Sasa tunaweza kuufahamu Ukristo katika njia mbili:

Moja. Uislamu, Uhindi, dini za jadi za KiAfrika nk. ni dini, lakini Ukristo siyo dini. Ndivyo wengine hufahamu (Vattimo and Girard 2010, ambao tayari nimewataja juu).

Pili. Ukristo ni dini, lakini aina za maisha za watu wengine ambayo siku hizi zimekuwa zimeitwa 'dini', siyo dini. Kulingana na njia hii ya pili, dini ni mojata, ni Ukristo.

Mimi naona njia ya pili ndiyo inafaa. Hii ni sababu kwa wasomi wanaotumia Kiingereza, watu wanaotaja dini ni wale wanaofahamu Ukristo. Yaani, mizizi ya ufahamu wao (wasomi kuu wa dunia wa wakati huu) umewekwa kwanza kupitia Ukristo, na kila aina ya 'dini' nyingine inalinganishwa na Ukristo huo, vile nimeshataja juu (Thatamanil 2015:61.)

Hata kuhani mkuu anasema, na maneno yake yamehifadhiwa katika Biblia; ni bora mmoja afe kwa ajili ya wengi (Yohana 11:50). Kwa hivyo, Wayahudi, hasa kuhani kuu mkubwa wao, hawakuwa waliona mwanga juu ya hilo jambo. Kutofahamu kwao ndivyo sababu kwa Injili ya Yohana mara kwa mara Wayahudi hushitakiwa kupitia maneno kali! Ndivyo Wayahudi walilaumiwa juu ya kifo cha Yesu (Kaplan 2016). Lakini hii haimaanishi WaYahudi wanakuwa na ujinga kubwa kushinda watu wengine. La hash! Ni vile tu ndio walikuwa watu wa Mungu, walitarajiwa kuwa tofauti. Watu wa mataifa, na hata wanafunzi wa Yesu, hawakuweza kugundua mpango wa Mungu wakati huo ulikuwa kumfufua Yesu ili alete amani mpya duniani. Ufufuo huo unatuwezesha kurudia jinsi tunafahamu dini na mila za watu wote duniani (Kaplan 2016): wote wasioamini ufufuo wa Yesu wana upungufu.

Kugundua jinsi Biblia inabadilisha mambo, lazima tutangulie kuitambua hali yetu yenyewe ya kuwalaumu wachawi (Kaplan 2016). Ni ngumu kwa mtu anayeendelea kushitaki wachawi akiona anavyofanya ni ya haki, kugundua maajabu ambayo Yesu alitufanyia.

6. Tamaa

Kutoka 20:17 inatuambia, tusitamani vitu vya wenzetu. Tufikirie juu ya tamaa. Kumbe, hali ya tamaa ya mtu ni muhimu. Binadamu hutamani vitu, lakini vipi? Kumbe, mtu anakitamani kile anacho mtu mwingine. Mtu anakitamani kile ambacho mwingine pia anakitamani. Kwa mfano, mzee anaweza fika hali ya kutomtamani tena mkewe. Anamzoea, tuseme. Lakini itakuwaje akigundua mwanaume mwenzake anamtamani sana mkewe. Sio ni rahisi yeye sasa aanze tena kuona dhamani yake? (Girard 2001). Kumbe kitu hakitaminiki mpaka mtu mwingine anayekitamani! Kwa hivyo msingi wa tamaa siyo tu kitu, lakini pia yule mtu (au wale watu) wanaotamani kile

kitu. Kitu kisichotaminika na watu wengine, hata mimi sitakitamani! Utambuzi huo juu ya tamaa ni wa msingi, na ni wa kuvuruga! Unakuwa kuvuruga sababu kwa hakika wafalsafa wengi hufanya utafiti wao kinyume wake, bila kuugundua (Alison 1996): siyo kitu tunatamani, lakini tunatamani hali ya yule mtu anacho kitu hicho, tunatamani kufanana naye, kumbe tamaa ni uigizaji, kutamani ni kuiga.

Hali ya tamaa kuwa juu ya kitu cha mtu, inafanya iwe ngumu kutofautisha tamaa na wivu.

Wivu ni upi? Wivu ni kukitamani kitu cha mtu, kwa kiwango cha kupendezwa yule mtu akidhoofika. Wanaoishi kulingana na jadi zao, huogopa sana wivu (Harrison 2018:3). Mimi binafsi nilishagundua jinsi wivu ndio nguvu unaofanya watu waogope uchawi (Harries 2012a). Ni kweli, wengi watu wetu WaAfrika huishi wakiwa wanaogopa wivu sana. Watu hujaribu kutouamusha wivu wa wenzao, kwa nini? Ili wasirogwe. Mbinu nyingi zinatamika kuhepa wivu! Maongezi ya watu yanaadhihirika; watu hutahadhari sana wasiongee kwa njia ambayo inaweza kuchochea wivu wa wenzao. Kwa mfano, ni sawa kumwuliza mtu mafanikio ya watoto wake, kwa kiasi. Ukionekana unataka kujua kupita kiasi, mwenzi wako sio atajiuliza kwa nini? Pengine, watoto wake wakiwa wanaendelea kushinda wako, utakuwa na wivu kwake, na wivu wako utaweza kuwaangamiza watoto wake. Kwa hivyo, hali ya juu ya wivu, inayotokana na hali ya juu ya tamaa, inayoitwa pia uchawi, inazuia aina ya maongezi au uhusiano.

Msingi wa umaskini ni upi? Mara nyingine tunafikiri ni haba ya vitu ndiyo inasababisha kushindana, na penye kushindana juu ya vitu ni ngumu kufanyikisha maendeleo. Lakini, tukiangalia kinyume, je, inawezekana kushindana juu ya vitu ndivyo msingi wa kuwa na mali haba? (Tijimes 1999:200). Wanaoshindana juu ya vitu, ni watu wenye tamaa hali ya juu, wanaoudhiwa kumwona mwenzi wao akifanyikiwa kuwashinda. Kawaida, watu aina hawa, hujua pia watu wengine hufanana nao. Yaani, mimi nikigundua tamaa moyoni wangu ni kwa hali ya juu, sio nikiwaangalia wengine, nitawadhania pia kuwa hivyo? Kwa hivyo, nitajua nikiwa na kitu, wakitamani. Nikiwa na ujuzi huo, nitaogopa kurogwa (kulaumiwa juu ya kile kitu), kulaumiwa ambacho kunaweza kuniumiza. Suluhisho ni kutokuwa na mali, au kuficha mali ulivyonayo. Ndivyo watu hufanye. Wasingekuwa wanaishi na watu wengine ambao wanavitamani vitu vyao, wangejiongezee mali, lakini hali vile ilivyo inafanya waogope. Kwa hivyo, ni tamaa ya hali ya juu inayosababisha umaskini Afrika. Siku hizi WaAfrika wengi wameinuliwa sana kiwango cha maisha yao. Hiyo ni sababu mali inaingizwa kwa wingi kutoka nje. Lakini hali ya kuongezeka mali haiwezi kusuluhisha mambo ya kurogana, sababu bado tofauti intakuwepo kati ya mtu moja na mwingine (Dreher 2019). Pia mali nyingine, kwa mfano

wanawake, hawawezi kutengenezwa kiwanjani. Hawatakuwa zaidi na wanavyozaliwa.

Ukristo unapunguza ushindi juu ya wanawake kwa kuisitiza mtu awe tu na mke mmoja. Injili inatuhimiza turidhike na rasilmali tunayo, na kutumainia uzima wa milele! Yule anayesikia ujumbe huo kwa ndani, kiwango chake cha kutamani vitu vya mwenzake duniani lazima kipungue. Watu wasipoogopana wivu wao kwa wao, ndivyo uongezeko wa mali kupitia maongezo ya rasilmali ya kisasa⁵⁰ utawezeshwa! Ndivyo ni jamii ya Ukristo, hasa wale wa Ulaya, walioanza utengenezaji ya rasilmali kupitia viwanda na mbinu za kisasa. Suluhisho kwa hali ya umaskini kumbe ni kupunguza tamaa ili kuzuia wivu na uharibifu unaoleta (angalia pia Maranz 2011:138-140). (Mtu fulani akipunguza tamaa yake, ataweza amini mwingine pia anaweza kufanya vile vile.) Ikiwa vile, kumbe msaada kutoka Ulaya hayasaidie, ila kinyume chake, kinawezakuwa kinaadhirisha.

Ni rahisi tamaa, penye haba (na kumbuka, tamaa ndiyo inaleta haba ya rasilmali), kuleta vita kati ya watu (Girard 2001:x). ‘Lakini’, wengine wanaweza sema, ‘tunaandaa sherehe mara kwa mara ili watu wote wawe pamoja, ili tuzuie vita visitokee’ (Mauss 1967:11). Ni sawa, sherehe, watu wakila pamoja, inasaidia hali zingine. Lakini hata hivyo, wachawi bado wanatafutwa na kushitakiwa na kuuawa! Kwa hakika, sherehe yenyewe inasaidia kuwatambua wachawi ni wakina nani – hasa wasio hudhuria sherehe hiyo (2008:135).

Ili kupunguza hali ya kusitaki wachawi, kitakacho saidia ni kile kinachoweza kupunguza kiwango cha tamaa. Biblia inatuambia tuitumainie mbingu, tutumainie hali ya kuwa watumishi, tuutumainie ufalme wa Mungu kwanza, nk. Kwa hivyo, kinachoweza kupunguza kiwango cha tamaa ya watu ni imani kwa Kristo.

Nakubali mara nyingine hiyo ya juu inawezekana haitokee sana. Sababu moja, watu wakimfahamu Yesu mwenye mali, wanatamani kufanana naye, ndivyo wanazidi kutamani mali. Wamisionari wengi kutoka Ulaya wamehusika na hali hiyo, yaani mara nyingi wamekuwa wanakuja na mali zaidi kuwagawia watu, na kwa wenyewe kutumia. Hiyo hufunza WaAfrika kuwa na tamaa hali ya juu. Wazungu hutambulika kama wenye mali sana (Reese 2010:63). Wazungu wengine, hata wakiwa WaKristo, siku hizi hawaoni hata maana ya kuwashirikishe WaAfrika sana na Injili. Badala yake wanahusika sana na usambarataji wa mali ya dunia (Harries 2011).

Watu hujifunza kupitia kwa uigizaji (Kaplan 2016). Lakini, watu wakijifunza kupitia kuigizana, vipi maana ya kuwatuma watoto shuleni

⁵⁰ Yaani, *capitalism*, ambayo pia kwa Kiswahili inawezaitwa ubepari, jina ambalo lenyewe linaonyesha jinsi *capitalism* inafahamika.

miaka nyingi? Sawa, watoto watashika maneno mengine wanaoambiwa darasani. Lakini, msingi wa ufahamu wao utazidi kutokea kwa uigizaji. Yaani, wanaojifunza shuleni wataingiza ndani ya msingi ambao ni uigizaji. Ni sababu hata shule zote zikiwa zinafunza kwa njia moja duniani pote, bado yale ambayo wanafunzi watakuwa wanafahamu hayatakuwa sawa. Ndivyo sababu kudhani watu wawili wako na uwezo sawa kulingana tu na elimu yao ya shuleni haina msingi. Siyo elimu inayoweza kumfanya MwAfrika afanane na Mzungu, au Mzungu na MwAfrika! La hashu. Kufikiri hivyo ni upuzi. Maana yake, elimu kwa watu fulani inahitajika ipangwe na watu wanaofahamu muktadha wa hawa watu, ipangwe na ifunzwe kulingana na muktadha wao. Ndivyo sababu – elimu peke yake haileti maendeleo.

Swali nyeti sasa KiAfrika linakuwa, tufanyeje? Kwanza, watu wafunzwe na lugha zao, siyo kupitia lugha ya mgeni. Pili, elimu iwe juu ya msingi wa Neno la Mungu, ili wanafunzi waerevuke na hekima ya ndani, hasa ili waanze kugundua jinsi kulaumiana juu ya matatizo mara nyingi, yaani kumshitaki mchawi, hakina msingi wa ukweli. Mungu ndiye mkuu. Bahati ya watu hutofautiana. Umuhimu ni kuzidi kulishika neno la Bwana, kuzidi kukuwa na imani yo yote ikitokea. Maendeleo siyo kitu rahisi kitakachokuja tu watu wakieleleka kupitia shule zao pasipo Mungu kuwaongoza, na pasipo watu kutubu na kuongoka.

7. Uoga wa nchi za Magharibi wa ukweli wa Mungu

Yaliyoandikwa humo, ni ya kuogofya. Sababu – kwa muda mrefu wakubwa wa dunia wamejaribu kujikimbiza kupitia msingi wa ufahamu ambao hapa tunavuruga. Yaani, msingi wa *modeni*, au msingi wa *sekula*. Mambo yaliyo juu, yakichukuliwa manani, itatubidi tutengue mengi ambayo kwa karibu miaka mia moja nchi za magharibi wamekuwa wamejenga. Maneno hayo yaliyo juu yanaweza kuturudisha katika karne ya kumi na tisa. Wakati wa karne huo wasomi wengi walioheshimika nchi za Ulaya walifahamu na kuamini Neno la Mungu bila kuyeyuka mbele ya wasomi wenzao *wamodeni* (Masuzawa 2005:103). Ni sababu wasomi wengi hawapendi kabisa kuyasikia hekima hiyo ‘mpya’ (ambayo kwa hakika ni ya zamani, lakini imesahaulika) iinuke (Kaplan 2016). Kumbe dini za jadi hazipo bure. Bali zinaitikia hali iliyopo. Na hali hiyo muhimu ambayo wasomi *wamodeni* hawajagundua, wameipuuza wakifikiria hamna kitu hapo. Wakilazimishwa kuigundua, wataweza lia kwa ajili hekima waliokuwa wakiitumia itatambulika siyo hekima hasa tena. Mimi binafsi, namshukuru Mungu sana kwa udhahirisho wake kwa mambo mengi, ambayo pengine nimeweza

kuona kushinda wengine sababu ya kuishi ndani ya jamii ya KiAfrika tangu 1988 mpaka sasa.

Kuna wasomi wengine wanaoitwa wanaanthropologia. Hawa hasa wamejaribu kuwafahamu watu wanaoishi nje ya nchi za magharibi. Lakini kumbe wamefanya kosa moja kubwa la msingi, yaani wamekuwa na udharau juu ya misingi ya dini za watu. Wamewachukua watu wenye dini kama wenye upungufu wa akili (Evans-Pritchard 1964). Kwa hivyo, kwa utafiti wao, wamekuwa wanapuuzwa mambo mengi, hali ambayo sasa inafanya tufae tuuanguka upya maandishi yao. Inaweza kuwa hali ya ufunuo upya ulio juu utasababisha kurudia maswali mengi ambayo awali yalishajibika. Ndivyo sababu Wazungu wengi hushikilia *usekula* na *umodeni*, kama mbwa anashika nyama mdomoni ukijaribu kumtolea (Kaplan 2016)! Lakini, kwa hakika, Ukristo unaigundua dini za jadi zaidi ya wanaanthropologia (Kaplan 2016). Wasomi wangefungua macho yao, wangeona ndivyo ukweli wa mambo. Angalia tu jinsi kanisa la Kristo linakuwa kwa bara la Afrika, kwa ajabu, wakati ni WaAfrika wachache sana wanaokuwa na hamu kujua anthropology (kati ya wachache hawa, kwa karibu wote, hamu ya kujua inalingana na ufanisi ya kifedha wanaotarajia sababu kufanya hivyo itawahusisha na Wazungu). Tunaweza angalia WaIslam. Ndio watu ambao wamepambana dhidi ya Injili kwa miaka nyingi. Pia wamejua, usipopinga Ukristo kwa ukali sana, watu watazidi kuingia kanisani ili wamfahamu Mungu! Kwa msingi, MwIslam amamwua mshirika wao anaye ongoka kuwa Mkristo. Kwan nini? Ili WaIslam wasipoteze waumini wao. Pinga Islam, na unaweza rudiwa na ukatili kali.⁵¹ WaIslam hawangepinga Ukristo mara kwa mara, na kuweka sheria kali ili ilinde dini yao dhidi yake, Ukristo usingekuwa unavuta watu sana. Pasingekuwepo Islam yenye nguvu, makanisa ya WaAfrika yangeshitawi sana zaidi, kama vile imekuwa zamani duniani pote kabla ya udanganyifu wa *modeni* kuingia.

8. Hitimisho

Mijadala yetu hii inadhibitisha ufunuo unaoletwa na msomi mmoja anayeitwa René Girard. Maono yake, tamaa ya watu ni vya vitu vya wengine, na dini za watu huokoa kutoka ukatili wa uchawi, yanaongea moja na moja kwa mazingira ya KiAfrika.

Kile kitu kinachoitwa modeni chenye kilitokea sababu ya injili ya Yesu. Lakini modeni imegeuka wakati huu kuwa udanganyifu kubwa kwa watu wengi. Hapa nimeonyesha jinsi udanganyifu wake unakuwa.

⁵¹ <https://www.ncronline.org/news/world/regensburg-redux-was-pope-benedict-xvi-right-about-islam>

Ninashauri ili mambo ya *umodeni* uwekwe kando na Injili ya Yesu ichukue nafasi yake inayofaa wakati huu. Binadamu wanatakikana watubu wamwamini Yesu. Ili kukamilisha maono hata ya wale *wamodeni* na *wasekula*, ndiyo imani kwa Kristo inayo hitajika. Jinsi wasomi wengi hukatae Injili ni udhaluma ambao haufai kukubaliwa.

Bibliography

- Alison, James, 1996, 'Girard's Breakthrough,' (originally published in The Tablet in 1996) <http://jamesalison.co.uk/texts/eng05.html>
- Andrade, Gabriel, nd. 'René Girard (1923–2015),' *Internet Encyclopedia of Philosophy: a peer reviewed academic resource*. <https://www.iep.utm.edu/girard/>
- Cowdell, Scott, 2013, *René Girard and Secular Modernity: Christ, culture, and crisis*. Notre Dame, Indian: University of Notre Dame Press.
- Cummins, Fred, 2016, 'Lecture 1. History of Cognitive Science. Part 1.' <https://www.youtube.com/watch?v=ZC2dEr4bmPg>
- Dreher, Rod, 2019, 'René Girard and the Covington Catholic Boys', January 27th 2019, www.theamericanconservative.com
- Evans-Pritchard, EE. 1964. 'Religion and the Anthropologist.' 155-171 in: Evans-Pritchard, 1964. *Social Anthropology and Other Essays*. New York: The Free Press.
- Frazer, James George, 1994, *The Golden Bough: A Study in Magic and Religion*. A new abridgement from the second and third editions. Edited and with an introduction and notes by Robert Fraser. Oxford: Oxford University Press.
- Girard, René, 2001, *I See Satan Fall Like Lightning*, Maryknoll: Orbis.
- Girard, René, 2010, *Battling to the End: conversation with Benoît Chantre*. (trans. By Mary Baker) East Lansing: Michigan State University Press.
- Girard, René, 2011, *Sacrifice*. (translated by Matthew Pattilo and David Dawson), East Lansing: Michigan State University.
- Harries, Jim, 2010. 'Mission in a Post Modern World: issues of language and dependency in post-colonial Africa.' In: *Exchange, Journal of Missiological and Ecumenical Research*, 39(4), Brill. 309-330.
- Harries, Jim. 2011. 'Material Provision' or Preaching the Gospel: reconsidering holistic (integral) mission.' 81-98 In: Harries, Jim, 2011.

- Vulnerable Mission; insights into Christian Mission to Africa from a position of vulnerability.* Pasadena: William Carey Library.
- Harries, Jim. 2012. "Witchcraft, Envy, Development, and Christian Mission in Africa." *Missiology: An International Review* 40(2): 129–139.
- Harries, Jim. 2012b, 'The Great Delusion: post-colonial language policy for mission and development in Africa reviewed.' *Transformation, an international journal of holistic mission studies* 29/1, January 2012, 44–61.
- Harries, Jim, 2015a, 'Intercultural Generosity in Christian Perspective: The 'West' and Africa.' *Transformation* 2015, Vol. 32(4) 269–280.
- Harries, Jim, 2015b, *Secularism and Africa: in the light of the Intercultural Christ*, Eugene, Oregon: Wipf and Stock.
- Harries, Jim, 2016, 'Shadow-boxing: the missionary encounter with Christian theology in world religions', *The Pneuma Review, Journal of Ministry Resources and Theology for Pentecostal and Charismatic Ministries & Leaders* <http://pneumareview.com/shadow-boxing-the-missionary-encounter-with-christian-theology-in-world-religions/>
- Harries, Jim, 2018a, 'Overcoming Invented Ogres: African Traditional Religions and World Religions in African Christian Perspective,' 171-184 *Evangelical Review of Theology*, 42:2, 2018.
- Harries, Jim, 2018b, 'Faith, Thought, Science, Secularism and the Gospel of Jesus in relation to Mission to Africa Today', *Faith & Thought*, No. 64, p37-41.
- Harries, Jim, 2018c, *African Heartbeat: and a vulnerable fool*. London: Apostolos Publishing Limited.
- Harries, Jim, 2019, 'Practising Mission and Development in a Multi-lingual African Context of Jostling for Money and Power,' *Evangelical Review of Theology*, (2019) 43:2, 152-166.
- Harrison, Robert Pogue, 2018, 'Evolution of Desire: A life of René Girard by Cynthia L. Haven and six books by René Girard.' *The New York Review of Books*, 20th December 2018, 5.
- Jindra, Michael, 2014, 'The Dilemma of Equality and Diversity,' *Current Anthropology*, 55(3), June 2014, 316-334.
- Jones, Ben, 2013. 'The Making of Meaning: churches, development projects and violence in Eastern Uganda.' *Journal of Religion in Africa*. 43 (2013), 74-95.

9. Masuhulisho ya hali za kulaumiana na kushitakiwa wachawi bara la Afrika 103

- Jones, Ben and Petersen, Marie Juul, 2013, 'Beyond Faith-Based Organisations: critiquing recent work on religion and development.' 1-19 *Third World Quarterly* 4(1-2)
- Kaplan, Grant, 2008, 'Interview with René Girard,' Phone interview conducted October 2008. <https://www.firstthings.com/web-exclusives/2008/11/an-interview-with-rene-girard>
- Kaplan, Grant, 2016, *René Girard; unlikely apologist: mimetic theory and fundamental theology*. Notre Dame, Indiana: University of Notre Dame Press.
- Masuzawa, Tomoko, 2005, *The Invention of World Religions: how European universalism was preserved in the language of pluralism*. London: University of Chicago Press.
- Marcel Mauss, 1967. *The Gift: forms and functions of exchange in archaic societies*. Translated by Ian Cunnison from *Essai sur le don, forme archaïque de l'échange, 1925*. New York: WW Norton and Company Incorporated. http://goodmachine.org/PDF/mauss_gift.pdf (accessed July 20, 2012).
- Mangalwadi, Vishal, 2011, *The Book that made your World: how the bible created the soul of western civilisation*. Nashville, Tennessee: Thomas Nelson.
- Maranz, David, 2001, *African Friends and Money Matters: observations from Africa*. Dallas: SIL International.
- Melland, F.H., 1923, *In Witch Bound Africa: an account of the primitive Kaonde tribe and their beliefs*. Philadelphia: J.B.Lippincott Company.
- Milbank, John, 1990, *Theology and Social Theory: beyond secular reason*. Oxford: Blackwell.
- Moyo, Dambisa, 2010. *Dead Aid: why aid is not working and how there is another way for Africa*. London: Allen Lane, Penguin Books.
- Nongbri, Brent, 2013, *Before Religion: a history of a modern concept*. London: Yale University Press
- Reese, Robert, 2010. *Roots and Remedies of the Dependency Syndrome in World Missions*. Pasadena: William Carey Library.
- Shamala, Lucas, 2008. *The Practice of Ubuntu among the Abaluyia of Western Kenya: a paradigm for community building*. Saabruicken, Germany: VDM Verlag.
- Tempels, Placide, 1959, *Bantu Philosophy*. Paris: Presence Africaine.

- Thatamanil, John, 2015, 'How not to be a religion: genealogy, identity, wonder.' 54-72 in: Johnson-DeBaufre Melanie and Keller, Catherine and Ortega-Aponte, Elias, (eds) *Common Goods: economy. Ecology, and political theology*. New York: Pordham University Press.
- Tijimes, Peter, 1999, 'Desire, Technology, and Politics,' *Contagion* 6, 85-89.
- Trener, David, 2014, 'Alasdair MacIntyre, George Lindbeck and the nature of tradition.' *PhD Thesis*. University of Nottingham.
- Vattimo, Gianni & Girard, René, 2010, *Christianity, Truth, and Weakening Faith. A Dialogue*, (edited by Pierpaolo Antonello, translated by William McCuaig), New York: Columbia University Press.

Sources

Chapter 1

Submitted to Kima International School of Theology Library February 2008 for the

Africa Literature Profile – Maarifa Lecture Presented at Kima International School of Theology on 20th February 2008

By: Jim Harries Mwalimu, Shule ya Mataifa ya Theologia, Kima, Kenya.

Maneno hayo yanalingana na maandishi ya Kiingereza yaliyo chapishwa:

Harries, Jim. 2008. 'A Linguistic Case for the necessity of Enculturation in Theological and Economic Teaching based on the 'Shape of Words': including a case study comparing Sub-Saharan Africa with the West.' *Journal of Intercultural Communication*. Issue 18, October 2008. <http://www.immi.se/intercultural/> ISSN 1404-1634

Chapter 2

Maandishi haya yameandikwa na: Jim Harries (Kima International School of Theology, PO Box 75, Maseno, Kenya. jimoharries@gmail.com tel. 0721 804282) ili yasomwe katika chuo cha Maseno, Institute of Research and Post-Graduate Studies.

Jim Harries (anayeitwa pia Jacob Otieno akiwa nyumbani) ni mmisionari chini ya Church of God, Kenya. Anafundisha katika Shule ya Biblia ya Church of God Kima, na pia kwa Yala Theological Centre, Yala, Gem. Pia ni mwanafunzi wa PhD, Birmingham University, UK.

Tarehe ya uchapishaji: 16.06.04

Chapter 3

Maarifa Lecture

Presented at Kima International School of Theology, on 15th March 2006.

By Jim Harries (KIST P/T Lecturer)

Chapter 4

(The (Im)possibility Of Inter-Cultural Dialogue)

Mahadhara ya Maarifa itakayotolewa kwenye chuo cha kimataifa cha theologia kilicho Kima, Kisumu, Kenya, tarehe 19.09.07 Mnenaji: Dkt. Jim Harries

Maarifa Lecture presented to the students and staff of Kima International School of Theology, Kisumu, Kenya on 19th September 2007. Presenter: Dr. Jim Harries

(Yanalingana na tolea ya Kiingereza inayoitwa: Intercultural Dialogue – an overrated means of acquiring understanding examined in the context of Christian Mission to Africa.)

Chapter 5

Mafunzo Maalum yaliyotolewa Babati Shule ya Biblia, Kanisa la Mungu la Tanzania, Manyara, Tanzania, tarehe 5 mwezi wa pili 2019.

Jim Harries, PhD.

Chapter 6

Mwandishi: Jim Harries, jimoharries@gmail.com Mwezi wa kwanza, 2019.

Nakala kwa Kiingereza imechapishwa hivyo: Harries, Jim, 2016, “To Compromise on Missionary Vulnerability in Africa? – a response to critics of ‘Vulnerable Mission’” *Global Missiology*, 3/13, April 2016. <http://ojs.globalmissiology.org/index.php/english/article/view/1881/4187>

Chapter 7

Mambo kadhaa yamefanya sasa Kiingereza iwe lugha ya kutamaniwa, kufunzwa, kutafutwa, na kutumika kama lugha ya pili au lugha geni (Chowdbury and Ha 2014:14).

Tuna Kiingereza zile zinazo hesabika ‘kawaida’ dunia nzima. ***Kiingereza za wenyeji.***

Tuna ***Kiingereza ingine ya asili*** – waliojifunza lugha hii ni waliozaliwa nchini ambapo lugha hii ni ya asili, kama UK, USA.

Chapter 8

Mafunzo yaliyotolewa Mwanza, kwa wachungaji wa kanisa la Mennonite, 19-21.08.2105

Mwalimu: Jim Harries, PhD.

+254721804282

SLP 932,40610, Yala, Kenya

Chapter 9

Mwandishi: Jim Harries, aliandika mwezi wa tatu 2019.

Juu ya Mwandishi. Jim Harries ameishi na kufanya huduma nchi za Afrika mashariki, hasa kufunza Biblia kupitia lugha za KiAfrika na dhehebu za wenyeji pamoja na kanisa la Orthodoxy ya Koptiki, tangu 1988.